# KUTATHMINI MATUMIZI YA MITINDO NA DHAMIRA KATIKA TAMTHILIYA ZA MASHETANI NA MASHETANI WAMERUDI: UTAFITI LINGANISHI

**SAFIA SAID MASSOUD**

**TASNIFU ILIYOWASILISHWA IKIWA NI SEHEMU YA MASHARTI YA KUTUNUKIWA SHAHADA YA UZAMILI (M.A. KISWAHILI - FASIHI) YA CHUO KUKUU HURIA CHA TANZANIA**

**2018**

# ITHIBATI

Aliyeweka saini hapa chini anathibitisha kuwa ameisoma Tasnifu hii iitwayo: ***Kutathmini Matumizi ya Mtindo na Dhamira katika Tamthiliya za Mashetani na Mashetani Wamerudi: Utafiti Linganishi:***na kupendekeza ikubaliwe na Chuo Kikuu Huria cha Tanzania kwa ajili ya kukamilisha masharti ya Digrii ya Uzamili katika Kiswahili ya Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

...............................................

Prof. Emmanuel Mbogo

(Msimamizi)

................................................

Tarehe

# HAKIMILIKI

Hairuhusiwi kuiga au kunakili kwa njia yoyote ile, iwe ama kazi nzima au sehemu ya Tasnifu hii, isipokuwa /shughuli halali, kwa ajili ya utafiti, kujisomea, au kufanya marejeo ya kitaaluma bila kibali cha maandishi cha Mkuu wa Kurugenzi ya Taaluma za Uzamili kwa niaba ya Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

# IKIRARI

Mimi, **Safia Said Massoud,** nathibitisha kwamba tasinifu hii ni kazi yangu binafsi na halisi na kwambahaijawahi kuwasilishwa na wala haitawasilishwa, katika Chuo Kikuu kingine kwa ajili ya kutunukiwaShahada yaUzamili auShahada nyengine yoyote.

………………………

Saini

………………………….

Tarehe

# TABARUKU

Kwa heshima na udhati wa moyo wangu, natabaruku kazi hii kwa marehemu baba yangu mpenzi Bw. Said Massoud Said na na marehemu mama yangu Bi. Bimkubwa Jaffar Khamis. Natamani sana leo hii mungeshuhudia mafanikio yangu! Pumzikeni kwa amani Allah akuhifadhini mahali pema peponi Amin. Mume wangu kipenzi Bw. Bakar Ali Omar nakwa watoto wangu; Hemed Bakar Ali, Munawarat Bakar Ali, Ifadat Bakar Ali, Jokha Bakar Ali, Nuaira Bakar Ali na Nadia Bakar Ali.

## SHUKURANI

Kwanza kabisa kabla sijasema neno lolote, napenda nitoe shukrani zangu zisizo na ukomo kwa ALLAH SUBHANAHU WATAALAH kwa sababu yeyé ndiye Mkuu na anayepaswa kushukuriwa kwa hatua yoyote ya maisha ya mwanadamu. Ninamshukuru kwa kunijaalia afya njema kipindi chote cha masomo yangu, kunipa nguvu, uwezo, akili, busara na maarifa katika kipindi chote cha masomo yangu ya uzamili. Nasema kwa unyenyekevu, Alhamdulillah Rabbilaalamina.

Pili, nawashukuru sana wazazi wangu wapenzi: Marehemu mama yangu Bimkubwa Jaffar Khamis na maehemu baba yangu Said Massoud Said kwa kunizaa, kunilea, kunisomesha, na kunifunza kuhusu malimwengu na ulimwengu. Mwenyezi Mungu azilaze roho zao mahala pema peponi, Amina. Vile vile, shukrani za pekee ni kwa mume wangu kipenzi Bw. Bakar Ali Omar kwa uvumilivu wake, huruma na kunitia moyo pale nilipokata tamaa.

Tatu, napenda kutoa shukrani zangu za dhati na zisizo ukomo zimikie Msimamizi wangu Prof. Emmanuel Mbogo kwa kunilea kitaaluma na kunikuza katika misingi ya nadharia na vitendo katika fasihi ya Kiswahili. Sina neno linalofaa kutoa shukrani zangu kwake bali namuombea afya njema na maisha marefu ili aendelee kutoa msaada na kulisukuma mbele gurudumu hili la kitaaluma kwa wanafunzi wanaohitaji maarifa zaidi na wao watoe mchango kwa taifa hili na jamii yetu kwa ujumla.

Nne, shukrani zangu za pekee ziwafikie uongozi mzima wa Chuo Kikuu Huria Cha Tanzania, kuanzia makao makuu hadi hapa Pemba. Aidha napenda kuwashukuru wote waliosaidia kwa hali moja au nyengine hadi nikafika hapa. Kwa vile ni wengi,

kwa heshima kubwa naomba niwataje wachache.Nawashukuru sana, Dkt.Mohamed, Bw. Bakar Kombo, Prof. Sengo, Dkt. Hadija Jilala, Dkt. Hilda Pembe wa Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.Pia, nawashukuru wanaidara wote wa idara ya Isimu na Taalimu za Fasihi kwa maoni na miongozo yao hadi leo nimefanikiwa,bila kuwasahau Bw. Ali Mussa na Bw. Sharif Juma Fakih kwa ushauri wao wa mara kwa mara.

## IKISIRI

Utafiti huu unahusu Kutathmini matumizi ya Mitindo na Dhamira katika Tamthiliya ya *Mashetani* na *Mashetani Wamerudi*. Utafiti huu ni wa maktabani ambao ulitumia sampuli lengwa nakuongozwa na Nadharia yaMuingilianomatini na Nadharia yaFasihi linganishi.Utafiti uligundua kuwa tamthiliya ya *Mashetani* imetumia vipengele vya kimtindo vinavyohusiana na matumizi ya lugha kama vile uteuzi wa msamiati pamoja na matumizi ya tamathali za semi. Mbinu nyenigine za kimtindo zilizotumika katikaTamthiliya za *Mashetani* na *Mashetani Wamerudi* mbinu hizo ni kama vile mandhari za fasihi simulizi, mtindo wa nyimbo, masimulizi, matumizi ya nafsi zote, majigambo, dayalojia na mtindo wa tamthiliya za majaribio. Piatamthiliya zote zimelingana kwa kutumia mtindo wa mashairi, nyimbo, majigambo, matumizi ya nafsi, mandhari ya fasihi simulizi, wahusika wa fasihi simulizi, matumizi ya ndoto, tamthiliya ya majaribio na mtindo wa masimulizi. Vile vile, zimelingana katika kutumia methali, nahau, misemo, jazanda, ishara, taswira na tamathali za semiImegundulikakuwa kuna tofauti ndogo kati ya tamthiliya teule ambapo*Mashetani* imetumia mchezo ndani ya mchezo ambapo mtindo huu hauko katika *Mashetani Wamerudi*. Taswira kama vile punda, jogoo, simba, batamzinga, kuku hazijitokezi katika tamthiliya ya *Mashetani.*Aidha, utafiti umegundua kuwa kuna kufanana kwa dhamira katika Tamthiliya teule. Tamthiliya hizi zimejadili dhamira za ukoloni mamboleo, harakati za ukombozi, ujenzi wa jamii mpya, nafasi ya mwanamke, matabaka, uongozi mbaya na ubadhirifu wa mali za umma, ukosefu wa demokrasia na elimu ya Kimagharibi. Pia, kunadhamira ya utandawazi, kujitoa mhanga, umoja na mshikamano, athari za utandawazi na ukosefu wa ajira hazijitokezi katika Tamthiliya ya *Mashetani.*

# YALIYOMO

ITHIBATI ........................................................................................................... ii

HAKIMILIKI ........................................................................................................ iii

IKIRARI iv

TABARUKU ......................................................................................................... v

SHUKURANI ....................................................................................................... vi

IKISIRI viii

ORODHA YA MAJEDWALI ............................................................................. xvii

SURA YA KWANZA ........................................................................................... 1

UTANGULIZI WA JUMLA ................................................................................. 1

1.1 Utangulizi ......................................................................................................... 1

1.2 Usuli wa Mada ya Utafiti ................................................................................ 1

1.3 Tatizo la Utafiti ................................................................................................ 5

1.4 Malengo ya Utafiti ........................................................................................... 6

1.4.1 Lengo Kuu ...................................................................................................... 6

1.4.2 Malengo Mahsusi ya Utafiti ........................................................................... 6

1.5 Maswali ya Utafiti ........................................................................................... 6

1.6 Umuhimu wa Utafiti ........................................................................................ 7

1.7 Mawanda ya Utafiti ......................................................................................... 8

1.8 Vikwazo vya Utafiti na Utatuzi wa Vikwazo .................................................. 9

1.9 Hitimisho ......................................................................................................... 9

**SURA YA PILI ....................................................................................................10**

**MAPITIO YA KAZI TANGULIZI NA MKABALA WA KINADHARIA.........10**

2.1 Utangulizi ....................................................................................10
2.1 Maana ya Tamthiliya ........................................................................10
2.2 Historia fupi ya Tamthiliya ...............................................................12
2.3 Mapitio ya Maandiko .........................................................................15
2.3.1 Maandiko Kuhusu Dhana ya Fasihi Linganishi ...................................16
2.4 Vipengele vya Ulinganisho ................................................................19
2.5 Mtindo katika Kazi za Fasihi .............................................................20
2.6 Vipengele vya Kimtindo katika Fasihi Linganishi ...............................21
2.7 Dhana ya Dhamira .............................................................................22
2.8 Kazi Tangulizi kuhusu Mtindo katika Tamthiliyaza Kiswahili .................24
2.9 Kazi Tangulizi kuhusu Tamthiliya Teuliwa..........................................27
2.10 Pengo la Maarifa.................................................................................29
2.11 Mkabala wa Nadharia .........................................................................29
2.11.1 Nadharia ya Mwingilianomatini..........................................................30
2.11.2 Nadharia ya Fasihi Linganishi.............................................................32
2.12 Hitimisho...........................................................................................36
**SURA YA TATU .........................................................................................37**
**MBINU ZA UTAFITI .................................................................................37**
3.1 Utangulizi............................................................................................37
3.2 Eneo la Utafiti ....................................................................................37
3.3 Usanifu wa Utafiti ..............................................................................38
3.4 Kundi Lengwa ....................................................................................38
3.5 Sampuli na Usampulishaji ..................................................................39
3.6 Ukusanyaji wa Data............................................................................40

3.6.1 Data za Msingi....40
3.6.2 Data za Upili....41
3.7 Mbinu za Kukusanya Data....42
3.7.1 Upitiaji wa Nyaraka....42
3.7.2 Usomaji Makini wa Nyaraka....43
3.8 Mkabala wa Uchambuzi wa Data za Utafiti....44
3.9 Usahihi, Kuaminika na Maadili ya Utafiti....45
3.9.1 Usahihi wa Data....45
3.9.2 Kuaminika kwa Data za Utafiti....45
3.9.3 Maadili ya Utafiti....45
3.10 Hitimisho....46
**SURA YA NNE....47**
**UWASILISHAJI, UCHAMBUZI NA MJADALA WA DATA ZA UTAFITI....47**
4.1 Utangulizi....47
4.2 Muhtasari wa Tamthiliya ya *Mashetani*....48
4.3 Muhtasari wa Tamthiliya ya *Mashetani Wamerudi*....48
4.4 Vipengele vya Mtindo katika Tamthiliya ya *Mashetani*....49
4.4.2 Mpangilio wa Maneno katika *Mashetani*....50
4.4.3 Matumizi ya Lugha katika *Mashetani*....51
4.4.3.1 Matumizi ya Jazanda katika Mashetani....52
4.4.3.1.1 Jazanda ya Ukweli....52
4.4.3.1.2 Jazanda ya Kisu....53
4.4.3.1.3 Jazanda ya Neno "Chewa"....53
4.4.3.1.4 Jazanda ya Neno "w*altz*" na "*Gashalazeritwas*"....54

4.4.3.1.5 Jazanda ya Neno “Mheshimiwa” ....................................................55
4.4.3.1.6 Jazanda ya Neno “Bwana”..........................................................55
4.4.3.2 Mbinu ya Kiishara katika Mashetani..............................................56
4.4.3.3 Mbinu ya Kitaswira katika *Mashetani*...........................................58
4.4.3.4 Mbinu ya Uteuzi na Matumizi ya Tamathali za Semi katika *Mashetani*....59
4.4.3.4.1 Tashibiha.........................................................................60
4.4.3.4.2 Tashihisi.........................................................................61
4.4.3.4.3 Takriri...........................................................................61
4.4.3.4.4 Tanakali Sauti....................................................................62
4.4.3.4.5 Mubalagha.........................................................................63
4.4.3.4.6 Kejeli............................................................................63
4.4.3.4.7 Sitiari...........................................................................64
4.4.3.4.8 Majazi............................................................................65
4.4.3.5 Mdokezo.............................................................................65
4.4.3.6 Nidaa...............................................................................66
4.4.3.7 Mchanganyo Ndimi.....................................................................67
4.4.3.8 Mbinu Nyingine za Kimtindo katika *Mashetani*.................................68
4.4.3.8.1 Mandhari za Fasihi Simulizi.......................................................69
4.4.3.8.2 Mtindo wa Kishairi................................................................69
4.4.3.8.3 Mtindo wa Nyimbo..................................................................70
4.4.3.8.4 Mtindo wa Masimulizi...............................................................71
4.4.3.8.5 Mtindo wa Matumizi ya Nafsi........................................................72
4.4.3.8.6 Matumizi ya Nafsi ya Kwanza.......................................................72
4.4.3.8.7 Matumizi ya Nafsi ya Pili.........................................................73

4.4.3.8.8 Matumizi ya Nafsiya Tatu....73
4.4.3.8.9 Mtindo wa Matumizi ya Dayalojia....74
4.4.3.8.10 Mtindo wa Majigambo....74
4.4.3.8.11 Mtindo wa Tamthiliya ya Majaribio....75
4.5 Mtindo Katika *Mashetani Wamerudi*....76
4.5.1 Uteuzi wa Msamiati....77
4.5.2 Matumizi ya Lugha katika Mashetani *Wamerudi*....78
4.5.2.1 Matumizi ya Jazanda katika *Mashetani Wamerudi*....79
4.5.2.1.1 Jazanda ya Jogoo....79
4.5.2.1.2 Jazanda ya Mbuyu....79
4.5.2.1.3 Jazan/da ya Neno Waltz....79
4.5.2.1.4 Jazanda ya Neno Shetani....80
4.5.2.2 Matumizi ya Kiishara katika *Mashetani Wamerudi*....80
4.5.2.3 Taswira katika *Mashetani Wamerudi*....81
4.5.2.4 Misemo katika *Mashetani Wamerudi*....82
4.5.2.5 Methali katika *Mashetani Wamerudi*....83
4.5.2.6 Nahau katika *Mashetani Wamerudi*....84
4.5.2.7 Uteuzi na Matumizi ya Tamathali za Semi katika *Mashetani Wamerudi*....85
4.5.2.7.1 Tashibiha....86
4.5.2.7.2 Tashihisi....87
4.5.2.7.3 Sitiari....87
4.5.2.7.4 Takriri....88
4.5.2.8 Majazi....89
4.5.2.9 Mdokezo....90

4.5.2.10 Nidaa ....................................................................................91
4.5.2.11 Mchanganyo Ndimi ..........................................................................92
4.5.2.12 Kweli Kinzani katika *Mashetani Wamerud*i .........................................93
4.5.2.13 Mjalizo katika *Mashetani Wamerudi*...................................................94
4.5.2.14 Karaha katika *Mashetani Wamerudi*...................................................95
4.5.2.15 Matumizi ya Lahaja katika *Mashetani Wamerudi*...................................95
4.5.2.3 Mbinu Nyengine za Kimtindo katika *Mashetani Wamerudi* ......................96
4.5.2.3.1 Mtindo wa Nyimbo katika *Mashetani Wamerudi*....................................97
4.5.2.3.2 Matumizi ya Ndoto*Mashetani Wamerudi*...............................................99
4.5.2.3.3 Mtindo wa Masimulizi katika *Mashetani Wamerudi* ...............................99
4.5.2.3.4 Mtindo wa Matumizi ya Nafsi katika *Mashetani Wamerudi* ...............100
4.5.2.3.4.1Mtindo wa Nafsi ya Kwanza ...............................................................100
4.5.2.3.4.2 Mtindo wa Nafsi ya Pili.....................................................................100
4.5.2.3.4.3Mtindo wa Nafsi ya Tatu.....................................................................101
4.5.2.4 Mtindo wa Kutumia Wahusika wa Fasihi Simulizi katika *Mashetani Wamerudi* ......................................................................................101
4.5.2.5 Mtindo wa Mandhari za Kifasihi Simulizi katika *Mashetani Wamerudi* ......................................................................................102
4.5.2.6 Mtindo wa Majigambo katika *Mashetani Wamerudi* ..............................103
4.5.2.7 Mtindo wa Tamthiliya ya Majaribio katika *Mashetani Wamerudi* ..........103
4.6 KulingananaKutofautianakwa Mitindoya tamthiliya ya*Mashetani naMashetani Wamerudi*......................................................................104
4.6.1 Ulinganishi na Ulinganuzi katika Sifa za Kimtindo katika Mashetani na *Mashetani na Mashetani Wamerudi* ............................105

4.6.1.1 Kufanana Mitindo ya Mashetani na *Mashetani Wamerudi* ......................106

4.6.1.1.1 Kufanana kwa Mbinu Nyengine za Kimtindo katika Tamthiliya Teule ....107

4.6.1.2 Kutofautiana kwa matumizi ya Mtindo katika TamthiliyaTeule ..............109

4.6.2 Kufanana kwa Dhamira katika Tamthiliya Teule ...................................111

4.6.2.1 Matabaka ..........................................................................................112

4.6.2.2 Ubadhirifu wa Mali za Umma................................................................114

4.6.2.3 Ujenzi wa Jamii Mpya ..........................................................................116

4.6.2.4 Nafasi ya Mwanamke ...........................................................................118

4.6.2.5 Uongozi Mbaya ....................................................................................120

4.6.2.7 Ukosefu wa Demokrasia .......................................................................123

4.6.2.8 Elimu ya Kimagharibi..........................................................................125

4.6.2.9 Ukoloni Mamboleo................................................................................126

4.6.3 Kutofautiana kwa Dhamira katikaTamthiliya teule.................................128

4.6.3.1 Dhuluma na Uonevu .............................................................................129

4.6.3.2 Kujitoa Mhanga ....................................................................................130

4.6.3.3 Umoja na Mshikamano .........................................................................131

4.6.3.4 Athari za Utandawazi............................................................................133

4.6.3.5 Ukosefu wa Ajira...................................................................................135

4.6.3.6 Ufisadi (Rushwa) ..................................................................................136

4.7 Hitmisho....................................................................................................137

**SURA YA TANO .........................................................................................139**

**MUHTASARI, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO ........................................139**

5.1 Utangulizi..................................................................................................139

5.2 Muhtasari ..................................................................................................139

5.2.1 Dhumuni Mahususi la Kwanza ..... 141
5.2.2 Dhumuni Mahususi la Pili ..... 143
5.2.3 Dhumuni Mahususi la Tatu ..... 145
5.2.4 Ufafafu wa Nadharia ..... 146
5.3 Hitimisho ..... 146
5.4 Mapendekezo ..... 147
5.4.1 Kwa Watafiti ..... 147
5.4.2 Kwa Serikali ..... 148
**MAREJELEO ..... 149**

## ORODHA YA MAJEDWALI


Jedweli Na. 4.1: Matumizi ya Lugha katika Mashetani........................................51

Jedweli Na. 4.2: Ishara katika Tamthiliya ya Mashetani ......................................57

Jedweli Na. 4.3: Matumizi ya Taswira katika *Mashetani*......................................59

Jedweli Na. 4.4: Tamathali za Semi katika Tamthiliya ya *Mashetani*.....................59

Jedweli Na. 4.5: Sitiari na Maana Zake katika *Mashetani*....................................64

Jedweli Na. 4.6: Mchanganyo Ndimi na Maana Zake ..........................................67

Jedweli Na. 4.7: Mbinu Nyengine za Kimtindo katika *Mashetani*..........................68

Jedweli Na. 4.8: Matumizi ya Lugha katika *Mashetani Wamerudi*.........................78

Jedweli Na. 4.9: Ishara na Maana zake katika *Mashetani Wamerudi*......................81

Jedweli Na. 4.10: Taswira na Maana zake katika *Mashetani Wamerudi*...................82

Jedweli Na. 4.11: Tamathali za Semi katika *Mashetani Wamerudi* ..........................85

Jedweli Na. 4.12: Matumizi ya Mbinu Nyingine za Kimtindo katika *Mashetani Wamerudi* .......................................................................96

Jedweli Na. 4.13: Mitindo ya Lugha inavyofanana katika *Mashetani na Wamerudi*.........................................................................106

Jedweli Na. 4.14: Mbinu Nyengine za Kimitindo Zinazofanana ............................108

Jedweli Na. 4.15: Matumizi ya Kimtindo yanavyotofautisha *Mashetani* na *Mashetani Wamerudi*.........................................................110

Jedweli Na. 4.16: Kufanana kwa Dhamira katika Mashetani na *Mashetani Wamerudi* ...................................................................112

Jedweli Na. 4.17: Kutofautiana kwa Dhamira za *Mashetani* na *Mashetani Wamerudi* ...................................................................129

# SURA YA KWANZA

# UTANGULIZI WA JUMLA

## 1.1 Utangulizi

Utafiti huu unahusu *Kutathmini Matumizi ya Mtindo na Dhamira katika Tamthiliya za Mashetani na Mashetani* Wamerudi*: Utafiti Linganishi.* Sura hii ni sura ya utangulizi inayobainisha usuli wa tatizo la utafiti lililofanyiwa uchunguzi katika utafiti huu. Kwa hivyo, sura hii inabainisha n yayaa kueleza usuli wa tatizo, tatizo la utafiti, malengo ya utafiti, maswali ya utafiti ambayo utafiti huu ulikusudia kuyafikia na maswali ambayo utafiti umeazimia kuyajibu, umuhimu wa utafiti, vikwazo na utatuzi wa vikwazo hivyo.

## 1.2 Usuli wa Mada ya Utafiti

Mara nyingi unaposanii kazi za fasihi ya mwandishi au msanii fulani, bila shaka kunahitajika mvuto na mnato katika kazi hiyo. Mvuto na mnato ni vipengele muhimu ili kumfanya msomaji ama msikilizaji avutike. Chemchemu ya mvuto wa kisanii hutokana na umakini na ubobezi wa mtunzi unaochapuzwa na matumizi ya mbinu za kisanii, mtindo ukiwemo ambao ndio nyenzo kuu katika kusanii kazi za fasihi.

Dhana ya mtindo katika kazi ya fasihi imekuwa ikijadiliwa kwa mitazamo tofauti miongoni mwa wataalamu wa fasihi. Wapo wanaouona mtindo kama ni upekee alionao mtunzi wa kazi ya fasihi. Pia, wapo wanaouona mtindo kuwa ni namna ya kuwasilisha dhamira za mtunzi na wengine huona kuwa mtindo ni utofauti uliopo kati ya mtunzi mmoja na mtunzi mwingine katika kusanii kazi ya fasihi. Mathalani,

Murry (1922:519) anaeleza kuwa mtindo ni jumla ya kila kitu kinachofanya maandishi ya mtu kutambulika. Anaendelea kufafanua kuwa mtindo ni matokeo ya moja kwa moja ya jinsi mtu anavyojieleza kulingana na tajriba yake katika kujifunza lugha.

Kwa upande wa Cristal na Davy (1967:10) wanafafanua neno mtindo kulingana na mitazamo minne, ambapo wanaona kuwa ni tabia za mtu katika matumizi ya lugha, tabia ya kimakundi katika matumizi ya lugha, mtindo kama tathmini yaani kiupimaji na mwisho wanauona mtindo kama upekee kulingana na lugha ya kifasihi.

Enkivist (1922:29) anaeleza kwamba mtindo mara nyingi huhusiana na vipengele vya kiisimu katika muktadha, mazingira ambamo hutokea. Kwa kuangalia mtindo wa matini mara nyingi vipengele mbali mbali vya kiisimu vya viwango tofauti lazima vilinganishwe na sifa zinazofanana katika matini nyengine na zinazochukuliwa kama kanuni yenye uhusiano wa kimuktdha na matini hiyo.

Njogu na Chimerah (2008) wanasema kwamba mtindo ni tabia ya utungaji inayopambanua mtunzi mmoja na mwengine. Ni dhana inayoelezea sifa zinazobainisha kazi fulani na kuitenga na kazi nyenginezo. Aidha, wanaendelea kueleza kuwa mtindo humtambulisha mtunzi anayehusika. Mawazo ya Njogu na Chimerah (wameshatajwa) yanatupa mwanga kwa kuona upeo wa kazi fulani ya mtunzi husika. Aidha, kazi hiyo itajikita katika utanzu husika pamoja na mtunzi husika. Hii ni kusema kuwa mtindo huweza kutafautiana kutegemea utanzu unaoshughulikiwa na mtunzi.

Msokile (1993), akimnukuu Senkoro (1987), anasema kwamba mtindo ile namna ambayo mwanasanaa huipa kazi yake ya fasihi sura ya kifani na ya kimaudhui kwa njia ambayo msanii mwengine asingeweza kuipa hata jambo linaloongelewa na wasanii hawa wawili ni lile lile moja. Anaendelea kusema kwamba mwandishi hutumia tajriba yake ya elimu, uzoefu na hata makaazi kuyasuka maudhui yake kwa njia ya upekee ili kuzuka na uyeye katika kazi fulani.

Madumulla (2009), anaeleza kuwa mtindo ni kipengele cha fani ambacho huonesha kazi ya sanaa namna ilivyosimuliwa. Kifaa kinachotumika zaidi katika kujadili mtindo wa fasihi ni lugha na jinsi ilivyotumika. Jilala (2016), anaona kuwa mtindo ni tabia ya mtu na mwengine katika uzalishaji wa kazi za kisanaa. Sifa hii ni ya kipekee ambayo mtunzi huwa nayo na hata kama mtu mmoja anaiga au kuathiriwa na mtunzi asili.

Kwa ujumla katika utafiti huu, mtafiti anaunga mkono mawazo ya Jilala (2016), kwamba mtindo katika kazi za fasihi hujibainisha katika sifa anuai kama vile; uteuzi wa msamiati wa mtunzi, miundo na mpangilio wa sentensi, uteuzi wa matumizi ya tamathali za usemi na jazanda, usawiri wa wahusika, motifu na dhamira zinazokaririwa katika kazi za watunzi, usimulizi na mbinu za usimulizi wenyewe na sifa ya uakifishi. Kwa msingi huo mawazo ya Jilala (ameshatajwa), yalikuwa nyenzo kuu katika kutathmini mitindo ya Tamthiliya teule za *Mashetani* na *Mashetani Wamerudi.*

Tamthiliya ya *Mashetani*ni ni tamthiliya iliyotungwa na E. Hussein. Hii nimiongoni mwa tamthiliya za majaribio ambayo mtunzi wa tamthiliya hiyo alileta upya wa

kimtindo ukilinganisha na tamthiliya za wakati wa ukoloni. Tamthiliya hii ilichota ujumi wa vipengele vya kisanii vya Mwafrika na hivyo kuifanya ionekane tofauti. Pia, kidhamira tamthiliya hii inajikita zaidi kujadili utabaka uliojengwa na wakoloni dhidi ya mtu mweusi.

Aidha, tamthiliya ya *Mashetani Wamerudi* ni tamthiliya iliyotungwa na Said Ahmedi Mohamed. Tamthiliya hii ni picha inayotokana na tamthiliya ya *Mashetani*. Kama asemavyo mtunzi wa tamthiliya hii katika dibaji ya tamthiliya ya *Mashetani Wamerudi* kuwa, tamthiliya ya *Mashetani Wamerudi* ni umbo jipya linalotokana na tamthiliya ya *Mashetani* ya E. Hussen (Mohamed, 2016). Umbo hili limeangazia dhana ya ukoloni katika miktadha ya ulimwengu wa utandawazi pamoja na mitindo ya kuwatumia wahusika wasomi waliobobea kama vile mhusika Prof. ambaye ana uwezo mkubwa wa kuchambua, kuweka wazi na kuwaelimisha wengine juu ya vitimbi vya wakoloni.

Sababu zilizomsukuma mtafiti kufanya utafiti huu ni kuwa hadi sasa hajaona utafiti uliowahi kufanyika kwa nia ya kutathmini matumizi ya mtindo na dhamira katika Tamthiliya ya *Mashetani* ya Ebrahim Hussein ikilinganishwa na tamthiliya ya *Mashetani Wamerudi* ya Said Ahmed Mohammed kwa mkabala wa Fasihi Linganishi na Muingilianomatini. Pia, kutokana na umaarufu wa tamthiliya ya *Mashetani* na usasa wa Tamthiliya ya *Mashetani Wamerudi* ilimsukuma mtafiti kufanya utafiti huuili kuona huo usasa anaoueleza msanii wa tamthiliya ya *Mashetani Wamerudi.*Kupitia dhamira utafiti huu ulifanyika ili kubaini wapiwakoloni (mashetani) walikwenda?, wamerudi kwa vipi?, Je, walirudi kufuata nini?

Hivyo basi, mtafiti ameona kuwa bado ipo nafasi inayohitaji kufanyiwa kazi. Kwa mantiki hiyo, katika utafiti huu mitindo na dhamira ilitathminiwa kama ilivyojidhihirisha katikaTamthiliya ya *Mashetani ya* Ebrahim Hussein na tamthiliya ya *Mashetani Wamerudi* ya Said Ahmed Mohammed kwa kutumia nadharia ya fasihi linganishi na Nadharia ya Mwingilianomatini.

## 1.3 Tatizo la Utafiti

Mtindo ni tabia ya mtu binafsi inayomtofautisha na mtu mwengine katika uzalishaji wa kazi za kisanaa. Sifa hii ni ya kipekee ambayo mtunzi huwa nayo na hata kama mtu mmoja anaiga au kuathiriwa na mtunzi asili (Jilala, 2016). Watafiti kama vile Salem (2013), Maina (2013), Vutagwa (2013), Onchangu (2013), Muthoni (2014), Ngesa na wenzake (2015), Jilala (2016), wamewahi kufanya utafiti unaohusu kuchunguza mitindo katika fasihi ya Kiswahili. Mathalani, Salem (2013), alifanya utafiti linganishi wa vipengele vya fani na maudhui katika tamthiliya za *Mashetani* na *Kivuli Kinaishi*. Katika utafiti huo Salem alifikia hitimisho kwamba, tamthiliya hizo zimelingana na kutofautiana katika vipengele vya fani na maudhui.

Ngesa na wenzake (2015), walifanya uchambuzi wa Tamthiliya ya *Mashetani* na *Kijiba cha Moyo* kwa mkabala wa Mwingilianomatini. Vipengele walivyovishughulikia ni mwingiliano matini wa kimaudhui na kijazanda. Walifikia hitimisho kwamba tamthiliya ya *Mashetani* na *Kijiba cha Moyo* zina mwingilianomatini kama pande mbili za sarafu moja. Hivyo, tamthiliya ya *Kijiba cha Moyo*imeifanya Tamthiliya ya *Mashetani* ieleweke zaidi.

Hivyo, tatizo letu la utafiti lilikuwa ni kutaka kuona jinsi Tamthiliya za *Mashetani* na *Mashetani Wamerudi* zinavyofanana na kutofautiana katika matumizi ya mtindo na dhamira kwa kutumia mkabala wa mwingilianomatini na fasihi linganishi.

## 1.4 Malengo ya Utafiti

Utafiti huu una lengo kuu na malengo mahususi yafuatayo:

### 1.4.1 Lengo Kuu

Lengo kuu la utafiti huu ni kutathmini Matumizi ya Mtindo na Dhamira katika Tamthiliya za *Mashetani* na *Mashetani Wamerudi*: *Utafiti Linganishi.*

### 1.4.2 Malengo Mahsusi ya Utafiti

Utafiti huu uliongozwa na malengo mahsusi yafuatayo:

(i) Kubainisha matumizi ya mitindo katika Tamthiliya teule za *Mashetani* na *Mashetani Wamerudi.*

(ii) Kulinganisha na kulinganua matumizi ya mitindo katika Tamthiliya za *Mashetani* na *Mashetani Wamerudi.*

(iii) Kulinganisha na kulinganua dhamira zinazojitokeza katika Tamthiliya teule za *Mashetani* na *Mashetani Wamerudi.*

## 1.5 Maswali ya Utafiti

Utafiti huu uliongozwa na maswali ya utafiti yafuatayo:

(i) Ni mitindo gani iliyotumika katika uwasilishaji wa tamthiliya teule za *Mashetani* na *Mashetani Wamerudi*?

(ii) Ni jinsi gani mitindo inafanana na kutofautiana katika tamthiliya za *Mashetani na Mashetani Wamerudi?*

(iii) Ni dhamira zipi zinazolingana na kutofautiana katika tamthiliya teule za *Mashetani* na*MashetaniWamerudi*?

## 1.6 Umuhimu wa Utafiti

Utafiti huu una umuhimu katika maeneo yafuatao:

**Kitaaluma:** Matokeo ya utafiti huu yametarajiwayatakuwa marejeleo muhimu kwa wasomi wa ngazi zote za taaluma ya fasihi na fani nyenginezo stahiki. Matumaini ya mtafiti ni kuwa wanafunzi, walimu, wahadhiri, wakufunzi na wasomi wengine wa kazi za fasihiwataweza kutumia utafiti huu kama ni nyongeza muhimu katika kazi mbalimbali za kitaaluma kwa mujibu wa mahitajio ya kazi husika. Sambamba na hilo watumiaji wa utafiti huuwatayatumia matokeo yake kuwa ni sehemu ya marejeleo yao ya kukamilisha malengo na madhumuni ya utafiti wao watakaokuwa wanaufanya. Aidha, matokeo ya utafiti huu yatatumika kama sehemu ya kujiimarisha, ili kubainisha pengo la maarifa ambalo wao watalijaza katika utafiti wao.

**Kinadharia:** Utafiti huu utatoa uthibitisho kwamba, nadharia za uhakiki wa fasihi zinapotumika kuhakiki kazi za fasihi huifanya kazi hiyo kuwa imara na yenye mashiko ambayo huaminika kitaaluma. Kupitia utafiti huu watafiti wa baadaye wataona umuhimu wa kutumia nadharia ya Fasihi Linganishi na Nadharia ya Mwingilianomatini katika uchambuzi wa kazi za fasihi. Hivyo, nadharia hizi zimejidhihirisha katika kazi hii kivitendo, jambo ambalo linatoa dira na mwongozo

katika uchambuzi wa kazi za fasihi hasa katika uwanja wa kutathmini mitindo na dhamira kwa mkabala wa kiulinganishi na mwingilianomatini.

**Kisera:** Utafiti huu unaeleza matatizo mengi ya kijamii ambayo yanaikumba jamii kwa sasa kama vile, masuala ya elimu, matabaka na umasikini, ukoloni na matatizo ya será ya utandawazi na ukoloni mamboleo kwa kadri matatizo hayo yalivyojadiliwa katika kazi za waandishi teule. Aidha, utafiti huu utawafaa katika kuainisha mambo ambayo yanastahili kuingizwa katika sera na kufanyiwa utekelezaji ili kuimarisha mipango ya utekelezaji wa mikakati ya kimaendeleo kwa manufaa ya ujenzi wa jamii mpya endelevu.

## 1.7 Mawanda ya Utafiti

Utafiti huu ulijikita kutathmini matumizi ya mtindo na dhamira katika katika Tamthiliya za *Mashetani ya* Ebrahim Hussein na *Mashetani Wamerudi* ya Said Ahmed Mohamed katika mkabala wa ulinganishi.Pamoja na kuwepo waandishi na watunzi wengi wa tamthiliya za Kiswahili haikuwa rahisi kuchunguza Tamthiliya zote. Hivyo utafiti huu ulijikita katika kuchunguza na kuchambua tamthiliya ya *Mashetani* ya Ebrahim Hussein na*Mashetani Wamerudi* ya Said Ahmed Mohamed.Mtafiti amewachaguwa waandishi hawa kwa sababu wasanii hawa wanazo atharikubwa katika fasihi ya Kiswahili . Ingawa waandishi hawa wana Tamthiliya nyingi lakini utafiti huu uliamua kuteua Tamthiliya za *Mashetani*na *Mashetani Wamerudi.* Hii ni kwa sababu mtafiti aliamini kwamba Tamthiliya hizo zina mwingiliano wa kimatini. Hivyo utafiti huu ulichunguza na kuchambua kazi mbili tu zawaandishi teule. Kwa maana hiyo kazi zao nyengine hazikushughulikiwa isipokuwa zile zilizotajwa. Kazi nyengineza waandishi teule na

zile zile za waandshi wengine zilijadiliwa hapa na pale ili kushadidia data za utafiti huuPia utafiti uliongozwa na nadharia ya fasihi linganishina mwingilianomatini. Pia ulikuwa wa maktabani.

## 1.8 Vikwazo vya Utafiti na Utatuzi wa Vikwazo

Kikwazo kilichomkabili mtafiti ni ugumu wa kupata marejeleo ya tasnifu na makala zinazochambua tamthiliya ya *Mashetani Wamerudi*. Hii inatokana na kwamba tamthiliya hiyo ni mpya katika kuchapwa kwake. Kikwazo hiki kilitatuliwa na mtafiti kwa kutalii dibaji ya *Mashetani Wamerudi* na kupata mawazo ya jumla kuhusu Tamthiliya hii. Hivyo mawazo hayo yalitusaidia katika kukusanya data, kuzichambua, kuziwasilisha na hatimae kujibu maswali ya utafiti huu.

## 1.9 Hitimisho

Sura hii imejadili kuhusu mambo ya msingi ya kiutangulizi. Sura hii imeelezea utangulizi wa jumla, mada ya utafiti, usuli wa mada ya utafiti, tatizo la utafiti, lengo kuu la utafiti. Vile vile sura hii imeelezea madhumuni mahususi ya utafiti, maswala ya utafiti, umuhimu wa utafiti, mipaka ya utafiti, vikwazo vya utafiti na utatuzi wake na hitimisho. Kwa hakika sehemu hii imetoa muelekeo wa namna ambayo utafiti huu ulikusudiwa kuwa kwa kuzingatia malengo, maswali na mada ya utafiti.

# SURA YA PILI

# MAPITIO YA KAZI TANGULIZI NA MKABALA WA KINADHARIA

## 2.1 Utangulizi

Mapitio ya kazi tangulizi ni usomaji wa maandishi ya watafiti watangulizi, unaofanywa na mtafiti kwa minajili ya uchambuzi kuhusu suala la utafiti. Mapitio ya kazi tangulizi yanaonyesha uhusiano wa maandishi hayo na mada ya utafiti. Pia, mapitio ya kazi tangulizi huonesha nadharia zilizotumika katika uchambuzi wa data. Vile vile, mapitio ya kazi tangulizi ni maarifa yanayopatikana kwa uchunguzi wa kina maandishi ya nyuma ambayo hufananishwa na taarifa hai zilizopatikana ndani ya utafiti wa sasa (Enon, 1998).

## 2.1 Maana ya Tamthiliya

Dhana ya tamthiliya imekuwa ikijadiliwa na kufasiliwa kwa mitazamo tofauti.

Mathalani, Mlama (1983:203), anafafanua kwamba tamthiliya, au drama ni aina mojawapo ya sanaa ya maonyesho ambayo usaniiwa utendaji wakehutegemea zaidi vitendona uongeaji, tofauti na aina nyenginekama vile ngoma ambazo hutegemea zaidiuchezaji na upigaji muziki. Tamthiliya ni ule utungo ambao unaweza kuwa umeandikwaau haukuandikwa ambao unaliweka wazo linalotaka kuwaslishwa katika umbo la tukio la kuliwezesha kutendeka mbele ya hadhira. Tamthiliya kwa mujibu wa Mlama na Balisidya (19760, kama wanavyonukuliwa na Mulokozi (1996), huwa na sifa zifuatazo:

(i) Dhana inayotendeka

(ii) Mtendaji

(iii) Uwanja wa kutendea

(iv) Watazamaji

Mulokozi, (1996:188) amefasili tamthiliya kuwa ni "fani ya fasihi iliyokusudiwa kutendwa jukwaani kwa ajili ya hadhira fulani. Kwa lugha nyingine huitwa mchezo wa kuigiza. Kwa kawaida tamthiliya huwa na masimulizi ambayo huigizwa na wahusikawa pande mbili au zaidi zinazogongana.Mgongano huo hatimaye huishia kwenye mgogoro ambao unaposuluhishwaau kutatuliwa, na ndio mchezo huwa umemaliza.

Mulokozi (1996) na (2017) anazikosoa sifa za tamthiliya zinazotolewa na Mlama na Balisidya (washatajwa), akidai kuwa sifa hizo pekee haziwezi kutofautisha kati ya sanaa za maonesho na matendo mengine ya kijamii ambayo si sanaa. Hivyo basi, anasema kuwa tamthiliya lazima iwe na sifa zifuatazo:

(i) Dhana inayotendeka

(ii) Uwanja unaotendewa

(iii) Watendaji

(iv) Hadhira

(v) Kusudio la kisanaa

(vi) Muktadha wa kisanaa

(vii) Ubunifu (umithilishaji).

Kutokana na fasili za wataalam hao tunaweza kusema kwamba, tamthiliya ni utungo wa drama ambayo huandikwa ili ziigizwe. Hii ina maana kwamba, badala ya kuwasilisha wazo kwa hadhira kwa kutumia maneno kama katika ushairi, sanaa za

maonyesho huliweka wazo lile katika hali ambayo tukio linaweza kutendeka kwa kutumia usanii wa kiutendaji, uigizaji unaoambatana na maneno au masimulizi.

Hivyo, katika kazi hii tuliyachukuwa mawazo haya, hasa yale yanayohusiana na mitindo na dhamira za tamthiliya ili kuona namna mitindo na dhamira inavyojidhihirisha au isivyojidhihirisha katika tamthiliya teule zile za mwanzo mwanzo zikiwakilishwa na *Mashetani* na zile za hivi karibuni zikiwakilishwa na tamthiliya ya *Mashetani Wamerudi*.

## 2.2 Historia fupi ya Tamthiliya

Mulokozi (1996) anaeleza kwamba, kabla ya kuja wakoloni, tamthiliya haikuwepo nchini bali aina za sanaa za maonyesho zilizokuwepo zilitofautiana na tamthiliya na zilijulikana kama sanaa za jadi. Kwa maana hiyo, historia ya tamthiliya ilianza wakati wa ukoloni hasa kuanzia mwaka 1920.

Kwa kuwa Wakoloni waliuenzi utamaduni waowalipoingia nchini walileta utawaladuni wao kwa mwavuli wa elimu na dini, ambapo walijenga shule ambazo zilifundisha elimu ya Kimagharibi. Kwa maana hiyo, tamthiliya zilifundishwa shuleni kwakuwa washiriki walishafundishwa kusoma na kuandika Kiingereza. Hivyo, waliojua kusoma na kuandika Kiingereza ndio walioweza kufundishwa tamthiliya na wakoloni. Kwa mfano, shule ya sekondari Forodhani ya sasa iliyojulikana kama St. Joseph Convert school, ilifundisha tamthiliya kama zile za *The Sherrifs kitchen, The ugly duckling, The birds of a feather ya Francis*.

Aidha, Tamthiliya hizi zilijulikana kama Drama zikiwa na madhumuni ya kuwafurahisha Wakoloni hao na kujikumbusha maisha ya kwao. Mulokozi (1996)

anamnuku Mlama (2003:187) akisema kwamba, “kwa vile katika kujifurahisha huko waliwatumia watanzania hasa watoto wa shule katika kuonyesha tamthiliya za akina Shakespear, Watanzaniawaliathiriwa kiasi cha kuweza kujishirikisha kikamilifu katika kutunga tamthiliya na kuzionyesha majukwaani. Hata hivyo, tamthiliya hizi hazikulenga utamaduni wala maadili ya watanzania. Kwa maana hiyo, watawaliwa hawakuweza kuzitumia ili kupata mwamko wa hali yao halisi.

Katika kudumisha tamthiliya hizi, wakoloni walihakikisha mfumo wa elimu iliyotolewa ilikuwa ni ya ki-ubaguzi kwa lengo la kudhibiti hali ya tamthiliya waliyoitaka. Shule za wazungu zilikuwa za daraja la kwanza, zikafuata za Wahindi kisha za waafrika. Ubaguzi huu ulidhibiti tamthiliya hizo na kuhakikisha kuwa zinaonyeshwa kwa lugha ya Kiingereza isipokuwa wahindi waliruhusiwa kutumia lugha yao. Wakoloni walidumisha ubaguzi kwa kuwafanya wahindi daraja la pili ili kuwabagua wasichanganyikane na waafrika. Hii ni mbinu ya kuzuia kuwepo kwa umoja na mshikamano ambao ungeweza kuleta vurugu dhidi ya serikali ya ukoloni.

Shule za Waafrika zilizoonyesha tamthiliya kwa Kiswahili ni zile zilizotafsiriwa kutoka lugha ya Kiingereza zilizojulikana kama ‘Bwana amekufa’ na ‘wanawake wenye adili’. Hata hivyo, tamthiliya hizi hazikuwa na tofauti yoyote katika fani na maudhui katika kutafsiriwa kwake. Katika mwaka 1938 zilianzishwa taasisi nyingine zaidi zilizojishughulisha na tamthiliya. Taasisi hizo ni Hindu volunteer iliyoonyesha tamthiliya za Kihindi iliyoanzishwa mwaka 1938 na The little Theatre iliyonyesha tamthiliya za Kiingereza. Taasisi hii ilianzishwa mwaka 1947 huko Dar-es-Salaam.Arusha little theatre ilianzishwa mwaka 1953.

Mnamo mwaka 1948 wakoloni wa Kiingereza walifanya mkutano ukiwa na lengo la kuzidisha utamaduni wao kwa kutilia mkazo bendi ya Matombola pamoja na tamthiliya na kuanzisha mashindano ya tamthiliya shuleni yaliyotilia mkazo ufasaha wa lugha ya Kiingereza zaidi kuliko mambo mengine. Wakati tamthiliya hizi zinaendelea chini ya udhamini wa wakoloni mashindano yaliyoanzishwa shuleni yaliua tamthiliya za Kihindi kwa kuwa hazikutilia mkazo lugha ya Kiingereza. Mashindano haya yalijulikana kama School drama competition yakiwa chini ya ufadhili wa British Council mwaka 1950.

Mlama (2003:207) anaendelea kusemakuwa, wakati drama hii ya kigeni ilipoendelea kushika mizizi chini ya udhamini wa wazungu, iliibuka aina nyingine ya drama ijulikanayo kama 'Vichekesho' wakati waingereza walipojishughulisha na maonyesho makubwa makubwa ya wanaTamthiliya ya kwao, wakitumia ufundi wa hali ya juu wa ki-maonyesho, baadhi ya Watanzania walivutiwa kutumia vipaji vyao vya kisanaa kuonyesha tamthiliya hizi ambazo hazikutegemea maandishi yoyote bali zilitungwa pale pale wakati wa kutenda. Vichekesho hivi vilipendwa na wakoloni kwa sababu vilionyesha Waafrika hawajaendelea na vilimfanya ajidharau na kujiona duni mbele ya utawala.

**Tamthiliya baada ya 1967**

Tamthiliya zilizoandikwa baada ya Azimio la Arusha zilizingatia misingi yake ambayo ni kukomesha unyonyaji wa mtu na mtu, njia kuu za uchumi kumilikiwa na wakulima na wafanyakazi na kuwa na utawala wa kidemokrasia. Kwa maana hiyo kulikuwa na haja ya kuinua utamaduni wa mtanzania kwa kutilia mkazo lugha ya *Kiswahili, kuanzishwa kwa Baraza la Kiswahili Tanzania (BAKITA) na Bunge la*

*Tanzania mwaka 1967. Baada ya kutangazwa kwa Azimio la Arusha, Tamthiliya zilizoandikwa zilikuwa na dhamira nyingi za kuwahamasisha watu tangu nyakati za ukoloni*. Mlama, (2003:215) katika makala hii anasema kwamba wengi watunzi hawa waliopitia mfumo wa elimu ambao uliwapa ujuzi wa utunzi kutokana na somo la Kiingereza au sanaa za maonyesho. Tamthiliya hizi walizoziandika, zilikuwa kama zile za nchi za Ulaya lakini zilikuwa zenye sura ya Kitanzania zaidi kwa vile walitumia vipengele fulani vya fani za sanaa za maonyesho zenye asili ya Tanzania katika kuandika tamthiliya hizo. Vipengele walivyovitumia ni kama vile ngoma, nyimbo, utambaji hadithi na majigambo katika utunzi wa tamthiliya mfano *Tiba,* Nkwera (1969*) Kinjeketile (1969), Mashetani (1971),* ya E. Hussein, *Ngao ya Jadi* (1976 ) na *Pambo (*1978) za Muhando na *Mashetani (1971)*vya E.Hussein,*Giza Limeingia (1980)* cha E. Mbogo. Tamthiliya hizi zilileta upya katika fani ya tamthiliya ambayo ilitegemea zaidi usanii bora wa vitendo na usomaji na kuweka usanii huu katika uafrika zaidi.

Katika kipindi hiki cha wakati wa vyama vingi kumejitokeza kazi nyingi za tamthiliya za Kiswahili. Badhi ya kazi hizo ni*Kilio Chetu (*1996) ya Medical Aid Foundation*, Orodha* (2006) ya Steve Renolds. *Ngoswe, Penzi Kitovucha Uzembeya E. Semzaba), Sundiata (2011), Nyerere na Safari ya Kanani (2015), Nyota ya Tom Mboya (2016), WangariMaathai (2015), Malkia Bibi Titi Mohamed (2016)*(zote za Mbogo, *Mashetani Wamerudi,* (2016), cha Said Ahmed Mohamed na kadhalika.

## 2.3 Mapitio ya Maandiko

Lengo la utafiti huu lilikuwa ni kutathmini matumizi ya mtindo na dhamira katika Tamthiliya za *Mashetani ya* Ebrahim Hussein *na Mashetani Wamerudi* ya Said

Ahmed Mohammed kwa mkabala wa Fasihi Linganishi. Hivyo basi, ili kufikia lengo la utafiti huu mtafiti amepitia maandiko kuhusu dhana ya Fasihi Linganishi, mtindo katika kazi za fasihi na dhana ya dhamira.

### 2.3.1 Maandiko Kuhusu Dhana ya Fasihi Linganishi

Ponera (2014) anasema kuwa kitaaluma fasihi linganishi ilianza mwishoni mwa karne ya kumi na tisa na kupata nguvu mwanzoni mwa karne ya ishirini. Kuibuka kwa dhana ya kufanya ulinganisho katika vipengele mbali mbali vya kifani kunanasibishwa na safari zilizokuwa zinafanywa na wataalamu katika sehemu tafauti za dunia. Ijapokuwa madhumuni ya safari hizo hayakuwa kuzitalii fasihi au sanaa za sehemu hizo, bali ilidhihirika kuwa kulikuwa na tofauti fulani walizozibaini katika utendekaji wa fasihi katika jamii hizo, hususani fasihi simulizi. Tofauti hizo, kwa namna moja au nyengine, ziliamsha uelewa wao wa kuzilinganisha na kuzilinganua fasihi au sanaa hizo.

Guyardkama alivyonukuliwa na Weisstein (1968), anasema kuwa fasihi linganishi ni tawi la historia ya fasihi. Somo hili ni mahusiano, mapatano, na maelewano ya kimataifa baina ya Byron na Pushkin, Goethe na Carllyle, Walterscott na Alfred de Vigny na baina ya kazi na hata maisha ya waandishi wanaotoka katika fasihi tafauti.

Kwa upande mwingine, Wellek (1988), anaiona fasihi linganishi kuwa ni somo linalojishughulisha na uhusiano wa vitu viwili. Vitu hivi vinaweza kuwa kazi ya mtu binafsi, waandishi au kundi la waandishi na binadamu au fasihi kwa ujumla. Kwa upande wake, Wellek (ameshatajwa), anaiona fasihi linganishi kuwa ni somo la fasihi nje ya mipaka ya nchi moja, ni kujifunza uhusiano baina ya fasihi kwa upande

mmoja na eneo lingine la maarifa kama vile sanaa, falsafa, historia ya sanaa za jamii, sayansi, dini na vipengele vyengine.

Kwa upande mwingine, anaieleza taaluma hii kuwa ni ulinganishi wa fasihi na fasihi nyingine au zingine na ulinganishi wa fasihi na mzunguko wa maelezo ya binadamu. Maelezo ya Wellek (ameshatajwa) yamenufaisha sana katika kusukuma mbele utafiti huu. Kutokana na kwamba mjadala wake umeingia ndani zaidi juu ya namna utafiti linganishi unavyoweza kufanyika. Anapotaja vipengele vya mtindo na dhamira ambavyo huweza kushughulikiwa na utafiti linganishi vinatoa muelekeo chanya kwa utafiti huu na namna data zitakavyochnguzwa na mtafiti.

Bassnett (1993) anaifafanua dhana ya fasihi linganishi kuwa ni taaluma ya usomaji matini za tamaduni tofauti ili kubaini mazingira zinapokutana na zinapoachana. Kwa msingi huu mtafiti wa fasihi linganishi huzizamia mbizi kazi za watunzi teule ili kuona namna kazi hizo zilivyoingiliana na kuachana.

Mulokozi (1996anasema kuwa wataalamu wa fasihi linganishi hukubaliana kimawazo kuhusu usuli wa dhana ya fasihi, inapochukuliwa kama dhana inayotokana na neno la Kiengereza "literature" kwamba, umo katika neno la Kilatini "littera" linalomaanisha "herufi" au "uandikaji". Kwa hivyo, neno hili "littera" ndilo lililozaa neno la Kiengereza "literature." Mantiki ya mawazo haya ni kuwa ubunifu wa kifasihi huweza kutafautiana au kufanana kutegemea mazingira ya mtunzi. Hali hii hutokana na hali ya kimazingira pamoja na utamaduni uliomzunguka mtunzi, kwavile ndio malighafi ya kazi husika.

Hali hii inajadiliwa na Ponera (2014), ambae anasema kwamba tunapoichukulia fasihi kuwa ni kiambata muhimu cha maisha ya mwanadamu si lazima tujikite kwa dhana ya fasihi kwa ngazi ya juu ya kitaaluma; bali twaweza kujieleza katika ngazi ya chini kama ufundi tu wa kuisana lugha na kuitumia katika matukio na vipengele mbali mbali vimtokeavyo mwanadamu kila siku katika maisha yake. Dhana ya ngazi ya juu inayoelezwa na Ponera (ameshatajwa) ni matumizi ya vipengele kama vile maghani, nyimbo na hadithi ndefu. Ngazi ya kawaida ya kifasihi inamaanisha uwezo wa kuisana lugha ambayo mwanaadamu yoyote anao na huitumia ili kukidhi mahitaji yake ya kila siku.

Kazi yoyote ya fasihi hufuata mitindo mahususi kutegemea utanzu husika, mandhari na mtunzi husika. Mtunzi wa kazi za fasihi huchota mitindo mahususi ya kisanii ambayo hujitokeza katika ujengaji wa fikra na dhamira alizozikusudia. Mitindo ya aina hii huweza kujitokeza katika kila kazi yake. Sifa hii ndiyo inayomfanya msomaji wa kazi fulani ya fasihi tumuelewe mtunzi wa kazi hiyo kwa kuisoma kazi hiyo kutokana na kujitokeza mitindo iliyozoeleka ya mtunzi wa kazi husika.

Vile vile, mitindo na dhamira iliyotumiwa na mwandishi huwafanya wasomaji wa kazi za kifasihi kuwatafautisha watunzi wa fasihi au hata kuwafananisha. Sababu ya mazingira ya kiutunzi nayo pia huwafanya wasomaji waone tafauti za watunzi wa kazi mbali mbali za fasihi.

Salem (2013) anasema kuwa utafiti linganishi huweza kufanywa kwa kulinganisha kazi za mwandishi mmoja katika vipindi tafauti ama katika kipindi kimoja cha kihistoria. Mathalan, tunaweza kulinganisha kazi za fasihi za Kezilahabi za kipindi

cha miaka ya sabini na kipindi cha miaka ya 2000 au kulinganisha kazi za fasihi za Shaaban Robert katika vipindi tofauti tofuti vya uandishi. Kufanya hivi kunatuonesha kuhusiana, kufanana na kutafautiana kwa uteuzi na matumizi ya lugha na maudhui na namna yanavyowasilishwa.

Baada ya kupitia maandishi ya waandishi waliozungumzia kuhusiana na fasihi linganishi tunasema kuwa fasihi linganishi ni taaluma inayojishughulisha na ulinganishaji wa kazi za fasihi. Taaluma hii inashughulikia tofauti au kufanana kwa fasihi ya makundi mawili au zaidi ya kijamii, kiisimu, kiutamaduni, kihistoria, kiitikadi, kiuchumi na kimataifa. Hivyo mawazo haya yalitumika katika kutathmini matumizi ya mitindo na dhamira katika Tamthiliya ya *Mashetani* ya Ibrahim Hussein ikilinganishwa na Tamthiliya ya *Mashetani Wamerudi*ya Said Ahmed Mohammed.

## 2.4 Vipengele vya Ulinganisho

Ponera (2014) anavieleza vipengele vinavyoweza kufanyiwa ulinganisho kwa kuvitaja kwambaa ni kama vilemaana, utamaduni, upokezi, unusura, uigaji na uathiriano, uwakati, mtagusano, tanzu mbali mbali, ukanda, mbinu za kibunilizi, mbinu za kimuundo, motifu na mtindo. Mawazo haya ya Ponera yana umuhimu mkubwa katika kusukuma mbele kazi hii. Hii ni kwa sababu vipengele hivi vilitoa muongozo kwa mtafiti kuhusiana na namna ya kukusanya data kutoka Tamthiliya teule ambazo zilichunguzwa kwa mkabala wa kiulinganishi.

Naye Jilala (2016) anaviweka vipengele vya kiulinganizi katika makundi matatu-ambayo ni fani, maudhui na utamaduni isimu (misingi ya kiisimu, misingi ya

kiutamaduni, stadi na ujuzi wa kilinganishi, misingi ya kimazingira, jiografia na muktadha). Mawazo ya Jilala (ameshatajwa) yalitoa uelewa mpana kwa mtafiti juu ya dhana ya fasihi linganishi kwa misingi ya kitaaluma. Kwa mantiki hii ni kwamba utafiti huu uliyachukuwa mawazo haya ili kusukuma mbele kazi hii.

## 2.5 Mtindo katika Kazi za Fasihi

Dhana ya mtindo ni changamano miongoni mwa kazi za fasihi. Dhana hii imekuwa ikitazamwa katikamitazamo tofauti. Kwamfano, katika kujadili mtindo Madumulla (2009), anaeleza kuwa mtindo ni kipengele cha fani ambacho huonesha kazi ya sanaa na namna ilivyosimuliwa. Nyenzo inayotumika zaidi katikakujadili kipengele cha mtindo ni lughana jinsi ilivyotumika.Madumulla (ameshatajwa) anautazama mtindo kwa masimulizi na matumizi ya lugha kuwa ndio vipengele muhimu katika kuangalia mtindo katika kazi ya fasihi. Utafiti huu uliona bado kuna pengo katika mtazamo huu. Mtafiti anauona mtindo kuwa umepinduka mipaka ya lugha na masimulizi. Pamoja na mapungufu ya mtazamo huu mtafiti aliyatumia maelezo hayo ili kuona namna vipengele vya kiusimulizi na lugha vilivyotumiwa nawatunzi wa tamthiliya teule kama vipengele vya mtindo katika kazi za fasihi.

Vile vile, Haji na wenzake (1981), wanaujadili mtindo katika kazi ya fasihi na kueleza kuwa unaweza kuwa wa kihistoria ambapo mwandishi husimulia maisha yake mwenyewe au mtu mashuhuri katikajamii yake. Jambo muhimu wanalolisisitiza ni kwamba historia na fasihi ni taaluma mbili tofauti. Kwa hivyo, fasihi inapochagua mtindo wa historia huwa haulazimiki kuifuata historia kama ilivyo kwa sababu fasihi ina uhuru wakupitia njia zake ambapo historia haina budi kujifunga na matukio na tarehe zake kama zilivyo.

Kwa mantiki hii Haji na wenzake (wameshatajwa), mawazo yao yalitumiwa na mtafiti ili kuchunguza mitindo inavyohusishwa na historia na pia kuzihusisha data zilizokusanywa kutoka Tamthiliya teule iwapo historia imejitokeza na namna watunzi hao walivyolingana ama kuachana katika upenyezi wa historia katika kazi zao.

Utafiti huu unautazama mtindo katika kazi ya fasihi kama upekee wa msanii unaojitokeza katika kazi yake ambayo hutofautiana na wasanii wengine.Tofauti hizi hujitokeza katika matumizi ya tanzu ndani ya utanzu, usawiri wa wahusika, motifu za safari, matumizi ya tamathali za usemi, usawiri wa mandhari, upangaji wa matukio, matumizi yambinu za uhalisiajabu pamoja na ujengaji wa maudhui ya mtunzi.

## 2.6 Vipengele vya Kimtindo katika Fasihi Linganishi

Njogu na Chimerah (2008) wanasema mtindo ni tabia ya utungaji inayopambanua mtunzi mmoja na mwengine. Ni dhana inayoelezea sifa inayobainisha kazi fulani na kuitenga kazi nyenginezo. Pia, mtindo humtambulisha mtunzi anayehusika.

Jilala (2016) anaifafanua dhana ya mtindo katika kazi za fasihi huku akihusisha na nadharia ya fasihi linganishi kwa kueleza kuwa mtindo katika kazi za fasihi ni ile sifa aliyonayo mtu ambayo inamtafautisha na mtu mwengine katika uzalishaji wa kazi za sanaa. Hii ni sifa ya pekee ambayo mtunzi mwengine hawezi kuwa nayo hata kama anaiga ama kuathiriwa na mtunzi asilia. Hivyo ili kufanikisha ulinganishaji wa kazi za fasihi, mwanafasihi linganishi anapaswa kuwa na uelewa wa vipengele vya mtindo. Mtindo huonesha sifa ya kipekee aliyonayo mtunzi mmoja na mtunzi

mwengine. Mtindo huweza kuwatofautisha watunzi wa kipindi, wakati na miongo tofauti na kuonesha sifa bainifu za kisanii zinazoweza kuwatofautisha wasanii, msanii binafsi na wasanii wa kipindi fulani. Kwa hali hiyo, ili kuweza kujua tofauti ya mwandishi mmoja na mwengine inatupasa kuvibaini vipengele vya kimtindo ambavyo vinamtafautisha msanii huyo. Mambo hayo ndiyo yatakayomuongoza mtafiti kujua muachano na mshikamano wa watunzi tofauti.

Jilala (2016) anavitaja vipengele vinavyochunguzwa wakati wa kuchunguza mtindo katika kazi za fasihi. Vipengele anavyovitaja ni uteuzi wa msamiati, miundo na mpangilio wa sentensi, uteuzi wa matumizi ya tamathali za usemi na jazanda, usawiri wa wahusika, motifu na dhamira zinavyokaririwa katika kazi za watunzi, usimulizi na mbinu za usimulizi wenyewe na sifa ya uakifishi. Kwa kutumia vipengele hivi mlinganishaji anaweza kubaini ama kufanana au kutofautiana kwa watunzi wa kazi anazozishughulikia.

Mawazo ya Jilala (ameshatajwa), yalitoa mchango mkubwa katika utafiti huu. Mawazo hayo yanaeleza namna mtafiti wa fasihi linganishi anavyopaswa kushughulikia kipengele cha mtindo katika kazi anayoitafiti. Utafiti huu unaona kuwavipengele vilivyotajwa kama nyenzo ya mtindo ni muhimu katika kufikia malengo ya utafiti huu. Hivyo, mawazo hayo yatasaidia katika uchunguzi wa data za utafiti huu ili kufikia lengo la utafiti huu.

## 2.7 Dhana ya Dhamira

Madumulla (2009) anaeleza kuwa dhamira ni wazo kuu katika kazi ya fasihi. Anaendelea kueleza kuwa, Senkoro anatahadharisha kuchanganya dhamira na

maudhui, jambo ambalo hutokea kwa wengi. Dhamira ni sehemu tu ya maudhui. Na aghalabu, dhamira kuu ndio hujenga kiini cha kazi ya fasihi. Dhamira kuu ndio husindikizwa na dhamira ndogo ndogo. Mawazo ya Madumulla (ameshatajwa) kuhusu dhamira yalikuwa na umuhimu mkubwa kwa utafiti huu, kwani mawazo hayo yalimpatia mtafiti mawazo ya namna ya kuzichunguza dhamira katika tamthiliya teule.

Ndungo na Wafula (1993) wanaiona dhana ya dhamira kama ni sehemu moja tu ya maudhui ya kazi ya fasihi. Hivyo dhamira ni kiini cha suala linalozungumzwa na mwandishi katika kazi ya fasihi. Waandishi hawa wamezigawa dhamira katika makundi mawili, nayo ni dhamira kuu na dhamira ndogo ndogo. Kwa mfano, wanasema kuwa unaweza kuwa na dhamira ya vita vya ukombozi, dhamira ya ujenzi wa jamii, dhamira ya utu bora, uvivu na ulanguzi.

Mawazo ya Ndungo na Wafula yalitusaidia katika utafiti huu kubaini dhamira katika kazi zitakazotafitiwa. Waandishi hao wametoa mifano ya dhamira zinazojitokeza katika kazi za fasihi. Kwa hivyo, mtafiti alichukua vidokezo hivyo kama ni mwanzo wa kutafiti dhamira katika kazi amthiliya teule.

Senyamanza (2012) anaifafanua dhana ya dhamira na kusema kuwa haipaswi kuchanganywa na dhana ya maudhui kwa sababu dhana hizo ni tofauti. Dhamira ni kiini cha suala linalozungumzwa na mwandishi katika kazi yake. Dhamira ni sehemu mojawapo tu ya maudhui ya kazi ya fasihi. Kwa kawaida dhamira kuu ndiyo hujenga kiini cha kazi nzima ya fasihi. Dhamira kuu husindikizwa na dhamira ndogo ndogo na hizi ndizo zijengazo dhamira kuu. Wazo kuu ambalo hasa ndilo libebalo wazo kuu

hutoa dhamira kuu.Kwa maoni ya utafiti huu ni kwamba dhamira ni makusudio ambayo msanii amekusudia kufikisha ujumbe kwa jamii husika. Makusudio haya hutokana na yale yaliyomgusa mtunzi katika nyoyo. Mguso huo huweza kuwa tamu ama chungu na hivyo kutaka kudhihirisha hisia alizonazo kwa jamii. Mguso huo huweza kuwa katika nyanja zote za mwanaadamu yaani kisiasa, kiuchumi, kiutamaduni na hata kijamii.

## 2.8 Kazi Tangulizi kuhusu Mtindo katika Tamthiliyaza Kiswahili

Musyoka (1996), katika kuhakiki fani katika Tamthiliya nne za Jay Kitsao, *Uasi* (1980) *Malimwengu Ulimwengu* (1983), *Bibi Arusi (*1983*) na Tazama Mbele* (1987) amechanganua vipengele vya fani katika usambamba wa msingi nakaida za utanzu wa tamthiliya. Anatubainishia kuwa fani ni uumbaji na ufundi wa kipekee ambao huhusishwa na mtindo wa mwandishi mahsusi. Kwa ujumla, ametathmini umbaji wa msanii na jinsi fani ilivyoathiri na kuchangia katika kiwango cha kisanaa na kazi hizo. Ametumia Nadharia ya Mwingilianomatini katika uhakiki wake. Kazi hii ilitoa mchangomkuubwa katika kusukuma mbele utafiti wetu. Hii inatokana na kazi hiyo kutumiavipengele vya fani, mtindo ukiwemo, pia imetumia Nadharia ya Mwingilianomatini. Kwa mantiki hii mtafiti alipata uelewa wa namna ya kufanya uchambuzi wa data za kimtindo kwa kutumia Nadharia ya Mwingilianomatini kama alivyofanya Musyoka**.**

Mugambi (1980), amehakiki maudhui katika tamthlia zilizochapishwa nchini Kenya za kipindi kati ya mwaka 1957 hadi 1981. Katika utafiti wake Mugambi (ameshatajwa) ameonyesha mbinu zakifani walizotumia watunzi katika tamthiliya hizo ili kuendeleza maudhui. Miongoni mwa maudhui aliyochanganua ni pamoja na

udhalimu, usaliti, ukombozi, nafasi ya mwanamke katika jamii, utetezi wa haki za wanyonge na ukoloni mamboleo. Aidha, ameonesha mandhari, wahusika, matumizi ya lugha hasa jazanda na tamathali za semi kama mbinu muhimu ktika ujenzi wa maudhui ya kazi za wakati huo. Ingawa kazi ya Mugambi (ameshatajwa) ilikuwa ni tofauti na tamthiliya zilizotafitiwa hata hivyo kazi hiyo ilikuwa na umuhimu katika kufikia lengo la utafiti huu kutokana na kuonesha namna ya kuibua dhamira za muandishi wa kazi teule. Pia, kazi hiyo ilikuwa na umuhimu kwetu kutokana na kuonesha namna mtindo katika kazi za fasihi unavyoweza kuendeleza maudhui.

Sarara (1997), amechanganua maudhui katika tamthiliya za Said Ahmed Mohammed. Ameyashughulikia maswala ya kijamii katika amthiliya tatu, *Pungwa (1988), Kivuli Kinaishi (1990) na Amezidi (1995).* Katika utafiti huo amechanganua maudhui yanayolenga jamii ya kisiasa kama vile; kudhulumiwa kwa wanawake, mapambo ilikuleta ukombozi, rushwa au ufisadi na umaskini miongoni mwa jamii. Utafiti wa Sarara ulitufaa sana. Kwanza, utafiti huo umechunguza maudhui ya msanii ambaye tunamshughulikia. Pili, kazi hiyo imechambua dhamira za kijamii kama tulivyofanya katika Tamthiliyateule. Tofauti ya kazi ya Sarara ni kwamba sisi tunachunguza mtindo na dhamira kwa mkabala wa kiulinganishi katika kazi tofauti na alizozitafiti wakati yeyé hakufanya kwa mkabala wa kiulinganishi.

Masoti (1993) amejadili maudhui katika Tamthiliya nne za Emmunuel Mbogo, *Giza Limeingia* (1980), *Tone La Mwisho* (1981), *Watoto Wetu* (1981), na *Ngoma ya Ng'wanamalundi* (1988). Katika kazi hiyo amejadili maudhui kwa misingi ya nadharia ya uyakinifu wa kijamaa miongoni mwa maudhui aliyoyahakiki ni ukombozi, dhulma, usasi wa usaliti ubinafsi na nafasi ya mwanamke katika jamii.

Pamoja na kwamba kazi alizozitafiti ni tofauti na tunazozitafiti, utafiti huo ulikuwa na manufaa makubwa katika kufikia lengo la utafiti wetu. Hii ni kwa sababu Masoti alifanya uchambuzi wa maudhui, dhamira zikiwemo kama tutakavyochunguza dhamira katika kazi teule. Hivyo, tuliona namna ya kuchambua na kuwasilisha data zinazuhusiana na dhamira kwa mkabala wa kifasihi.

Too (2011) alitafiti Tamthiliya ya *Nguzo Mama* (1982), ya Penina Muhando. Alitumia Nadharia Umuundo na Simiotiki. Katika uchunguzi huo alifanya uchanganuzi wa vipengele vya lugha na namna vilivyotumiwa na msanii teule. Kazi hii pia ilikuwa na umuhimu katika utafiti wetu kutokana na kutoa muongozo wa namna ya kufanya uchambuzi wa data zinazohusiana na vipengele vya lugha katika fasihi.

Mningo (2015), alichunguza mwingilianomatini katika tamthiliya za Emmanuel Mbogo ya *Fumo Liyongo* na *Ngoma ya Ng'wanamalundi* kwa mkabala wa kiulinganishi. Katika utafiti huo pia alichunguza vipengele vya kimtindo kama vile; matumizi ya hadithi, matumizi ya ngoma, matumizi ya majigambo, matumizi ya ushairi, matumizi ya wahusika wa fasihi simulizi, usihiri (uchawi) ambapo alilinganisha kazi za mwandishi mmoja katika vipindi tofauti huku akiongozwa na nadharia ya Mwiitiko wa Msomaji na nadharia ya Mwingilianomatini. Kazi ya Mningo (ameshatajwa) ilikuwa na mchango mkubwa katika utafiti wetu. Kwa sababu ilichunguza vipengele vya mtindo ambavyo ni miongoni mwa lengo la utafiti wetu.

## 2.9 Kazi Tangulizi kuhusu Tamthiliya Teuliwa

Saleem (2013), alifanya utafiti linganishi wa tamthiliya ya *Mashetani* na *Kivuli Kinaishi* kwa kutumia mkabala wa kiulinganishi. Lengo kuu likiwa ni kuchunguza kiulinganifu na utofauti uliopo kati ya tamthiliyaza *Mashetani*na *Kivuli Kinaishi* na sababu zilizofanya Tamthiliya hizo zifanane au zitofautiane kimaudhui na kifani. Utafiti huu kwa vile ulihusu fani basi kipengele cha mtindo pia kilichunguzwa. Utafiti wa Saleem (ameshatajwa) ulikuwa ni mfano mzuri wa utafiti linganishi. Kazi hiyo ilimpatia mtafiti uelewa wa namna ya kufikia malengo yake. Hii ni kwa sababu alichunguza Tamthiliya mbili za *Kivuli Kinaishi* na *Mashetani* ambapo *Masheitani* ni moja ya kazi iliyotafitiwa katika utafiti huu. Pamoja na kulingana huko, kazi ya Saleem (ameshatajwa) ni tofauti na kazi hii kwa sababu utafiti huu ulilenga kufanya uchunguzi wa kimtindo na dhamira kwa mkabala wa Nadharia ya Fasihi Linganishi na Mwingilianomatini kati ya *Mashetani* na *Mashetani Wamerudi*.

Jilala (2016), alichambua kwa kiulinganishi fasihi ya Kiafrika na fasihi ya Kimagharibi kwa kutumia mifano kutoka Tamthiliyaya *Mashetani* (1971), na *MfalmeAdepode* (1971). Uchunguzi huo ulihusisha vipengele vya kimtindo na dhamirakatika Tamthiliyaza *Mashetani* na Mfalme *Adpode*. Uchunguzi huo ulitoa mawazo mapya juu ya namna ya kufanya utafiti linganishi katika Tamthiliya teule. Jilala alichunguza vipengele vya kimtindo kama vile; motifu ya safari, vipengele vya lugha, hadithi ndani ya hadithi. Utafiti huu wa Jilala (ameshatajwa) ulikuwa na maarifa muhimu sana ya kuufanya utafiti huu kufikia malengo yake.

Hii inatokana na kwamba kuna mlingano wa uchambuzi wa data kwa mkabala wa kiulinganishi kama tulivyofanya katika kazi hii. Tofauti ya uchambuzi wake na

utafiti huu ni kwamba Jilala (ameshatajwa) analinganisha Tamthiliya ya *Mashetani* (1971), na *Mfalme Adepode* (1971), lakini utafiti wetu ulichunguza Tamthiliya za *Mashetani* na *Mashetani Wamerudi* ili kuona jinsi zilivyofanana na kutofautiana katika matumizi ya mtindo na dhamira. Wafula (1999), alifanya uchambuzi wa jazanda ya shetani katika tamthiliya ya *Mashetani*. Katika uchambuzi huo Wafula anaonesha namna jazanda ya shetani inavyotumiwa na msanii katika kuchora picha ya ukoloni na ukoloni mamboleo.

Uchambuzi huu ingawa haukufanyika kwa mkabala wa kiulinganishi kama tulivyofanya katika utafiti huu hata hivyo, kazi hiyo ina manufaa makubwa katika kusukumba mbele utafiti huu. Hii ni kutokana na kuibua dhamira ambazo zimechorwa kupitia mtindo wa mhusika sheitani. Tofauti ya kazi ya Wafula na yetu ni kwamba yeye anatumia shetani kuibua dhamira wakati sisi tutachunguza kwa kina vipengele vya mtindo na kidhamira huku tukivilinganisha na Tamthiliya ya *Mashetani Wamerudi.*

Mohamed (2016), anaeleza kuwa tamthiliya ya *Mashetani* ilifinyangwa makusudi kushikamana na tamaa baada ya muhula wa ukoloni, maendeleo ya historia ya siasa ya Tanzania, Kenya na Afrika kwa ujumla. Anaeleza kuwa Hussen katika tamthiliya hii alijadili yale aliyoyaona mapema katika nchi za kiafrika zilivyoanza kupita njia mbaya hasa njia ya kiuchumi, kisiasa, kielimu, kisayansi na kiteknolojia na kiutamaduni.

Hali hii iliwafanya Waafrika wakemee ukoloni mamboleo kwa mdomo tu. Ili kuendeleza historia ya kisiasa mtunzi wa *Mashetani Wamerudi* ameamua kuandika

historia ya utandawazi. Maelezo haya yanayotolewa na Mohamed (ameshatajwa), yanayodokeza dhamira za tamthiliya ya *Mashetani Wamerudi* yalikuwa na mchango mkubwa katika utafiti huu. Hii ni kutokana na kwamba utafiti wetu pia ulichunguza dhamira anazozieleza Mohamed ili kuona ni kwa jinsi gani zimejidhihirisha ama hazikujidhihirisha katika tamthiliya teule.

## 2.10 Pengo la Maarifa

Kutokana na mapitio tuliyoyafanya tumeona kwamba mpaka sasa tafiti mbalimbali zimefanyika kuhusu maudhui na fani katika tamthiliyaya *Mashetani*lakini mtafiti hajaona kazi ambayo imefanyika kwa lengo lakutathmini matumizi ya mtindo na dhamira katika tamthiliya ya *Mashetani*ya E. Hussein na ikilinganishwa na Tamthiliya ya hivi karibuni ya *Mashetani Wamerudi* iliyoandikwa na Said A. Mohamed katika mkabala wa kiulinganishi na Nadharia ya Mwingilianomatini. Kwa hivyo, utafiti huu, ulijikita kutathmini matumizi ya mtindo na dhamira katika Tamthiliya teule ili kuziba pengo hilo.

## 2.11 Mkabala wa Nadharia

Nadharia ni mawazo, mpango, mwongozo, maelezo, yaliyowekwa ili kusaidia kutatua au kutekeleza jambo fulani (Msokile, 1993). Nadharia za uhakiki ni muongozo unaomuelekeza msomaji na mhakiki kwenye vipengele vya msingi vya nadharia anayoitumia (Wamitila, 2002). Hivyo, utafiti huu umeongozwa na nadharia ya Mwingilianomatini na nadharia ya Fasihi Linganishi. Nadharia ya Mwingilianomatini inachunguza namna matini za kifasihi zinavyoingiliana katika vipengele vya fani na maudhui. Pia, nadharia ya Fasihi Linganishi hutumika kulinganisha namna vipengele vya fani na maudhui katika matini za kifasihi

zinavyolingana na kutofautiana. Kwa hivyo, mtafiti ameona kuwa nadharia hizo zinauhusiano mkubwa. Hivyo basi, nadharia hizi zimefanyiwa uchambuzi kama ifuatavyo:

### 2.11.1 Nadharia ya Mwingilianomatini

Kwa mujibu wa Wamitila (2002) na Njogu na Wafula (2007) Mwingilianomatini ni moja ya nadharia ya fasihi, ambayo hutumika katka kuchunguza na kuchambua data za utafiti na kubaini kazi moja ndani ya kazi nyengine katika za fasihi. Nadharia hii iliasisiwa na Mfaransa, JuliusKristeva, Kristeva aliizua nadharia hii ya Mwingilianomatini kutokana na fikra zilizotokana na nadharia ya Usemezano ya Mrusi Mikhail Bukhtin mwaka ( 1895 – 1975). Bakhtin, anaamin katika nadharia hiyo ya usemmezano huwa kazi ya fasihi ina alama ya sauti ambazo huingiliana na kutoa mwangwi katika kazi nyengine zilizopita, zilizopo kwa sasa au zitazotungwa baada ya hizo zilizotangulia. Hii ina maana kuwa athari ya kazi moja huweza kuonekana katika kazi nyengine zilizopo kwa sasa au zitakazotungwa baadae.

Hivyo mawazo ya Bukhtin yalifanya kuzuka kwa mawazo ya Kristeva na kuyaendeleza mawazo hayo na ndio alipozuka na nadharia ya mwingilianomatini mnamo mwaka 1960. Kristeva katika nadharia yake hiyo anaamin kuwa katika kazi yoyote ile inayomuhusu mwanaadamu haiwezi kuangalia peke yake hivyo matini hiyo itakuwa na mafungamano na kazi nyengine inayochangiana nayo nakukamilishana katika miktaza mbali mbali. Mawazo haya yanashadidiwa na Jilala (2016), anapoeleza kuwa Nadharia ya Mwingilianomatini ni dhana inayorejelea uhusiano wowote unaoweza kuonekana katika matini moja na nyengine au matini

zaidi ya moja. Uhusiano huu unaweza kujitokeza katika kipengele kimoja au vipengele mbali mbali, fani, maudhui au hata vyote kwa pamoja.

Ngesa (2015) anaeleza kuwa dhana ya mwingilianomatini inarejelea msingi kuwa matini ya kisanaa si zao la mwandishi mmoja bali ni zao la jinsi matini hiyo huhusiana na matini nyingine na miundo ya lugha yenyewe. Dhana hii husisitiza kuwa matini zote za kisanaa zaweza kuchukuliwa kama matini moja kuu ambapo hujibizana; kila moja ikisemezana na nyingine kwenye usemezano uliotanuliwa (Plotell & Charney 1978). Aidha, matini zote huhusiana kwa njia moja au nyingine, na vilevile matini zenyewe hutegemeana ili kuzalisha maana. Kwa mujibu wa Ngesa (ameshatajwa) baadhiya mihimili mikuu ya nadharia ya mwingilianomatini ni pamoja na:

(i) Matini yoyote ile ni mabadiliko ya mpangilio wa matini nyingi tangulizi.

(ii) Kazi za kifasihi huundwa kutokana na mifumo ya kanuni na tamaduni mbali mbali zilizowekwa na kazi tangulizi za kifasihi ambapo taswira za maisha ya kawaida na uhusiano wa kimaana huunganishwa na kubadilishwa.

(iii) Matini moja hufafanua usomekaji wa mkusanyiko wa matini zote za kongoo moja, ambapo matini tangulizi hufyonzwa na kujibiwa na matini mpya.

(iv) Matini za kifasihi huwa zimechota, kunukuu, kugeuza, kuiga kwa namna ya kubeza au kurejelea kwa njia moja au nyingine matini nyingine.

(v) Kila usomaji wa matini huwa ni kijalizo cha matini tangulizi na hivyo basi huigeuza kwa kiwango. Kwa jinsi hii kauli inayonukuliwa hubadili na kuelezeaupya kauli asilia kwa kuiambatanisha na muktadha mwingine wa ki-isimu na kijamii.

Nadhariahii inachambua lengo mahsusi la kwanza na la pili ili kuonesha uathiriano na mwingiliano baina ya kazi moja na nyengine.

### 2.11.2 Nadharia ya Fasihi Linganishi

Nadharia ya Fasihi Linganishi ina husishwa sana Zepetnek. Zepetnek (1998), anasema kuwa Nadharia ya Fasihi Linganishi ni kama nyenzo ya kuyachanganua na kuyashughulikia masuala ya ulimwengu. Kwa mtazamo huu, taaluma hii huweza kuelezwa kwa namna kuu mbili. Kwanza ni utambuzi wa maarifa yahusuyo lugha na utamaduni wa taifa zaidi ya moja na huchunguza jinsi maarifa yanavyotumiwa katika kuustawisha uga wa fasihi. Pili, Fasihi Linganishi ni taaluma ambayo stadi zake zimeelekezwa katika itikadi ya kuzijumuisha fasihi zote za ulimwenguni, pamoja na tanzu ambazo hazipewi umbele au hazichangamkiwi sana katika kushughulikiwa.

Ponera (2014), na Jilala (2016), wanaeleza kuwa, chimbuko la dhana ya Fasihi Linganishi liko katika maneno ya Kifaransa yaani *`la Literature Comperee`* yenye maana ya `Fasihi Linganishi` kwa Kiswahili. Baadae huko Ulaya dhana hii ilipewa majina mbali mbali kulingana na vipindi ilivyopitia. Miongoni mwa majina hayo ni “Fasihi Linganishi ya Kihistoria”, “Fasihi Linganishi ya Kisasa” na “Fasihi Linganishi ya Kimataifa”.

Fikra za kulinganisha fasihi za jamii au mataifa mbali mbali ni za kale ikilinganishwa na sura ya ulinganishaji ilivyo hivi sasa kama nyanja ya kitaaluma. Hapa ina maana kuwa, kabla hata ya kuifanya dhana hii ya fasihi linganishi kuingizwa katika hali na hadhi hii ya kitaaluma tayari kulikuwapo na misingi kadhaa ya kikanuni iliyokuwa inafuatwa na jamii hizo katika kulinganisha utendekaji wa

fasihi zao na za jamii nyengine. Misingi hiyo ilikuwa inaongozwa na vionjo vya jamii zilizokuwa na nguvu ya kihadhi kama vile; jamii za Wayunani. Mathalani, zama za mwanafalsafa wa Kiyunani, Aristotle zilishuhudia kuwepo kwa ulinganishaji na ulinganuzi wa kazi mbali mbali za Tamthiliya kwa lengo la kuchuja na kupata kazi bora zilizowafikiwa kupelekwa kwa hadhira.

Pia, jamii za zama baada ya Kristo zilijihusisha na ulinganishaji na ulinganuzi wa matini za kidini (Biblia). Kadhalika, wasanii wa kiarabu wa enzi za kati walijishughulisha na ulinganishaji na ulinganuzi wa kazi za kisanaa. Hata hivyo, pamoja na kufanya mambo mengi yanayohusiana na ulinganishaji wa kazi za kisanaa zama hizo ni wazi kuwa ulinganishaji wenyewe ulifanywa kwa misingi isiyo rasmi.

Fasihi linganishi katika umbo la sasa la kitaaluma, ilianza mwishoni mwa karne ya 19 na kupata mashiko mwanzoni mwa karne ya 20. Kiusuli, kuibuka kwa dhana ya kufanya ulinganisho katika vipengele vya kifani kunanasibishwa na safari zilizokuwa zinafanywa na wataalamu mbali mabali katika sehemu tofauti za dunia. Ijapokuwa madhumuni ya safari hizo ilikuwa si kuzitalii fasihi au sanaa za sehemu hizo, bali ilidhihirika kuwa kulikuwa na tofaututi fulani walizozibaini katika utendekaji wa fasihi na sanaa kwa ujumla, hususani fasihi simulizi.

Maarifa ya awali ya taaluma hiyo yalijikita katika kulinganisha maudhui ya sanaa na kaida za maisha ya kila siku ya mwanadamu na mambo yamzungumkayo kama vile dini, siasa na matabaka. Wadau wakubwa wa fasihilinganishi wa mwanzoni walikuwa ni watu binafsi wachache kama vile; Paul Van Tieghem wa Ireland aliyeendesha makongamano huko Sorbonne kati ya mwaka 1827 na 1840. Wengine ni Dostoevsky na Marius Franco ambao walijitokeza katikati ya miaka ya 1800.

Jilala (2016), anamnukuu Zepetnek (1998), akifafanua misingi ya Nadharia ya Fasihi Linganishi ifuatavyo:

(i) Kutambua taaluma hii kwakuzingatia mbinu, stadi sahihi katika mafunzo ya fasihi kwa lengo la kuimarisha uhusiano wa fasihi linganishi na tamaduni nyengine.

(ii) Fasihi linganishi ni nadharia na pia ni mbinu muhimu inayodaiwa kujikita hasa katika uhusiano baina ya utamaduni, lugha, fasihi na maarifa.

(iii) Kuwa na hamu ya mwanafasihi linganishi mwenye uwezo mkubwa wa kutambua lugha na fasihi za jamii tofauti pamoja na maarifa mengineyo kwa undani na uhusiano wa nadharia na mbinu nyenginezo stahiki.

(iv) Kuwa na hamu ya kujifunza fasihi linganishi ikihusishwa na stadi nyengine kama (sanaa, filamu, utamaduni, maigizo na mengineyo) ambayo nayo yanahusishwa na matawi makuu ya taaluma ya sayansi jamii katika fani zake za Historia, Sosholojia, Saikolojia na nyenginezo.

(v) Kutambua na kujifunza lugha na fasihi katika mazingira yakuzingatia nadharia ya fasihi na matumizi yake lakini mazingira hayo yakienda sambamba na lugha ya kiingereza ambayo imekitwa katika taaluma nyingi za nasaba yake.

(vi) Kutambua nadharia na mbinu za fasihi linganishi zinazolenga na uhusishwaji wa utafiti na uchambuzi wake kwa lengo la kutolea ushahidi wake juu ya ubora na udhaifu.

(vii) Kuwa na hamu ya kuitumia vyema fasihi linganishi kwa kuzingatia nadhria na mbinu kuihusisha na mwamko wa kimawazo na kiitikadi ya siasa yake.

(viii) Kutambua vyema uhusiano na uhusishwaji wa kimaudhui baina ya kazi za sanaa kwakuzingatia wakati,mfumo,wahusika, upekee na madhumuni husika katika uhalisia na udhanaishi wake kitaifa na kiulimwengu.

(ix) Kuhamasika juu ya matumizi ya nadharia katik mfumo wa kiutandawazi, kiteknolojia, kiviwanda na mawasiliano katika utekelezaji wa maendeleo na kuhadharisha juu ya jamii, utaaifa, jinsia na mafunzo menginyo.

(x) Kuwa nashauku kubwa ya kujifunza nadharia ya fasihi linganishi ili kuweza kuwa mweledi na mjuzi kwa matumizi yake katika fasihi, sanaa na matumizi mengineyo stahiki.

Nadharia hii kwa miongo kadhaa inatumika kufanyia uchambuzi wa kazi za kifasihi hasa katika bara la Ulaya na Amerika. Hata hivyo, nadharia hii imekuwa ikikosolewa kwamba, fasihi linganishi haijitoshelezi kwa sababu ya kuchanganya taaluma mbali mbali kama vile Tafsiri, Nadharia ya Uhakiki, Anthropolojia, masomo ya Dini, Historia na Jiografia. Kwa mantiki hii inadaiwa kuwa ni rahisi sana kwa walinganishaji kuangukia katika dimbwi la unusu nusu wa maarifa.

Pamoja na kasoro hizo, nadharia ya fasihi linganishi inaonekana kuwa na ubora kutokana na kuwa ni somo la utafiti wa fasihi bila mipaka. Muono huu hutokana na matakwa ya msingi wa fasihi linganishi ambao ni kuwa na ujuzi na uwezo wa kusoma, kuandika, kuchunguza na kuhakiki hadhi ya kazi za jamii mbali mbali za kuanzia Mashariki hadi Magharibi; na Kaskazini hadi Kusini mwa dunia. Vilevile, fasihi linganishi inamtaka mdau wake azitalii kazi za vipindi mbali mbali kama vile; kazi za zama za giza hadi zile za ufufuo wa ustaarabu, za kabla ya ukoloni hadi zile za baada ya ukoloni na za urasimi mkongwe hadi zile za ulimbwende na uhalisia.

Kwa sifa hii utafiti huu umeona hauna budi ila kuitumia nadharia hii ili kufikia lengo la utafiti wetu.

Hivyo, katika utafiti huu Nadharia ya Mwingilianomatini na Nadharia ya Fasihi Linganishi zilitumika ili kumuongoza mtafiti kutathmini mbinu za kimtindo na dhamira zilizotumika katika tamthiliya teule ili kuona namna zinavyolingana na kutofautiana kutokana na lengo mahsusi la pili ambalo lilikuwa kulinganisha na kulinganua matumizi ya mitindo katika tamthlia teule za *Mashetani* na *Mashetani Wamerudi*.Pia tulizitumia kujibu lengo mahsusi la tatu ambalo lilikua nikulinganisha na kulinganua dhamira katika tamthilia teule za *Mashetani* na *Mashetani Wamerudi*

## 2.12 Hitimisho

Sura hii imepitia na kujadili vipengele vya msingi kuhusu dhana ya mtindo katika kazi za fasihi, tafiti kuhusu mitindo, tafiti kuhusu Tamthiliya teuele. Katika mapitio ya maandiko mtafiti alibaini kuwepo pengo la kimaarifa ambalo lilihitaji kuzibwa. Pengo la kimaarifa katika utafiti huu ni kutoonekana kwa kazi iliyotathimini na kulinganisha mitindo na dhamira katika Tamthiliya za Kiswahili kwa kutumia mifano ya Tamthiliya ya *Mashetani* ya Ebrahim Hussein na *Mashetani Wamerudi* ya Said Ahmed Mohammed ili kuona ni jinsi gani wasanii hawa ambao wanatoka katika mazingira tofauti na kazi hizo zilizoandikwa katika vipindi tofauti zinalingana na hata kutofautiana katika matumizi ya vipengele vya kimtindo na dhamira kwa mkabala wa Nadharia ya Fasihi Linganishi na Nadharia ya Mwingilianomatini. Aidha, katika sura hii mumeelezwa nadharia zilizoongoza utafiti huu ambazo ni Nadharia ya Mwingilianomatini na Nadharia ya Fasihi Linganishi.

# SURA YA TATU

# MBINU ZA UTAFITI

## 3.1 Utangulizi

Sura hii inajadili juu ya mkabala wa utafiti, mbinu na vifaa ambavyo vilitumika katika utafiti huu. Sura hii imegawanyika katika sehemu kuu nane, sehemu ya kwanza inahusu eneo ambalo utafiti ulifanyika, sehemu ya pili ni usanifu wa utafiti, sehemu ya tatu ni kundi lengwa, sehemu ya nne ni sampuli na mbinu za usampulishaji na sehemu ya tano ni ukusanyaji wa data. Sehemu ya sita inabainisha na kueleza mbinu za ukusanyaji wa data, sehemu ya saba ni mkabala wa uchambuzi wa data za utafiti na sehemu ya nane inaelezea usahihi, kuaminika na maadili ya utafiti. Sura hii inamalizia kwa kutoa hitimisho.

## 3.2 Eneo la Utafiti

Kwa mujibu wa Enon, (1980), anaeleza kuwa eneo la utafiti la kigeografia ni sehemu ambapo mtafiti amekwenda au ametumia katika kukusanya data za utafiti wake. Eneo la utafiti unafanyika kulingana na vile mtafiti alivyopendekeza ili kupata data za kujibu maswali ya utafiti wake. NayeCreswell (2009), anasema eneo la utafiti huteuliwa kulingana na lengo kuu la mtafiti kwamba eneo hilo lililoteuliwa ni lazima liweze kutoa data za kukamilisha malengo mahsusi ya utafiti.

Kwa hivyo eneo la utafiti huu lilikuwa katika maktaba ya Chuo Kikuu Huria cha Tanzania, Maktaba ya Chu Kikuu cha Dar es salaam katika Taasisi ya Taaluma Kiswahili (TATAKI), maktaba kuu Pemba, iliopo Chake chake na maktaba ya Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar (SUZA). Maeneo hayo yalichaguliwa na mtafiti

kwa sababu utafiti huu ni wa maktabani. Pia, mtafiti aliamini kuwa sehemu hizo zitamuwezesha kupata dataza utafiti wake kwa uhakika, haraka na wepesi.

## 3.3 Usanifu wa Utafiti

Utafiti huu ulitumia umbo la kimaelezo. Enon (1999), anasema kuwa umbo la kimaelezo ni njia ya kukusanya data na kuzifanyia uchambuzi kwa njia ya maelezo bila ya kutumia tarakimu. Umbo la utafiti pia hujuulikana kwa jina jengine kama ni usanifu wa utafiti yaani *research design*. Usanifu wa utafiti ni mchoro au ramani unaoonesha namna utafiti utakavyofanyika tangu kukusanya data na kuandika ripoti ya utafiti Robson (2007).

Hivyo, data za utafiti huu zilikusanywa, kuchambuliwa na kuwasilishwa kwa njia ya kimaelezo. Pia, majadwali yalitumika katika kuwasilisha data za utafiti huu kwa kiwango kidogo. Mtafiti alitumia mbinu hii kwa sababu ni rahisi katika kuchambua data za kifasihi hasa ikizingatiwa kuwa fasihi ni sanaa ya maneno.

## 3.4 Kundi Lengwa

Cooper (1989) anafasili kundi lengwa kuwa ni wanachama wote au hata mmoja, kundi au elementi ambazo mtafiti amekusudia kuzihusisha katika utafiti wake. Aidha kundi lengwa ni jumla ya watu au vitu vyote ambavyo mtafiti amevikusudia kuvifanyia utafiti (Kombo na Tromp 2006; Enon 1998). Hivyo basi, kundi lengwakatika utafiti huu walikuwa ni waandishi wa tamthiliya teule ambao ni Ebrahim Hussein wa tamthiliya ya *Mashetani* na Said Ahmed Mohammed wa tamthiliya ya *Mashetani Wamerudi.* Mtafiti aliwateua watunzi wa tamthiliya hizo kwa kuamini kuwa kuna muathiriano na muachano wa kimtindo na kidhamira katika

Tamthiliya hizo. Kwa mantiki hiyo, aliona ipo haja ya kuweka wazi suala hilo kwa misingi ya kisayansi.

### 3.5 Sampuli na Usampulishaji

Kothari (1999) anasema kuwa sampuli ni istilahi inayotumika kumaanisha sehemu ya watu au vitu vinavyotafitiwa kutoka katika kundi kubwa. Sehemu hiyo huteuliwa na mtafiti kwa kuzingatia sifa na tabia zao ambazo zinaweza kukidhi katika kuwakilisha kundi kubwa la watu vitu. Pia, Bryman (2004), anasema sampuli ni mchakato wa kuchagua kikundi cha vitu au watu ili kitumike katika utafiti kama kiwakilishi cha kundi lolote linalotafitiwa kwani sio rahisi kutafiti kundi zima.

Uteuziwa sampuli, kama unavyoelezwa na Bryman (2004), ni mchakato wa kuchagua kikundi cha watu au vitu ili kitumike katika utafiti kama kiwakilishi cha kundi lote linalotafitiwa kwavile sio rahisi kutafiti kundi zima. Utafiti huu ulitumia mbinu ya madhumunimaalumu katika kupata sampuli yake. Powell na Connaway (2004), wanasema kuwa katika uteuzi wenye madhumuni maalumu sampuli huteuliwa kutegemea vigezo vinavyohusiana na maswali ya utafiti kuliko kigezo cha nasibu au kubahatisha, hivyo wanaochaguliwa huteuliwa kutokana na nafasi zao kwa kuamini kwamba ndio rasilimali ya utafiti husika kwa kupata data zitakazojitosheleza kukamilisha utafiti.

Kwa ujumla, Usampulshaji ni utaratibu maalum anaoutumia mtafiti kuweza kupata kundi maalum la watu au vitu watakaotafitiwa ili waweze kuwakilisha kundi kubwa la watafitiwa. Mtafiti huteuwa kundi hilo ili kukidhi mahitajio yake kwa mujibu wa malengo, maswali na mada ya mtafiti ipasavyo. Kwa maana hiyo mtafiti huhitajika

kujua ni aina gani sampuli atakayoichagua ili kutimiza mahitajio yake ya utafiti. Katika utafiti huu, mtafiti atatumia mbinu ya usampulishaji lengwa ili kufanikisha utafiti wake vyema.

Katika utafiti huu, mbinu ya usampulishaji lengwa ilitumika kwa lengo la uteuzi wa Tamthiliya teule ambapo ilikuwa ni imani ya mtafiti kuwa mbinu hiyo ni mwafaka katika kutimiza malengo na kujibu maswali ya utafiti huu. Kwa kupitia mbinu hiyo Tamthiliya teule ni *Mashetani* na *Mashetani Wamerudi*. Kulingana na malengo ya utafiti huu mbinu hii ilionekana kufaa kutokana na tatizo la utafiti huu kujikita katika kutathmini matumizi ya mtindo na dhamira katika Tamthiliya za *Mashetani* na *Mashetani Wamerudi* ili kuona namna vipengele hivyo vinavyofanana na kutofautiana katika Tamthiliya teule.

## 3.6 Ukusanyaji wa Data

Kwa kawaida mtafiti yeyote yule pindi akifanya utafiti wa kitaluma ni lazima atumie vyanzo vya aina mbili vya data ambavyo ni data za msingi na data za upili. Hivyo basi, katika utafiti huu tulikusanya data za msingi na zile za upili ili kuweza kukamilisha malengo ya utafiti huu.

### 3.6.1 Data za Msingi

Data za msingi ni data ambazo zinakusanywa kwa mara ya kwanza na mtafiti na hazijawahi kukusanywa na mtafiti mwengine yeyote kwa lengo na matumizi kama yanayofanywa na mtafiti (Furlong, 2000). Data za msingi pia hujulikana kama data ghafi ambazo ndiyo kwanza zinaingia katika taaluma ya utafiti kwa mara ya kwanza tayari kwa ajili ya kuchambuliwa na kuchanganuliwa. Data hizo

zikishachambuliwa na kuandikwa katika ripoti au tasinifu hubadilika jina na kuwa ni data za upili (Young, 1984). Kwa hivyo, data za msingi katika utafiti huu zilikusanywa kutoka katika Tamthiliya ya*Mashetani* na Tamthiliya ya *Mashetani Wamerudi*.

### 3.6.2 Data za Upili

Kothari (1990) anaeleza kwamba data za upili ni data ambazo tayari zimeshaingizwa kwenye machapisho ambayo mtafiti huyasoma kuhusiana na mada yake ya utafiti ili kupata uelewa na kushadidia hoja zitokanazo na data za msingi. Naye Creswell (2009), anasema data za upili ni zile ambazo tayari zilikwishakusanywa na watafiti wengine kwa ajili ya kutimiza malengo ya utafiti wao na kuandikwa katika ripoti, makala, majarida, wavuti na vitabu, tayari kwa ajili ya kusomwa kama marejeleo katika maktaba mbali mbali. Data za upili pamoja na kutumika kushadidia data za msingi katika uchambuzi wa data lakini pia hutumika katika sura ya pili ya tasnifu inayohusiana na mapitio ya kazitangulizi zinahusiaina na mada inayotafitiwa (www.cles.org.uk/wp-content/uploads/2011 /01/research methods-handbook.pdf). Nia kuu ya kukusanya data za upili ni kwa ajili ya kujazilishia na kukazia maarifa yanayotolewa kupitia data za msingi.

Data za upili katika utafiti huu zilikusanywa kutoka katika machapisho yapatikanayo Chuo Kikuu Huria cha Tanzania, maktaba kuu Chake Chake Pemba, Maktaba ya Chuo Kikuu Huria cha Tanzania, kituo cha Pemba na maktaba za Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar (Suza). Katika maktaba hizi mtafiti alisoma makala, ripoti, tasnifu, majarida, vitabu na maandishi pepe katika wavuti natovuti zinazohusiana na mada ya utafiti huu.

### 3.7 Mbinu za Kukusanya Data

Katika utafiti huu mbinu kadhaa zilitumika katika kukusanya data. Kothari (1990), anafafanua dhana ya ukusanyaji wa data kama ni zoezi la awali katika utafiti ambalo humuwezesha mtafiti kupata taarifa atakazozihitaji katika kufanikisha lengo lake la utafiti. Pia, mbinu za kukusanya data huweza kufafanuliwa kama njia zinazotumika katika kufanikisha zoezi la kukusanya data za utafiti. Ni taratibu na vifaa anavyovitumia mtafiti katika kufanya uchunguzi, kuhifadhi na kuchambua data za utafiti.(www.hcmuaf.edu.vn/data/quoctuan/researchmethodology-methodsand techniques 2004).

Hivyo, data za utafiti huu zilikusanywa kwa kutumia mbinu za upitiaji wa nyaraka maktabani na usomaji makini wa tamthiliya teule. Mbinu ya upitiaji wa nyaraka ilitumika katika kukusanya data za upili na mbinu ya usomaji makini ilitumika katika kukusanya data za msingi.

#### 3.7.1 Upitiaji wa Nyaraka

Utafiti huu ulitumia mbinu yaupitiaji nyaraka. Hucker ( 2001), anafafanua neno nyaraka kuwa ni kitu chochote kilichoandikwa au kuchapishwa ambacho humsaidia mtafiti kupatadata za utafiti wake. Naye Kothari (2008), anashadidia kwa kusema kwamba neno"nyaraka" linarejelea machapishona maandiko mbali mbali yanayopatikana katika maktaba. Kimsingi, mbinu ya upitiaji wa nyaraka maktabani ni mbinu ya kukusanya data za upili kwa mtafiti, kukusanya machapisho yanayohusiana na mada yake ya utafiti na kuyasoma kwa uzingativu. Aidha, Merrian (1998), anaeleza kuwa katika maktaba mtafiti huweza kupata data nyingi, kwa urahisi bila gharama. Data za upili pamoja na kutumika katika kushadidia hoja

zitokanazo na data za msingi katika uchambuzi wa data lakini pia hutumika katika uandishi wa sura ya pili ya tasinifu inayohusika na “Mapitio ya kazi Tangulizi na Mkabala wa Kinadharia.” Data za upili katika utafiti huu zilikusanywa kutoka katika machapisho yanayopatikana katika Maktaba za Chuo Kikuu Huria cha Tanzania, Maktaba ya Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar (SUZA), Maktaba Kuu Chake Chake Pemba. Katika maktaba hizi mtafiti alisoma makala, ripoti, tasinifu, majarida, vitabu na maandishi pepe katika wavuti na tovuti zinazohusiana na mada yake na kwa kuangalia malengo mahsusi ya utafiti wake.

### 3.7.2 Usomaji Makini wa Nyaraka

Flick (2011) anafafanua kwamba usomaji makini ni mbinu ya kukusanya data za msingi ambapo mtafiti huchambua mambo yaliyomo katika makala za mwanzo zinazohusiana na mada ya utafiti. Mbinu hii humfanya mtafiti kuzigawa na kuzisoma matini mbali mbali zitakazohusiana na mada ya utafiti pamoja na kuchukuwa maelezo, sentensi au maneno.

Kothari (2008), anaieleza dhana ya usomaji makini au wakati mwingine hujulikana kama usomaji wa kina kama mbinu ya kukusanya data za msingi kutoka katika matini zilizoteuliwa katika utafiti. Kupitia mbinu hii, mtafiti huteua matini maalumu na kuzisoma matini hizo kwa kina huku akidondoa baadhi ya maneno, sentensi au aya ambazo ndizo huwa data za utafiti wake. Salim (2015), anasema kuwa husemwa ni mbinu ya usomaji makini kwa sababu mtafiti husoma kazi hizo tena na tena hadi pale anapojiridhisha kuwa sasa amepata data alizokuwa anazihitaji katika kukamilisha malengo ya utafiti wake.

Kwa hivyo, data za msingi katika utafiti huu zilikusanywa kwa kutumia mbinu ya usomaji makini kutoka katika Tamthiliyaza *Mashetani* na *Mashetani Wamerudi*. Katika kufanikisha zoezi la ukusanyaji wa data, mtafiti aliandaa shajara maalumu ambapo aligawanya kulingana na malengo mahususi ya utafiti huu ikiwa na kichwa cha habari kinachohusiana na malengo mahususi ya utafiti wake. Hii ilirahisisha zoezi la ukusanyaji wa data.

### 3.8 Mkabala wa Uchambuzi wa Data za Utafiti

Uchambuzi wa data ni kitendo muhimu sana katika kuhakikisha kuwa matokeo ya utafiti yanapatikana na hivyo utafiti mzima nao kukamilika. Katika utafiti huu tulitumia mbinu ya mkabala wa kimaelezo kuchambua na kujadili data za utafiti na matokeo yake. Kothari (1990) anaeleza kuwa mkabala wakimaelezo ni mbinu ya uchambuzi wa data ambapo mtafiti huzichambua data zake kwa kuzitolea maelezo yanayohusiana na madhumuni ya utafiti wake.

Mbinu ya kimaelezo hutumika sana katika kuchambua data zinazohusiana na fasihi kwa sababu fasihi ni taaluma ya maneno aidha ya kuandikwa au kuzungumzwa. Hata hivyo, haina maana kuwa katika uwasilishaji na uchambuzi wa data za utafiti hatuwezi kutumia mbinu ya mahesabu, huweza kutumika pia. Mbinu ya maelezo ilitumika ili kuchambua data tulikazozikusanya kwa mbinu ya usomaji makini. Mtafiti ameona mbinu hii ya uchambuzi wa data ilikuwa rahisi kufikia malengo ya utafiti huu. Pia, mtafiti alitumia mbinu hii kwa sababu mada ya utafiti wake imejikita katika usanii wa kimtindo na uwasilishaji wa dhamira, hivyo basi, mbinu hii ilifaa kufikia lengo la utafiti huu.

## 3.9 Usahihi, Kuaminika na Maadili ya Utafiti

### 3.9.1 Usahihi wa Data

Usahihi wa mbinu za kukusanyia data ni utaratibu unaowezesha kupatikana kwa data sahihi na za kuaminika za utafiti (Cohen na wenzake, 2000). Usahihi wa data katika utafiti huu ulihakikishwa kwa kutumia mbinu ya usomaji makini wa Tamthiliya teule na upitiaji wa nyaraka. Katika uchambuzi wa data, mkabala wa kimaelezo ndio uliotumika. Usahihi wa mbinu hizi unatokana na ukweli kuwa upungufu wa kila moja unakamilishwa na ubora wa mbinu nyengine. Vile vile, usahihi wa mbinu na nadharia za uhakiki wa fasihi zilizotumika katika utafiti huu zilijadiliwa katika mjadala baina ya mtafiti na msimamizi wake.

### 3.9.2 Kuaminika kwa Data za Utafiti

Kuaminika kwa data za utafiti kunatokana na uwezo wa mbinu za utafiti kutoa matokeo yale yale ya utafiti unaporudiwa kwa kutumia mbinu zile zile (Kothari, 2008). Kuaminika kwa data kunajitokeza pale ambapo kunakuwa na uhusiano ama ulingano katika taarifa zinazotolewa na watu wale wale kwa muda tofauti (Furlong na Lavelace, 2000). Katika utafiti huu, kuaminika kwa data kulihakikishwa kwa kutumia nadharia ya Fasihi Linganishi na Nadharia ya Mwingilianomatini na mbinu nyengine mchanganyiko za kukusanyia data.

### 3.9.3 Maadili ya Utafiti

Maadili ya utafiti huhusishwa na mila na desturi ambayo jamii huyaamini katika eneo ambalo mtafiti analenga kuchunguza kitu au jambo fulani. Lengo la maadili katika utafiti ni kulinda mambo ya kibinaadamu yanayoaminiwa na jamii. Pia, kuhakikisha kuwa utafiti unafanyika katika muktadha unaokubalika; kwa mtu mmoja

mmoja, kikundi cha watu au jamii kwa ujumla na kuhakikisha kuwa miradi ya kiutafiti inazingatia maadili kama vile; masuala ya uongozi na athari zake, utunzaji siri na utoaji wa habari (http://researchethics). Miongoni mwa vitu muhimu anavyotakiwa mtafiti kuvizingatia ni maadili ya utafiti yanayohusu kupata kibali cha kufanya utafiti na kutunza siri za watafitiwa. Hivyo, katika utafiti huu, maadili ya utafiti yalizingatiwa ipasavyo kabla na baada ya kukusanya data. Kwasababu utafiti wetu ulikuwa wa maktabani tulihakikisha kuwa madondoo kutoka katika Tamthiliya teule yanafanywa kwa usahihi na umakini na baadae kuchambuliwa kifasihi kwa kuongozwa na Nadharia ya Fasihi Linganishi na Nadharia ya Mwingilianomatini.

## 3.10 Hitimisho

Sura hii ya tatu ya utafiti tunaweza kuiita kuwa ni sehemu ya ufundi na utaalamu kwani imeeleza mambo ambayo ni ya msingi sana katika kuwezesha ukusanyaji na uchambuzi wa data za utafiti. Katika kuufanya utafiti wetu kukamilika na kuwa wa kitaaluma tulikusanya data za msingi na data za upili kwa kutumia mbinu za upitiaji wa nyaraka maktabani na usomaji makini wa Tamthiliya teule. Data za upili zilitumika katika kushadidia hoja zitokanazo na data za msingi ili kuimarisha uchambuzi na matokeo ya utafiti kwa jumla. Pamoja na hayo, katika sura hii pia tumeeleza watafitiwa, sampuli na mbinu ya usampulishaji.Vile vile, sehemu hii imeeleza eneo la utafiti huu, usahihi, kuaminika na maadili ya utafiti.

# SURA YA NNE

# UWASILISHAJI, UCHAMBUZI NA MJADALA WA DATA ZA UTAFITI

## 4.1 Utangulizi

Sura hii imefanya uwasilishaji, uchambuzi na mjadala wa data za utafiti. Katika hali ya kawaida ni katika sura hii ndiko kunakoelezwa mambo yaliyogundulika katika utafiti wa aina yoyote. Mambo hayo hufafanuliwakufuatana na malengo ya utafiti yaliyowekwa. Kwa muktadha huo uwasilishaji na uchambuzi wa data katika sura hii umefanywa kwa kuzingatia madhumuni mahususi (malengo mahsusi) ambayo yalikuwa matatu.

Lengo mahususi la kwanza lilikuwa nik`ubainisha matumizi ya mitindo katika Tamthiliya teule ya *Mashetani* na *Mashetani Wamerudi.*Lengo mahsusi la pili ni kulinganisha na kulinganua matumizi ya mitindo katika tamthiliya ya *Mashetani* na *Mashetani Wamerudi* na lengo mahsusi la tatu ni kulinganisha na kulinganua dhamira zinazojitokeza katika Tamthiliya teule za *Mashetani* na *Mashetani Wamerudi.*

Sura hii imegawanyika katika sehemu kuu nne. Sehemu ya kwanza imehusu matumizi ya vipengele vya mtindo katika Tamthiliya teule.Sehemu ya pili ni namna tamthiliya teule zilivyofanana na kutofautiana katika matumizi ya mitindo.Sehemu ya tatu inahusu kulingana na kutofautiana kwa dhamira katika tamthiliya teule na sehemu ya nne ni hitimisho. Madhumuni mahususi yamefafanuliwakatika uchambuzi wa data kwa mfuatano huu huu baada ya kueleza usuli wa waandishi teule na muhtasari wa Tamthiliya teule kama ifuatavyo:

## 4.2 Muhtasari wa Tamthiliya ya *Mashetani*

Tamthiliyaya *Mashetani* ni tamthiliyaambayo ilitungwa na msanii Ebrahim N. Hussein na kuchapishwa kwa mara ya kwanza mnamo mwaka (1971). Tamthiliya hii ni tamthiliya ya kimajaribio inayosawiri mazingira ya kikoloni kwa mchezo kati ya Juma na Kitaru ambapo kati yao Kitaru ni binadamu na Juma ni shetani. Hii ni tamthiliya inayoakisi ukoloni mkongwe katika nchi za dunia ya tatu. Tamthiliya hii ilimtumia muhusika shetani kama jazanda ya ukoloni na binadamu kama raia wa nchi za ulimwengu wa tatu na jinsi raia hao walivyoathiriwa na ukoloni.

Pia, Hussein katika tamthiliya ya *Mashetani* ameonesha kuwa elimu ya kikoloni imeleta mkanganyiko katika fikra za wananchi na kupelekea matabaka yanayohasimiana katika jamii. Kundi lililobahatika kupata elimu ya kimagharibi linaitumiaelimu hii kama ni nyenzo ya kupata madaraka, nafasi za uongozi na kutwalia mali za umma. Fursa hizi zinatumiwa vibaya na vibaraka wa ukoloni mamboleo ili kuwanyanyasa na kuwakandamiza waliokosa elimu hio. Kimsingi elimu ya kikoloni inaonekana kutowasaidia wananchi kwani haiendani na mazingira na mahitajio yao. Wanapokea sera na mikataba kikasuku bila ya kuhakiki faida na hasara zake.

## 4.3 Muhtasari wa Tamthiliya ya *Mashetani Wamerudi*

Tamthiliya ya *Mashetani Wamerudi* ni Tamthiliyailiyotungwa na msanii Said Ahmed Mohamed na kuchapishwa kwa mara ya kwanza mwaka (2016). Tamthiliya hii inahusu mjadala mzito kuhusu ukoloni katika nchi za dunia ya tatu na jinsiulivyoathiri na unavyoendelea kuathiri nchi hizo.Msanii wa Tamthiliya hii amemtumia muhusika Sheta kuonesha ukoloni mamboleo katika muktadha wa

kiutandawazi na muhusika Prof.ni ishara ya wanajamii katika nchi za dunia ya tatu ambao wanaonekana kuwa na muamko na msimamo mkali wa kutaka kuondokana na ukandamizaji na kuazimia kujikomboa ili kuleta mabadiliko katika jamii zao kwa kushirikiana na kuwa bega kwabega na wahusika kama Vijana na Msichana.

*Mashetani Wamerudi* ni Tamthiliya inayoleta mivutano baina ya pande mbili; upande wa mashetani (wakoloni) na vibaraka wao, na upande wa vijana na wazee wanaochachamaa katika kutafuta mabadiliko na ukombozidhidi ya ukoloni mamboleo katika bara la Afrika. Tamthiliya hii inaonesha mgogoro kati ya mhusika Prof. na Sheta. Mwisho wa mvutano Profesa Hafi – leo –wala-kesho anakufa kifo cha ajabu na kuleta tanzia pamoja na tamaa ya kuamsha silaha ya ukombozi!

## 4.4 Vipengele vya Mtindo katika Tamthiliya ya *Mashetani*

Lengomahsusi la kwanza katika utafiti huu linahusu kubainisha vipengele vya mtindo katika tamthiliya ya *Mashetani* na *Mashetani Wamerudi.* Lengo hilo la limekwenda sambamba na swali la msingi la kwanza la utafiti huu linalosema: Ni mitindo gani iliyotumika katika Tamthiliya teule ya *Mashetani* na *Mashetani Wamerudi?* Mtafiti amezingatia kwa kina lengo na swali hilo la kwanza la utafiti huu na amebainisha mitindo mbalimbali iliyojitokeza katika Tamthiliya ya *Mashetani* na baadae tamthiliya ya *Mashetani Wamerudi* kama ifuatavyo:

### 4.4.1 Uteuzi wa Msamiati katika *Mashetani*

TUKI (2004), wanafasili dhana ya msamiati kwa kueleza kuwa ni jumla ya maneno yote katika lugha. Data za utafiti huu zinaonesha kuwa mwandishi wa Tamthiliya ya *Mashetani* ameteua misamiati ambayo inasawiri ujumbe alioukusudia. Katika

Tamthiliya ya *Mashetani,* msamiati umeteuliwa kulingana na lengo la dhamira za mtunzi na kulingana na sifa ya mhusika. Mfano matumizi hayo ya msamiati ni: *Shetani (uk.1), chewa (28), mbuyu (uk.1), pango (uk.1), jini (uk.1), rafiki (uk.3), upepo (uk.5), waltz (uk.8), kisu (uk.9), Gashalazeritwas (uk.4)* na kadhalika.

Wamitila (2008), anasema kuwa uchunguzi wa msamiati hupaswa kuchunguza masuala ya lugha sanifu na isiyokuwa sanifu na labda umuhimu wake. Katika Tamthiliya ya *Mashetani*, maneno haya mathalani *shetani, jini, mbuyu, pango* na *waltz* yalitumika kijazanda kusawiri uhasama na mgogoro uliokuwepo baina ya wakoloni na watawaliwa wakati wa ukoloni. Hali hiiilijitokeza kwa sura tofauti baada ya nchi za Kiafrika kupata uhuru wa bendera. Watawala wazawa walichukua madaraka na kuanza kuyatumia kwa manufaa yao na hivyo kuwakaribisha wakoloni kuendelea kunyonya bara hili kwa manufaa ya wachache.

### 4.4.2 Mpangilio wa Maneno katika *Mashetani*

Mwandishi wa Tamthiliya ya *Mashetani* amezingatia sana upangiliaji wa maneno katika sentensi kama zilivyo taratibu za lugha ya Kiswahili. Taratibu za utungaji wa sentensi za Kiswahili huwa na *kiima* na kufuatiwa na *kiarifu*; na *kikundi nomino* na kufuatwa na *kikundi tenzi*. Mifano ya uzingativu wa mpangilio wa sentensi umejitokezakama ifuatayo:

*(i)* *Unanijua mimi nani? (uk. 1).*

*(ii)* *Una maana sikufaulu? (uk. 7).*

*(iii)* *Umepata kumsikia nani akijichinja mwenyewe? (uk. 8).*

*(iv)* *Kosa limefanyika (uk. 11)*

*(v)* *Mpanda ngazi na mshuka ngazi hawawezi kushikana mikono (uk. 56)*

Mifano hiyo inaonyesha kuwa mwandishi wa *Mashetani* amefuata mpangilio wa Kiswahili sanifu katika kupanga maneno ya lugha ya Kiswahili katika sentensi. Kama hali hii inavyoshadidiwa na Massamba na wenzake (2003), wanaposema kuwa sentensi za Kiswahili huanza kwa Kiima na kufuatiwa na Kiarifu. Katika mfano nambari (i) hadi (iii) tunaona kuwa japo kiima hakijidhihirishi kwa kuwa na nomino inayoonyesha kuna nomino kapa ambayo inajenga sentensi hiyo na uwepo wake - unajidhihirisha katika kitenzi. Hivyo, tunaweza kusema kuwa Mwandishi wa tamthiliya*Mashetani* amezingatia kwa kiasi fulani upangiliaji wa maneno katika sentensi zake.

### 4.4.3 Matumizi ya Lugha katika *Mashetani*

Data zilizokusanywa na mtafiti kutoka katika tamthiliya ya *Mashetani* zilionesha kuwa tamthiliya hii imetumia vipengele anuai vya matumizi ya lugha kama mbinu ya kimtindo. Vipengele hivyo vilifanyiwa uchambuzi na kuwasilishwa katika Jadweli kama ifuatavyo:

**Jedweli Na. 4.1: Matumizi ya Lugha katika *Mashetani***

| Nambari | Kipengele cha Lugha |
|---|---|
| 1 | Jazanda |
| 2 | Ishara |
| 3 | Taswira |
| 4 | Misemo |
| 5 | Tamathali za semi |
| 6 | Nahau |
| 7 | Methali |
| 8 | Mdokezo |
| 9 | Mchanganyo ndimi |
| 10 | Nidaa |

Chanzo: Data za utafiti kutoka Tamthiliya ya *Mashetani*, Julai 2017

**Kielelezo namba 1** hapo juu, kinaonesha vipengele vya lugha ambavyo vimetumika katika Tamthiliya ya *Mashetani* kama inavyojionesha. Miongoni mwa vipengele hivyo ni tamathali za semi, misemo, nahau, methali, mdokezo, mchanganyo ndimi na nidaa. Vipengele hivyo vimefanyiwa uchambuzi na mtafiti kama ifuatavyo:

#### 4.4.3.1 Matumizi ya Jazanda katika Mashetani

Ngesa na wenzake (2015), wanasema kuwa jazanda ni utumiaji wa maneno kimafumbo ambapo neno hutumiwa ili kuwakilisha jambo jengine. Data zilizokusanywa katika Tamthiliya ya *Mashetani* zinaonesha kuwa Tamthiliya hiyo imetumia mtindo wa kijazanda. Mtindo huu unajidhihirisha kama ufafanuzi unavyoonesha hapo chini.

##### 4.4.3.1.1 Jazanda ya Ukweli

Katika ukurasa wa (12, 56 na 57), jazanda ya neno "ukweli" imetumika kuonesha kuwa ukweli ni silaha madhubuti ya kutuondoa katika mkanganyiko na migogoro yote katika jamii zetu. Mwandishi amedhirisha jazanda hii kama ifuatavyo:

*Ukweli?*

*Ukweli ndio upi?*

*Ukweli ni huu….Kuna lile lipaswalo kufanywa,na yule apasayekulifanya.*

*Mimi-mimi au yeye-mimi anayetaka kulitekeleza azimio hili?*

*Kamasiujuwi ukweliwa swali hili basi siujui ukweliwa kitendo changu,maisha yangu wala azimi langu*

*(Uk 12).*

#### 4.4.3.1.2 Jazanda ya Kisu

Neno“*Kisu*” kama jazanda kimetumika katika Tamthiliya ya *Mashetani*kuwakilisha uwezo, juhudi au maarifa ambayo Waafrika waliotawaliwa na wakoloni walijipatia na ambayo yaliwawezesha kupigania uhuru wao hatimaye kumwondoa mkoloni. Msanii anasema:

*SHETANI/: Wakati wangu wa kufa umefika.*
*“(Shetanina Binadamu wanatazamana. Wote wanatabasamu. Shetani anampa Binadamu kisu. Wanashikana…)” (uk.* 8).

#### 4.4.3.1.3 Jazanda ya Neno “Chewa”

Katika Tamthiliya hii neno “*chewa”* limeteuliwa na mwandishi likiwakilisha nguvu na ulafi w/a wakoloni katika kutaka kujipatia maslahi yao. Chewa ni kiumbe mkubwa aishiye baharini mwenye uwezo wa kumeza kila kitu kilichomo baharini. Kiumbe huyo anaweza kubadili mwelekeo wa meli au mashua kwa kuvuta mkondo wa maji na kulazimisha chombo hicho kwenda asikotaka nahodha. Msanii anatumia ndoto ya Kitaru kutusimulia hadithi ya chewa huyo kwa kusema:

> *“KITARU: Hadithi ya chewa. Mbali sana ukivuka bahari saba, kuna chewa mkubwa. Chewa huyu akivuta pumzi maji yote yanakupwa, maji yote yanaingia kinywani mwake. Anaweza kutoka huko aliko, kuivuta na kuimeza mashua yoyote anayoitaka. Mashua inavutwa tu na mkondo wa maji, ikitaka isitake. Na huyu chewa siyo chewa bali Shetani” (uk. 28).*

Kwa hiyo neno *chewa* limeteuliwa na msanii na kutumika kimajazi ili kuonesha tabia ya ulafi na nguvu ya wakoloni hasa katika mfumo wa ukoloni mamboleo. Katika mfumo huu wa kijamii, nchi changa huwa hazina uwezo na haziwezi kujiamulia mambo yahusuyo ustawi wao mpaka nchi za kibeberu ziwaoneshe njia ya kupita ndipo waweze kunufaika kiuchumi.

#### 4.4.3.1.4 Jazanda ya Neno "w*altz*" na "*Gashalazeritwas*"

Maneno haya yaliteuliwa ili kusawiri aina ya mahusiano baina ya nchi za Kiafrika na watawala wao wa zamani. Upokeaji na utekelezaji wa sera na mifumo ya utawala bila kuihakiki kunakoashiriwa na uchezaji wa ngoma kama ya "*waltz"* unaonesha kuwa uhuru uliopatikana katika nchi nyingi za Afrika ni wa bendera. Jazanda kama "*Gashalazeritwas"* unasawiri pia athari za kigeni katika mifumo yetu ya elimu kama matumizi ya lugha za watawala wetu wa awali, mathalani lugha ya Kijerumani. Kimsingi neno "*Gashalazeritwas"* linaakisi athari za Kijerumani katika utawala wa nchi zilizotawaliwa na Wajerumani. Inashangaza pia kuona kuwa sherehe za kupatikana kwa uhuru zinasherehekewa kwa ngoma ya "*waltz"* ambayo ni utambulisho wa utamaduni wa Shetani. Kwa uteuzi wa neno hili msanii ametuonesha kuwa katika jamii zetu tunaamini kuwa tuko huru wakati ambao bado tunatekeleza mipango ya watawala wetu wa kikoloni wa zamani kupitia sera za uwekezaji, na utekelezaji wa mipango ya maendeleo kama inavyoelekezwa na nchi za kibeberu. Mwandishi amedihirisha hayo kama ifuatavyo:

*Shetani: Hebu basi nikunong'oneze maana siriyenyewe ni kwa lugha ya kishetani. Liseme neno nililokufunza*
*Binaadamu: Gashalazeritwas*
*Shetani: Sema nikusikie*
*Binaadamu: Gashalazeritwas*
*Shetani: Sema kwa dhati yako*
*Binaadamu: (Anasema kwa dhati) Gashalazeritwas*
*Shetani: Sasa acha likuumize*
*Binaadamu:(Linamuumiza) Gashalazeritwas*
*Shetani: Sema likutoe damu*
*Binaadamu: Linamtoa damu Gashalazeritwas (uk 3 na 4)*

Kwa hakika dhana ukoloni mamboleo bado inaendelea kuchukua nafasi katika maisha yetu ya kila siku ikiwemo katika jamii za kiafrika. Hivyo ni vyema Waafrika

wakaendelea kuwa natabia ya kusimamia misingi ya kimaendeleo kutoka katika jamii zao ili kupiga vita ukoloni mamboleo.

#### 4.4.3.1.5 Jazanda ya Neno "Mheshimiwa"

Salem (2013), anasema kwamba jazanda hii ilitumika wakati wa utawala wa kikoloni kwa nia ya kuonesha ubwana dhidi ya mtu mweusi (utwana). Mara baada ya uhuru msamiati huu ulibadilishwa. Nia kuu yakufanya hivyo ilikuwa ni kuonesha matumaini yatokanayo na kuangushwa kwa utawala wa kikoloni. Msamiati *mheshimiwa* ulianza kutumiwa na watu wa kada na rika mbalimbali kuwatambulisha watu wenye uwezo kiuchumi au wale wanaonasibishwa na tabaka tawala. Kasumba ya kupenda kuitwa *mheshimiwa* pia ilikuwa maarufu kwani viongozi wa Kiafrika waliojiona kuwa wanastahili kuitwa hivyo kwa kuleta uhuru wa nchi zao.Msanii anaeleza kama ifuatavyo:

KITARU: *Ah, Mheshimiwa.*
JUMA: *Unasemaje chief? Nasikia unalala tu. Holiday inakupa time kidogo. (uk. 14)*

Dhana ya kuitana mheshimiwa bado inaonekana kuchukua nafasi kwa jamii zetu. Watawala wengi hupenda kuitwa kwa cheo hicho na kuona wametukuzwa kwa kupewa daraja kubwa ukilinganisha na wengine. Hali hii ni vyema ikazingatiwa na isitumike vibaya kwa sababu husababisha matabaka katika jamii, jambo ambalo sio jema kwa maendeleo ya taifa.

#### 4.4.3.1.6 Jazanda ya Neno "Bwana"

Mtunzi wa Tamthiliya ya *Mashetani* ametumia neno *"bwana"* wakati Juma anapomwulizia mama Kitaru kama yupo. Msanii anasema:

*JUMA: Je, bwana yupo?"*

*MAMA: Hata. Utamweza siku hizi. Anafanya kazi usiku na machana!*

*Hana kituo. Yeye na baba yako hajulikani anayempita mweziwe*

*Afadhali baba yako, kazi yake iko nyumbani. Je ulikuwa na shida naye!*

*JUMA: Hapana. Nilitaka kumwamkia tu. (Uk.14)*

Kasumba hii pia inaonekana wakati mhusika Juma na Kitaru wakitumia neno mheshimiwa pamoja na neno la Kiengereza "*chief*" wakimaanisha utukufu na ubora wa daraja kitabaka kuliko wengine. Msanii anasema:

*KITARU: Ah, Mheshimiwa.*

*JUMA: Unasemaje chief? Nasikia unalala tu. Holiday inakupa time kidogo. (uk.14)*

Salem (2013), anasema kuwa, Kitaru na Juma ni zao la tukio hili la kihistoria ndio maana wanaitana *mheshimiwa* na kuchanganya msimbo inayokuja kufutwa na Azimio la Arusha lililohimiza usawa wa watu wote na badala yake watu wakatambulishana kwa neno ndugu.

#### 4.4.3.2 Mbinu ya Kiishara katika Mashetani

Ni kitu kinachofahamika au kuaminika katika jamii inayohusika ambacho hutumika kama alama ya kitu kingine na kueleweka kwa wanajamii wengi (Senkoro, 1982 na2011). Ni neno au usemi wenye maana inayowakilisha dhana nyingine kwa kuhusiana nayo. Yaani neno, au usemi huo huwa na viwango viwili vya maana. Maana ya moja kwa moja na maana ya kitamathali. Katika Tamthiliya ya *Mashetani* mtunzi ametumia ishara kama vile:

**Jedweli Na. 4.2: Ishara katika Tamthiliya ya *Mashetani***

| Na. | Mbinu ya Ishara | Maana ya Ishara |
|---|---|---|
| 1. | Shetani | Ukoloni |
| 2. | Mbuyu | Mandhari ya Afrika |
| 3. | Kicheko | Kejeli za Wakoloni |
| 4. | Kimya | Tafakuri juu ya mapinduzi |
| 5. | Kuzungumka mbuyu | Mivutano kati ya tabaka mbili |

Chanzo: Data kutoka Tamthiliya ya Mashetani, Julai 2017

Katika Tamthiliya ya *Mashetani,* ishara hizo zimetumika kuashiria mambo mbalimbali. Mfano, ishara ya *shetani,* huwakilisha ukoloni mambo leo ambao upo katika jamii baada ya ukoloni mkongwe kuondoka. Jamii za Kiafrika ziliingia katika utawala wa ukoloni mamboleo ambapo anayetawala anakuwa haonekani kama vile ambavyo huwezi kumwona *shetani.* Hivyo *shetani* imetumika kiishara zaidi.

Ishara nyingine ni *mbuyu* ambao unawakilisha eneo ambalo matabaka haya mawili hayawezi kukutana wala tabaka tawaliwa haliwezi kulikamata tabaka tawala. Hivyo ishara ya *kuzunguka mbuyu* ni muundo wa duara ambapo inawakilisha jamii mbili zinazokinzana kiuchumi, kiutawala na kimaendeleo. Wakati jamii moja ikijaribu kuikamata jamii nyingine inakuwa ni kama tendo la kuzunguka mbuyu.

Ishara nyingine ni ishara ya *kicheko* ambayo imetumika kama dhihaka ama kejeli juu ya jamii tawaliwa ambayo inaamini imejitegemea Jamii hiyo inajihisi kuwa tayari imepatauhuru wakati bado ipo chini ya ukoloni mambo leo ambao umekuja kwa sura mpya ya shetani. *Kimya* kwa upande mwingine ni ishara ambayo inaashiria tafakari

ya juu ya mapinduzi ambapo jamii tawaliwa inahitaji kutafakari juu ya mbinu za ukombozi kutoka kwa adui asiyeonekana yaani ukoloni.

#### 4.4.3.3 Mbinu ya Kitaswira katika *Mashetani*

Taswira ni lugha ya picha ya kitu au mahali kwa kutumia ishara (Senkoro 2011). Taswira zinaweza kuwa taswira za hisi, za mawazo au taswira zinazoonekana. Katika utafiti huu iligundulika kuwa msanii wa Tamthiliya ya *Mashetani* ametumia mtindo wa mbinu ya kitaswira katika kujenga maudhui ya kazi yake ya sanaa. Taswira zilizojitokeza katika Tamthiliya ya *Mashetani* ni kama zifuatazo:

*(i)* *Shetani*
*(ii)* *Binadamu*
*(iii)* *Mbuyu*
*(iv)* *Kisu*
*(v)* *Kifo*
*(vi)* *Manyoya*
*(vii)* *Gashalazeritwas*
*(viii)* *Daktari*
*(ix)* *Shereheza Waltz*
*(x)* *Kicheko*

Katika utafiti huu mtafiti alikusanya maneno ya kitaswira yaliyotumika katika Tamthiliya ya *Mashetani.* Baadae mtafiti aliyafanyia uchambuzi maneno hayo kwa mkabala wa kitaswira ili kupata dhima za taswira hizo. Jadweli lifuatalo linafafanua taswira hizo.

**Jedweli Na. 4.3: Matumizi ya Taswira katika *Mashetani***

| Na. | Neno | Maana ya kitaswira |
|---|---|---|
| | Shetani | Ukoloni |
| | Binadamu | Mwafrika |
| | Mbuyu | Mandhari ya kiafrika |
| | Kisu | Uwezo, juhudi au maarifa ambayo Waafrika waliotawaliwa na wakoloni walijipatia na ambayo yaliwawezesha kupigania uhuru wao na kumwondoa mkoloni |
| | Gashalaze ritwas | Kuacha mila na desturi za kiafrika na kushika mila za kizungu. Ni uakisiko wa athari za lugha ya Kijerumani |
| | Daktari | Mbinu ya kuondokana na ubepari |
| | Shereheza Waltz | Maandalizi ya mwafrika kuweza kujitawala mwenyewe |
| | Kicheko | Unafiki |
| | Manyoya | Hali ya kutoka tabaka la chini na kuwa Bwanyenye |

Chanzo: Data kutoka katika Mashetani, Julai 2017

#### 4.4.3.4 Mbinu ya Uteuzi na Matumizi ya Tamathali za Semi katika *Mashetani*

Tamathali za semi ni usemi wa kufananisha kitu dhana tofauti au zinazofanana. Tamathali za semi ni maneno au sentensi ambazo hutumiwa na wasanii wa fasihi ili kutia nguvu katika maana, mtindo na hata sauti katika maandishi ama kusema (Senkoro, 2011). Katika Tamthiliya ya *Mashetani* tamathali za usemi zimejitokeza kama ifuatavyo katika Jadweli nambari 4.4.

**Jedweli Na. 4.4: Tamathali za Semi katika Tamthiliya ya *Mashetani***

| Na. | Tamathali ya semi |
|---|---|
| 1. | Tashibiha |
| 2. | Kejeli |
| 3. | Sitiari |
| 4. | Tashihisi |
| 5. | Takriri |
| 6. | Majazi |
| 7. | Mubalagha |
| 8. | Tanakali sauti |

Chanzo: Data kutoka katika Tamthiliya ya Mashetani, 2017

Jadweli namba 4.4 linaonesha tamathali za semi ambazo zimeonekana kutumika katika Tamthiliya ya *Mashetani* kama inavyoonekana katika jadweli hilo. Tamathali za semi ambazo zimetumika ni tashibiha, sitiari, tashihisi, takriri, taswira, ishara, majazi na mubalagha. Vipengele hivyo vimefanyiwa uchambuzi kama ifuatavyo:

#### 4.4.3.4.1 Tashibiha

Tashibiha ni tamathali ya usemi inayotoa mfano wa vitu unaojengwa kwa maneno kwa kulinganisha vitu viwili au zaidi kwa kutumia vilinganishaji, kama, mithili ya, mfano, na kadhalika (Mulokozi, 2002). Utafiti huu ulichunguza na kubaini tashibiha zinazojitokeza katia Tamthiliya ya *Mashetani*, kipengele hiki kimetumika kama ifuatavyo

(i) *"Kaganda hapo juu ya kiti kama mfalme" (uk.37)*
(ii) *" Unajiweka nyuma kama mkia"(uk 45).*
(iii) *"Pigana kama u mwanaume" (uk 10).*
(iv) *"Huachi Kitaru kunifanya kama kitu" (uk51).*
(v) *"Mambo mengi kama shetani" (uk24).*
(vi) *"Naye daktari ana manyoya kama sisi" (uk 49).*
(vii) *"Linaruka kama ndege"(uk.22)*
(viii) *"Umejipachika hapo viguu juu kama ndege" (uk.36)*
(ix) *"Mdomo kama cherehani"(uk.36)*

Katika mifano hiyo tunaona kuwa msanii amelinganisha dhana moja na dhana nyingine kwa kutumia viunganishi. Kwa mfano, katika tashibiha "*kaganda hapo juu kama mfalme" (uk.37)*, msanii analinganisha tabia ya mfalme kukaa na kuagiza kila kitu kinafanywa na wafuasi wake wakati yeye analetewa taarifa. Mbinu hii ya kisanaa ina dhima ya kuonesha chanzo cha migongano katika jamii ambayo inaonesha utabaka kati ya tabaka la juu na tabaka la chini.

#### 4.4.3.4.2 Tashihisi

Senkoro (1982), anafasili tashihisi kuwa ni tamathali ya usemi ambayo wakati mwingine huitwa tamathali ya binadamu. Kwa tamathali hii vitu visivyo na sifa walizonazo watu hupewa sifa hizo. Mifano ya tashihisi kutoka kwenye Tamthiliya ya *Mashetani* ni:

> *"mimi shetani…Ninajenga. Ninabomoa" (uk.1).*

Kupitia tashihisi hii msanii anaonesha namna shetani (ukoloni) ulivyo na athari katika ulimwengu. Ukoloni umekuwa na nyuso mbili. Uso wa kwanza unaonesha hali ya upendo miongoni mwa nchi changa kwa kutoa misaada kadhaa ambayo haina nia njema ya kuzijenga nchi maskini. Uso wa pili unaonesha namna ukoloni unavyoathiri moja kwa moja nchi za dunia ya tatu kwa kuzivuruga nchi changa kutokana na nguvu za kibabe na sera kandamizi. Mifano mengine ya tashihisi katika Tamthiliya ya *Masheta*ni pale msanii anaposema:

> *"degree" inakupa tonge la wali na mchuzi wa kuku badala ya tonge ya ugali na maharage" (uk. 17).*

Matumizi ya tashihisi hii inadhihirisha wazi dhana ya mamlaka baina watu wa matabaka mawili, yaani tabaka la juu na tabaka la chini. Hali hii hupelekea kuwepo kwa ubaguzi katika jamii, jambo ambalo ni vyema likapigwa vita ili kujenga jamii imara na zenye mafanikio.

#### 4.4.3.4.3 Takriri

Ni mtindo wa usemi ambao msemaji hurudia neno au maneno yaleyale kwa makusudi ya kutia mkazo au kusisitiza jambo. Kahigi na Mulokozi (1979), wanaielezea takriri kuwa ni uradidi, yaani urudiaji wa sauti, neno, kirai, kishazi na hata senetensi katika kazi za kifasihi. Katika tamthiliya ya *Mashetani* data

zinaonesha kuwa msanii ametumia mbinu ya takriri. Baadhi ya takiriri hizo ni kma zifuatazo:

(i) *"Nimemuua, Nimemuua, nimemuua" (uk. 8).*

(ii) *"Hodi, Hodi, Hodi" (uk. 13).*

(iii) *"Karibu, karibu" (uk. 13)*

(iv) *"Ndiyo, ndiyo, ndiyo" (uk31)*

(v) *"Usiogope, usiogope, usiogope" (uk. 2)*

(vi) *"Taabu, taabu, taabu tu" (uk. 41).*

(vii) *"Mtazame, mtazame, Mtazame" (uk. 43).*

(viii) *"Njooni!, njooni!" (uk. 22)*

(ix) *"Ukweli? Ukweli? Ukweli?" (uk. 53).*
*"Sivyo! Sinyo! Sivyo! Hata kidogo" (uk. 3).*

(x) *"Amekufa! Nimemuua! Nimemuua! Nimemuua! au walitaka nimuue"(uk. 8).*

(xi) *"Marhaba marhaba mwanangu" (uk. 13).*

(xii) *"Ndiyo, ndiyo" (uk. 31).*

(xiii) *"Ulikuwa unasema, unasema" (uk. 38).*

Kupitia mwandishi tunaona kuwa msanii ametumia takriri neno ambapo neno moja linarudiwa rudiwa ili kuweka mkazo na msisitizowa yale anayoyazungumza katika kazi yake. Mathalan, katika mfano wa kwanza (i), msanii amerudia rudia neno "nimemuua" ili kuonesha namna muafrika alivyokuwa na harakati za kuondokana na ukoloni. Hata hivyo, anajikuta akiwa haamini iwapo amefanikiwa kuondokana na ukoloni huo.

#### 4.4.3.4.4 Tanakali Sauti

Ni tamathali ya semi inayotoa au kuiga sauti za mlio wa vitu, watu au wanyama (Senkoro, 2011). Data za utafiti huu pia zilionesha kuwa Tamthiliya ya *Mashetani* imetumia tanakali sauti kama moja ya mtindo wa kisanii. Mifano ya tanakali sauti iliyokusanywa na mtafiti ni kama ifuatayo:

(i) *"Shhh…njoo" (uk. 22)*

(ii) *"Ke, ke, ke, ke, ke, ke, Kama cherehani" (uk. 36,)*

(iii) *"kwe, kwe, kwe, kwe" (uk. 38)*

(iv) *"Ayi? Ayi (uk 36) uss! funga mdomo" (uk. 39)*

(v) *"Mama! Ayi! Ayi! Mungu wangu" (uk. 35).*

(vi) *"Gash …Gash …ah" (uk. 4).*

(vii) *"Aah, Aah! Ndiyo! Ndiyo, ndio Aha! Kwani ndiye huyu bwana mwenyewe?" (uk. 3).*

#### 4.4.3.4.5 Mubalagha

Mubalagha ni tamathali ambayo hutia chuku kuhusu uwezo wa viumbe tabia zao na kuhusu sifa zao kwa madhumuni ya kuchekesha na kusisitiza. Kahigi na Mulokozi (1979), wanailezea chuku kuwa ni mbinu ya kisanii ambapo kitu, mtu au jambo hukuzwa zaidi ya uwezo. Mtafiti alibaini kuwa mwandishi wa Tamthiliya ya *Mashetani* ametumia baalagha zifuatazo:

(i) "*Nimeshikwa na kazi mpaka kopeni*"(uk14)
(ii) "*Mtoto kiburi kimempita kimo*" (uk38)

Katika mfano namba moja (i), tunaona msanii akisisitiza wingi wa kazi alizonazo mhusika mama Kitaru. Ambapo anatia chumvi wakati anapoeleza namna alivyobanwa na kazi na kutokuwa na nafasi. Katika mfano namba mbili (ii) mama Kitaru anatia chumvi anapotuelezea jinsi Juma alivyokuwa na kiburi kupita kiasi hata kufikia kumpita kimo.

#### 4.4.3.4.6 Kejeli

Kejeli ni maneno yanayotumika kueleza sifa za mtu kinyume na sifa alizonazo mtu huyo (Senkoro, 1982). Katika Tamthiliya ya *Mashetani* mwandishi ametumia kejeli kama kipengele cha kimtindo kama ifuatavyo:

(i) *Aibu hii. mtoto wa University bwana! (uk15).*

Katika Tamthiliya hiyo, msanii anaonesha kejeli kwa wasomi wa ngazi ya Chuo Kikuu. Mjadala huu unaonesha kuwa elimu ya Kimagharibi ambayo ililetwa na wakoloni haikumuandaa Muafrika kujitambua ipasavyo na kufanya mapinduzi katika nyanja zote za maisha yake. Kwa hali hiyo, elimu ya Kimagharibi ilimuandaa kijana wa Afrika kuendelea kumtegemea mkoloni. Mifano mengine ya kejeli ni kama ifuatayo:

(ii) *Nasikia unajifungiafungia ndani sana, nini tena? (uk 15).*
(iii) *Mpaka ubembelezwe. Ma,hebu mwandikie kadi mheshimiwa umualike aje katika party. Maana hivi hivi hainywi hii soda (uk 15).*

#### 4.4.3.4.7 Sitiari

Sitiari ni tamadhali ya semi inayotumika kuumba picha fulani inayotoa athari fulani au inayoamsha mwitikio fulani kutoka kwa hadhira (Mulokozi, 2002). Katika Tamthiliya ya *Mashetani* kuna matumizi ya Sitiari kama jadwali namba 5hapo chini linavyoonesha.

**Jedweli Na. 4.5: Sitiari na Maana zake katika *Mashetani***

| Na. | Sitiari | Maana ya Sitiari hiyo |
|---|---|---|
| 1. | Binaadamu | Utu wa Mwafrika |
| 2. | Nguvu | Uwezo wa wakoloni kutawala Afrika |
| 3. | Mchezo wa Kuzunguka mbuyu | Mpaka baina ya mtawala na mtawaliwa |
| 4. | Urafiki wa Juma na Kitaru | Kuonesha utabaka |
| 5. | Kisu | Harakati za kujikomboa dhidi ya ukoloni |
| 6. | Mbuyu | Mandhari ya Afrika |
| 7. | Manyoya | Mbinu za Kikoloni |
| 8. | Shetani | Ukoloni mamboleo |

Chanzo: Data kutoka Tamthiliya ya *Mashetani,* Julai 2017

#### 4.4.3.4.8 Majazi

Ni jina lenye kubeba maana ambayo aghalabu huakisi tabia au hali ya mhusika mwenye jina hilo (Senkoro, 1982). Mwandishi wa Tamthiliya ya *Mashetani* ametumia majazi kama vile:

(i) Jina la *Shetani*
(i) Jina la *Binadamu*

Jina la mhusika Shetani limetumika ili kuonesha vitimbi vya wakoloni vikilinganishwa na Shetani kutokana na ubaya wake. Jina hili linachorwa kutokana na tabia ya wakoloni kuwa wanyonyaji, wakandamizaji, wezi wa mali za nchi nyengine pamoja na kuingiza kila aina ya maangamizi. Aidha, jina la Binadamu limetumika ili kuonesha utu wa Mwafrika katika bara hili.

#### 4.4.3.5 Mdokezo

Mtafiti alidondoa data kutoka Tamthiliya ya *Mashetani* na kubaini kuwa msanii wa Tamthiliya ya *Mashetani* ametumia mtindo huu kwa kiwango kikubwa. Mdokezo ni hali ya mtunzi kukatiza maneno au kuacha maneno bila kukitaja kitu au maneno ambayo kwa kawaida ni wazi na huweza kujazwa kwa ubunifu. Mifano ya mdokezo katika Tamthiliya ya *Mashetani* ni:

(i) *"inamaana …haiwezekani…nikiamini hivyo…basi yeye hakufa…" (uk 8)*

(ii) *"Ni kweli – kuwa mimi…hata kidogo… kivuli…? Mimi …" (uk 11)*

(iii) *"kama ndege … vile …ndege" (uk 29)*

(iv) *"Ahsante kama ni hivyo…" ( uk 31)*

(v) *"ugonjwa huu, ninavyofikiri mimi…"(uk. 33 )*

(vi) *"…hata kidogo…kivuli…? Haiwezekani?" (uk. 9)*

Katika Tamthiliya ya *Mashetani* mdokezo umetumika kisanii kwa lengo la kujenga dhamira ya kazi hii. Kwa mfano, msanii anaposema:

*"Ugonjwa huu, ninavyofikiri mimi…"* (uk. 3/3).

Hadhira inaposikia maneno hayo huwa makini kutaka kujua msanii amelenga nini anataka kusema. Mdokezo unatumika pia kama korasi ambayo inamfikirisha msanii na hivyo kumpa nafasi msomaji au msikilizaji kujaza nafasi hiyo kwa fikira zake kutegemea muktadha wa mazungumzo yanayoendelea.Mfano mwengine tunakutana nao pale msanii anaposema:

"*inamaana … haiwezekani… nikiamini hivyo … basi yeye hakufa…" (uk. 8)*

Msanii anamuonesha binadamu (Muafrika) ambaye ana mgogoro na mawazo yake kuhusu kifo cha Shetani (ukoloni) kama kweli kafa ama la. Lengo la Binadamu ni kumuua shetani (Muafrika kuondoa ukoloni). Hali hii inamfanya Binadamu (Muafrika) awe hana uhakika na mapambano yake zidi ya ukoloni, iwapo amefanikiwa kuuondoa au hakufanikiwa.

#### 4.4.3.6 Nidaa

Ni msemo unaoonesha kushangaa au kushangazwa na jambo fulani (Senkoro, 2011). Data za utafiti huu zimeonesha kuwa tamathali hii imetumiwa na msani wa Tamthiliya ya *Mashetani* katika kuisanii kazi yake. Mifano ya matumizi ya nidaa katika Tamthiliya hii ni mingi, baadhi ya mifano hiyo ni kama ifuatayo:

*(i)* *"Doo, doo! Salaale! " (uk. 42)*
*(ii)* *"Gari mpya! Benzi!" (uk. 22)*
*(iii)* *"Umbe! (uk 21)*

(iv) *yangu! Naam! Maliyangu" (uk. 22)*

(v) *"Sielewi! (uk 25)*

(vi) *hadithi!" (uk. 24)*

#### 4.4.3.7 Mchanganyo Ndimi

Data za utafiti huu zinaonesha kuwa wahusika wa Tamthiliya hii kama vile Juma, Kitaru na Baba Kitaru wametumia maneno ya lugha ya Kiengereza wakati wa mazungumzo yao. Baadhi ya maneno yaliyotumika ni kama yafuatayo yakiambatanishwa na maana zake.

**Jedweli Na. 4.6: Mchanganyo Ndimi na Maana Zake**

| Na. | Neno | Maana |
|---|---|---|
| 1. | Chief | Bwana |
| 2. | Holiday | Mapumziko |
| 3. | Time | Wakati |
| 4. | I say | Ninasema |
| 5. | Party | Sherehe |
| 6. | Outline of African History | Muongozo wa historia ya Afrika |
| 7. | University | Chuo Kikuu |
| 8. | You must read it | Lazima ukisome |

Data kutoka Tamthiliya ya *Mashetani*, Julai 2017

Mwandishi ametumia lugha ya Kiengereza ili kuonesha wahusika wanatokana na tabaka la wasomi waliopata elimu ya kikoloni. Mifano mingine ya uchanganyaji wa lugha ni:

(i) *Unasemaje chief. Nimekusikia unalala tu, Holiday inakupa time kidogo (uk. 15).*

(ii) *What nonsense. Mwambie Mfaume aweke chakula mezani. Mtu anaumwa kichwa that's very normal (uk 27).*

(iii) *Aam …. Yes…can you fetch one beer and one whisky? Whisky! Double or single? No one beer for him and one whisky for me. Ndiyo bwana; hiyo whisky iwe double au single? (uk 40).*

#### 4.4.3.8 Mbinu Nyingine za Kimtindo katika *Mashetani*

Utafiti huu ulifanyika ili kubaini mbinu zingine za kimtindo ambazo zilizotumika katika kuisanii Tamthiliya ya *Mashetani*. Data za utafiti huu zimeonesha kwambaTamthiliyaya *Mashetani* imetumia mbinu nyengine za kimtindo kama zinavyojidhihirisha katika Jadwali Namba 4.7.

**Jedweli Na. 4.7: Mbinu Nyengine za Kimtindo katika *Mashetani***

| | |
|---|---|
| 1 | Mtindo wa Mandhari ya Fasihi Simulizi |
| 2 | Mtindo wa Kishairi |
| 3 | Mtindo wa Usimulizi |
| 4 | Mtindo wa Majigambo |
| 5 | Mtindo wa Matumizi ya Nafsi |
| 6 | Mtindo wa Matumizi ya wahusika wa fasihi simulizi |
| 7 | Mtindo wa Tamthiliya za Majaribio |
| 8 | Mtindo wa Dayalojia |

Chanzo: Data kutoka Tamthiliya ya *Mashetani,* Julai 2017

Data za utafiti zilizokusanywa kutoka katika Tamthiliya ya *Mashetani* zimeonesha kwamba Tamthiliya hiyo imetumia mbinu za kimtindo kama vile mtindo wa fasihi simulizi, mbinu ya kishairi, mtindo wa kishairi, mtindo wa usimulizi, mtindo wa majigambo, mtindo wa wahusika wa fasihi simulizi na mtindo wa matumizi ya nafsi**.** Mitindo hii imefafanuliwa kama ifuatavyo:

#### 4.4.3.8.1 Mandhari za Fasihi Simulizi

Haya ni mazingira ya kifasihi ambayo hutumika katika kujenga masimulizi ya riwaya, Tamthiliya na ushairi au hadithi fupi (Senkoro, 1982, Wamitila, 2010). Data zilizokusanywa kutoka Tamthiliya ya *Mashetani* zimeonesha kuwa msanii ametumia mandhari ya bara la Afrika kutokana na kutumia mbuyu ambao ni miongoni mwa vikale vya bara hili hasa katika upwa wa Afrika Mashariki. Kutokana na tukio la Kitaru kuumwa kichwa baada ya kushiriki mchezo uliochezwa baina yake na JumaMbuyu unaelezwa na jamii inayopenda maovu na kuyaficha kwa kisingizio kuwa shetani anawachukia. Leo mti huu badala ya kuwa sehemu ya kutatulia matatizo, pango lililopo katika mbuyu linakuwa sehemu inayotisha. Salem (2013) anasemaa:

> *Kwenye miti mikubwa hususani mbuyu ni sehemu ambayo Mashetani na mizimu huishi. Hivyo uteuzi wa mbuyuni kuwa ni mandhari ya /ambapo mchezo wa shetani na binadamu ulifanyika ni wa makusudi na msanii amejenga uhalisia wa tamaduni kuhusu imani na mielekeo ya jamii kuhusu uwepo wa viumbe hivi dhahania vilivyopo kwa jamii juu ya uwepo,* (Salem, 2013).

Kutokana na data hiyo tunaona kuwa msanii ametumia mtindo wa mandhari ya fasihi simulizi ndani ya fasihi andishi. Hii ni kutokana na kwamba mandhari kama hizi za mibuyu tunakutana nazo katika ngano za fasihi simulizi za Uswahilini.

#### 4.4.3.8.2 Mtindo wa Kishairi

Data za utafiti huu zinaonesha kuwa Tamthiliya ya *Mashetani* imetumia mtindo wa ushairi katika kuipamba kazi yake na kuwasilisha dhamira. Kwa mfano, msanii anamtumia mhusika binadamu akitamba ushairi kama ifuatavyo:

*BINADAMU:* *Wako wapi walio wakijitapa?*
*Sasa twawataka.*
*Wako wapi walio wakijitapa?*
*Sasa twawataka.*
*Tumekwisha (anacheka) wakamata.*
*Wakamata.*
*Tumekwisha wabwatabwata.*
*Wako wapi waliokuwa juu jana?*
*Sasa twawataka.*
*Wako wapi waliokuwa juu jana?*
*Sasa twawataka.*
*Tumekwisha waangusha*
*Waangusha.*
*Tumekwisha wasagasaga.*
*Tumekwishawakamata*
*Wakamata.*
*Tumekwisha wabwatabwata.*
*Tumekwisha waangusha*
*Waangusha.*
*Tumekwisha wasagasaga. (uk. 42)*

Shairi hili linatumika ili kuonesha namna Muafrika alivyokuwa na mawazo ya kudhani kwamba amefanikiwa kuondoa ukoloni mara baada ya kupambana na kufanikiwa kuondoa ukoloni mkongwe katika bara la Afrika. Ni matumaini ya wananchi wa bara hili kwamba katika wakati huu wa uhuru wangeishi bila kuathiriwa na mabeberu wa kikoloni. Hata hivyo, kwakweli imekuwa hali hiyo sivyo kutokana na ukoloni mamboleo na utandawazi kuendelea kukandamiza bara hili.

**4.4.3.8.3 Mtindo wa Nyimbo**

Wimbo ni kila kinachoimbwa (Mulokozi, 1996). Data za utafiti huu zinaonesha kuwa Tamthiliya ya *Mashetani* imetumia mtindo wa wimbo. Kwa mfano, msanii anamtumia mhusika Baba Kitaru kuimba wimbo wa kufurahia maisha ya kifahari kama ifuatavyo:

*Baba Kitaru:*

*"Papa pa pa pa pa*
*Ilike some money.*
*Papa pa pa pa pa*
*Ilike some honey*
*Papa pa pa pa pa*
*Avery good life*
*Papa pa pa pa pa*
*Avery beautiful wife*
*Papa pa pa pa pa*
*Avery goodwife*
*Papa pa pa pa pa*
*A very good life" (uk.22)*

Mtafiti amebaini, baadhi ya watu mfano, Baba Kitaru ambao wanawakilisha tabaka la juu baada ya nchi za Afrika kupata uhuru wa bendera kutoka kwa wakoloni wanavyofurahia maisha ya kifahari huku tabaka tawaliwa likiwa katika hali ngumu ya maisha.

**4.4.3.8.4 Mtindo wa Masimulizi**

Usimulizi ni namna mtunzi anavyotoa visa vyake kupitia kwa wahusika ambao anawapa lugha, matendo na kuwavisha uhalisia (Mutembei, 2010). Msanii anatumia mtindo wa masimulizi wakati anaposimulia hadithi ya chewa ambaye ana uwezo usio wa kawaida. Msanii anasema:

> *"Mbali sana, ukivuka bahari saba, kuna chewa mkubwa, chewa huyu akivuta pumzi maji yote yanakupwa, maji yote yanaingia kinywani mwake anaweza kutoka huko aliko kuivuta na kuimeza mashua yoyote anayoitaka mashua inavutwa tu na mkondo wa maji ikitaka isitake. Na huyu chewa siyo chewa bali shetani"* (uk 28)

Mtafiti amebaini kuwa, msaniiametumia mtindo wa masimulizi kuwapa wahusika nafasi ya kuzungumza na kusimulia juu ya visa ambavyo kwa ujumla wake vinajenga kazi ya fasihi. Katika kisa hiki msanii anaonesha namna wakoloni

wanavyotumia mbinu za kuzilazimisha nchi changa na kuzipangia wanavyotaka wao ikiwamo kuzikandamiza na kuzipangia masharti wanayoyataka wao kwa manufaa ya nchi za kibepari.

#### 4.4.3.8.5 Mtindo wa Matumizi ya Nafsi

Data katika Tamthiliya ya *Mashetani* zinaonesha kuwa msanii ametumia nafsi zote tatu. Mifano ya matumizi haya ya nafsi yanajidhihirisha kama ifuatavyo:

#### 4.4.3.8.6 Matumizi ya Nafsi ya Kwanza

Msanii ametumia nafsi ya kwanza kwa kiwango kikubwa. Kwa mfano, mtindo wa matumizi ya nafsi ya kwanza tunauona kupitia mhusika Shetani anaposema:

*"Mimi shetani*
*Sio jini wala kuhani*
*Ninajenga*
*Ninabomoa*
*Ninatukuza*
*Ninadhalilisha nitakavyo" (uk. 1)*

Msanii anaonesha namna ukoloni ulivyo ulimwenguni leo hii. Msanii anaeleza kwamba wakoloni wamekuwa wakiamua vile namna wanavyotaka kuuendesha ulimwengu kwa kupitia sera zao za kikoloni. Kwa mantiki hiyo, sera zao ndizo zinazojenga na wakati huo huo zinabomoa. Mifano mengine ya matumizi ya nafsi I ni kama ifuatayo:

(i) *Mimi ni nguvu (uk 1)*
(ii) *Sijali* (uk1)

Mwandishi anaonesha namna matumizi ya nafsi yalivyojitokeza katika Tamthiliya ya *Mashetani.* Kwa kiasi kikubwa nafsi ya kwanza katika mifano hiyo inaonesha jinsi ambavyo wakoloni wanajiona wananguvu na kujitukuza dhidi ya Waafrika.

#### 4.4.3.8.7 Matumizi ya Nafsi ya Pili

Mtunzi wa Tamthiliya ya *Mashetani* vile vile ametumia nafsi ya pili katika kazi hii. Kwa mfano, matumizi ya nafsi ya II tunayaona wakati mhusika Shetani akizungumza na Binadamu katika mchezo kati ya Binadamu na Shetani. Kwa mfano:

"Unaninyenyekea" (uk. 2)

Kwa kurejelea Tamthiliya hii, mtafiti amebaini kuwa mhusika Shetani akimuuliza Binadamu. Mtafiti anaona kuwa nchi za kibeberu zimekuwa zikijikweza na kujiona wabora dhidi ya nchi changa na hivyo nchi changa kuangukia miguuni kwa nchi hizo huku zikitekeleza sera za kikoloni. Mifano mengine ya matumizi ya nafsi ya II ni kama ifuatayo:

*(i) "Unanicha" (uk. 2)*
*(ii) "Unanitukuza" (uk. 3)*
*(iii) "Unanipa heshima" (uk.*
*(iv) "Sema" (uk. 4)*
*(v) "Uko wapi" (uk. 5)*
*(vi) "Ukiniambia" (uk. 5)*
*(vii) "Huoni" (uk 5)*
*(viii) "Unajua kama" (uk. 6)*
*(ix) "Jiulize mwenyewe" (uk. 20)*

#### 4.4.3.8.8 Matumizi ya Nafsiya Tatu

Data za utafiti zilionesha kuwa kuna matumizi ya nafsi ya tatu katika Tamthiliya ya *Mashetani*. Mifano ya matumizi ya nafsi ya tatu ni kama ifuatayo:

*(i) Wakitupenda (uk. 38)*
*(ii) Wanakuja (uk. 40)*
*(iii) Wanaacha (uk. 40)*

#### 4.4.3.8.9 Mtindo wa Matumizi ya Dayalojia

Vile vile data za utafiti huu zilizokusanywa zimeonesha kuwa mwandishi ametumia mtindo wa daiolojia katika Tamthiliya ya *Mashetani*. Mtindo huu umejitokeza kwa kiwango kikubwa. Mfano, majibizano kati ya Juma na Mama Kitaru kama ifuatavyo:

Juma: *Shikamoo*
Mama: *Marahaba – Marahaba, Mwanangu, pita unasita nini? Habari za nyumbani?*
Juma: *Hata sisiti. (uk 45)*

#### 4.4.3.8.10 Mtindo wa Majigambo

Utafii huu uligundua kuwa mtunzi wa Tamthiliya ya *Mashetani* ametumia mtindo wa majigambo. Mtindo huu unatumiwa kwa kiasi kikubwa na mhusika Shetani wakati wa mchezo na Binadamu. Kwa mfano:

*SHETANI: Unanijua mimi nani?*
*Mimi shetani.*
*Siyo jini wala kuhani.*
*Mimi shetani.*
*Uwezo wangu hauhifadhiki.*
*Wema wangu hauhisabiki.*
*Ubaya wangu hausemeki.*
*Ninajenga.*
*Ninabomoa.*
*Ninatukuza.*
*Ninadhalilisha nitakavyo.*
*Mimi ni nguvu na nguvu ni mimi.*
*Mimi ni uwezo na uwezo ni mimi.*
*Tazama miujiza. (Anajibadilisha). Sasa mimi nani? (uk.1)*

Majigambo hayo yanaonesha namna utawala wa kikoloni unavyojiona kuwa bora na kujifanya kuwa na uwezo wa kila kitu dhidi ya mataifa maskini ulimwenguni. Maelezo ya Shetani yanadhihirisha kuwa wakoloni wameyatawala mataifa machanga na wanayaendesha vile wanavyotaka wao kwa kutumia ukoloni mamboleo. Matokeo

yake ni kwamba mataifa machanga yapo kutekeleza sera za makoloni hayo nchini mwao.

#### 4.4.3.8.11 Mtindo wa Tamthiliya ya Majaribio

Katika utafiti huu mtafiti alichunguza mbinu za kimtindo ambazo zimetumika kutunga Tamthiliya ya *Mashetani*. Salem (2013), anamnukuu (Mulokozi, 1994), akieleza kuwa Tamthiliya za mwanzo za Kiswahili zilijikita katika misingi ya Kiaristotle na kufikia miaka ya 1980 kulitokea mapinduzi na mabadiliko ya utunzi wa Tamthiliya za Kiswahili. Ni katika wakati huu ambapo watunzi wa kazi za fasihi za Kiswahili waliona kuna umuhimu wa kutumia fasihi simulizi ya Kiafrika katika utunzi wa Tamthiliya za Kiswahili. Hivyo basi, Tamthiliya hizi ziliitwa Tamthiliya za majaribio kwa sababu zilikuwa na lengo la kufanya majaribio ya kukiuka misingi ya Kiaristotle na kuingiza vipengele vya fasihi simulizi vya Kiafrika katika utunzi wa Tamthiliya ili kuzipa uhalisia Tamthiliya za Kiswahili kulingana na fasihi simulizi ya Kiafrika.

Hivyo basi, data zilizokusanywa kutoka Tamthiliya ya *Mashetani* zilibainisha kuwa Tamthiliya hii ni ya kimajaribio. Mathalani, tunaona kuna matumizi ya ngano, ambapo tunasimuliwa hadithi ya chewa katika kutoa taswira ya ukoloni mamboleo ambao unafananishwa na chewa ambaye anauwezo na nguvu za ziada za kuivuta mashua (nchi za dunia ya tatu). Hali hii ni sawa na ukoloni mamboleo ambapo mataifa tajiriyamekuwa yakiziendesha nchi maskini vile wanavyotaka wao kwa manufaa yao binafsi. Hadithi hiyo inasema:

> *"Mbali sana, ukivuka bahari saba, kuna chewa mkubwa, chewa huyu akivuta pumzi maji yote yanakupwa, maji yote yanaingia kinywani mwake anaweza kutoka huko aliko kuivuta na kuimeza*

> *mashua yoyote anayoitaka mashua inavutwa tu na mkondo wa maji ikitaka isitake. Na huyu chewa siyo chewa bali shetani"* (uk 28).

Pia, mwandishi wa Tamthiliya hii ametumia wahusika ambao hutumiwa na fasihi simulizi mfano mwandishi amemtumia shetani kama mhusika. Kwa kawaida fasihi andishi hutumia wahusika watu, lakini mwandishi anapotumia viumbe wengine ambao si watu ana kuwa anatengeneza kazi yake kuwa fasihi ya majaribio.

Vile vile msanii ametumia mandhari tunazokutana nazo katika fasihi Simulizi za Kiafrika. Mwandishi anawatumia wahusika Juma na Kitaru ambao wanaigiza mchezo kwenye mbuyu. Ambapo wahusika hao wanabadilisha majina ya uhusika wao. Mmoja anakuwa Shetani na mwengine Binadamu. Msanii ametumia mandhari ya kwenye mbuyu ili kuonesha uhalisia wa ujumi wa Mwafrika. Kwa mfano:

Juma: *"Wananchi kwa mara nyingine chini ya mbuyu huu mimi Juma na rafiki yangu Kitaru tunakuonyesheni mchezo wa Shetani na Binadamu. Mimi nitakuwasheani na Kitaru atakuwa Binadamu( uk1)*"

Kwa hakika mitindo iliyojitokeza katika tamthiliya ya *Mashetani* imezidisha thamani ya kuweza kufanikisha vyema upande mmoja ya lengo mahsusi la kwanza na swali la kwanza la utafiti huu. Hivyo basi uchambuzi unaoendelea ni upande wa pili wa tamthiliya ya *Mashetani Wamerudi* kwa kuzingatia lengo mahsusi la kwanza na swali la kwanza la utafiti huu.

## 4.5 Mtindo Katika *Mashetani Wamerudi*

Katika utafiti huu, mtafiti alichunguza ni jinsi gani mtunzi wa Tamthiliya ya *Mashetani Wamerudi* ametumia mbinu za kimtindo katika ujenzi wa kazi yake. Sifa

za kimtindo ambazo zilifanyiwa uchunguzi na mtafiti katika Tamthiliya ya *Mashetani Wamerudi* ni kama zifuatavyo:

(i) Uteuzi wa msamiati

(ii) Miundo na mpangilio wa sentensi

(iii) Uteuzi wa tamathali za semi

(iv) Usimulizi

(v) Matumizi ya Mashairi

(vi) Matumizi ya tanzu za fasihi Simulizi ndani ya fasihi andishi

(vii) Matumizi ya vipengele vya fasihi simulizi ndani ya fasihi andishi

(viii) Matumizi ya nafsi

Kwa kuzingatia sifa hizo za kimtindo, sifa hizi zinajadiliwa kama zilivyojidhihirisha katika Tamthiliya ya *Mashetani Wamerudi* kama ifuatavyo:

### 4.5.1 Uteuzi wa Msamiati

Data za utafiti huu zinaonesha kuwa mwandishi wa Tamthiliya ya *Mashetani Wamerudi* ameteua misamiati ambayo inasawiri ujumbe alioukusudia. *Mashetani Wamerudi* ni miongoni mwa Tamthiliya zinazohakiki aina ya maisha ya jamii za Kiafrika baada ya kupatikana kwa uhuru wa bendera. Aidha, Tamthiliya hii inayashughulikia mahusiano ya wakoloni na makoloni yao wakati wa ukoloni mkongwe na baada kupatikana kwa uhuru wa bendera kulikofuatiwa na uibukaji wa ukoloni mamboleo.

Katika Tamthiliya ya *Mashetani Wamerudi* misamiati imeteuliwa kulingana na lengo nadhamira za mtunzi hasa katika kusawiri ukoloni mamboleo katika nchi changa.

Kwa mfano, matumizi ya msamiati *shetani, mbuyu, jogoo*, *simba, punda*, *bata mzinga,kuku, chozi, tembonawaltz* yametumika kijazanda kusawiri uhusiano uliopo kati ya nchi zilizowahi kutawaliwa na ukoloni na wakoloni. Kwa mfano, neno "shetani" limetumika kuashiria ukoloni mamboleo katika nchi za dunia ya tatu kama vile Tanzania.

Tunaporejelea nadharia ya Mwingilianomatini ambayo ni moja ya nadharia inayoongoza utafiti huu tunagundua kuwa kuna muingilianomatini kati ya Tamthiliya ya *Mashetani* na *Mashetani Wamerudi* katika matumizi ya misamiati. Mathalani, neno shetani katika Tamthiliya zote teule limetumika kuashiria ukoloni mamboleo katika nchi changa.

### 4.5.2 Matumizi ya Lugha katika Mashetani *Wamerudi*

Data zilizokusanywa na mtafiti kutoka katika Tamthiliya ya *Mashetani Wamerudi* zilionesha kuwa Tamthiliya hii imetumia vipengele anuai vya matumizi ya lugha kama mbinu ya kimtindo. Viengele hivyo vilifanyiwa uchambuzi na kuwasilishwa kama ifuatavyo:

**Jedweli Na. 4.8: Matumizi ya Lugha katika *Mashetani Wamerudi***

| Na. | Kipengele cha Lugha |
|---|---|
| 1. | Jazanda |
| 2. | Ishara |
| 3. | Taswira |
| 4. | Tamathali za semi |
| 5. | Misemo |
| 6. | Nahau |
| 7. | Methali |
| 8. | Mdokezo |
| 9. | Mchanganyo ndimi |

Chanzo: Data za utafiti, Tamthiliya ya *Mashetani Wamerudi*, 2017

Jadwali namba 8 hapo juu linaonesha vipengele vya lugha ambavyo vimetumika katika Tamthiliya ya *Mashetani Wamerudi* kama inavyojionesha. Miongoni mwa vipengele vilivyoainishwani; jazanda, tamathali za semi, ishara, taswira, misemo, methali, nahau, mdokezo na mchanganyondimi. Vipengele hivi vimefanyiwa uchambuzi kama ifuatavyo:

#### 4.5.2.1 Matumizi ya Jazanda katika *Mashetani Wamerudi*

Katika Tamthiliya hii msanii ametumia jazanda kadhaa ambazo zimebeba ujumbe wa mwandishi. Baadhi ya jazanda hizo ni kama zifuatazo:

##### 4.5.2.1.1 Jazanda ya Jogoo

Jazanda ya jogoo imetumika katika Tamthiliya ya *Mashetani Wamerudi* ili kuonesha ukoloni na namna unavyofanya vitimbi katika kunyonya bara hili la Afrika.

##### 4.5.2.1.2 Jazanda ya Mbuyu

Mbuyu kama jazanda limetumika katika Tamthiliya ya *Mashetani Wamerudi* kuwakilisha mandhari ya bara la Afrika na namna eneo hilo lilivyoathiriwa. Ambapo Waafrika waliotawaliwa na wakoloni walijikuta wakipambana na wasaliti wa Waafrika wengine.

##### 4.5.2.1.3 Jazan/da ya Neno Waltz

Jazanda ya neno *waltz* inaashiria athari za kikoloni katika bara la Afrika. Kwa uteuzi wa neno hili msanii anatuonesha kuwa katika jamii zetu tunaamini kuwa tu huru wakati ambao bado tunatekeleza mipango ya watawala wetu wa kikoloni wa zamani kupitia sera za kikoloni kwa utekelezaji wa mipango ya maendeleo kama inavyoelekezwa na nchi za kibeberu.

#### 4.5.2.1.4 Jazanda ya Neno Shetani

Mtunzi wa Tamthiliya ya *Mashetani Wamerudi* anatumia neno *shetani* katika Tamthiliya hiyo ili kusawiri ukoloni mamboleo katika bara hili la Afrika. Jazanda ya shetani inaonesha namna ukoloni unavyobadili mbinu mbali mbali katika kuhakikisha unahodhi na kuendeleza sera za kikoloni katika bara la Afrika. Kubadilika badilika kwa shetani kunaashiria namna ukoloni unavyotumia mbinu kama vile za ubinafsishaji, uwekezaji na utoaji mikopo kama ni mwevuli wa kuendeleza ukoloni mamboleo katika bara hili.

### 4.5.2.2 Matumizi ya Kiishara katika *Mashetani Wamerudi*

Jilala (2016), anamnukuu Senkoro (1982), akieleza kuwa ishara ni neno au usemi wenye maana inayowasilisha dhana nyengine kwa kuhusiana nayo. Yaani, neno au usemi huo huwa na viwango viwili vya maana. Katika fasihi, dhana ya ishara inatumika kuelezea kitu fulani ambacho huwakilisha kitu chengine.

Katika Tamthiliya ya *Mashetani Wamerudi* mtunzi ametumia ishara kama ifuatavyo:

(i) Unamuogopa nani? Shetani? (uk. 3)

(ii) Jogoo anaendelea kupaparika na kupiga mashuzi (uk. 10)

(iii) Ugonjwa wa kizunguzungu (uk.20)

(iv) Usisahau kwamba sasa haukubaliki ushetani Kinachokubalika ni ubinadamu wetu sisi na nyinyi. (uk.71)

(v) Mwangaza wa tochi unazidi kuenea kusadiki kwamba kumepambazuka japo kidogo. (uk.32)

(vi) Wale walioomba wachomwe visu pasi na kufa (uk. 11)

Ishara zilizotumika katika mifano ya hapo juu zinabeba maana kama jadwali namba 9 hapo chini linavoonesha.

**Jedweli Na. 4.9: Ishara na Maana zake katika Mashetani Wamerudi**

| Na. | Ishara | Maana |
|---|---|---|
| 1. | Shetani (uk. 3) | Ukoloni mamboleo |
| 2. | Jogoo (uk.10) | Utandawazi |
| 3. | Mashuzi (uk. 10) | Athari za ukoloni |
| 4. | Ugonjwa wa kizunguzungu (uk.20) | Matatizo yanayotokana na ukoloni |
| 5. | Ubinaadamu (uk. 71) | Utu |
| 6. | Tochi (uk. 32) | Muamko |
| 7. | Visu | Ukombozi |
| 8. | Chozi (uk. 20) | Nchi maskini |
| 9. | Tembo (uk. 20) | Nchi tajiri |

Chanzo: Data kutoka Tamthiliya ya Mashetani Wamerudi, Julai, 2017

### 4.5.2.3 Taswira katika *Mashetani Wamerudi*

Taswira ni lugha ya picha ya kitu au mahali kwa kutumia ishara (Senkoro, 2011). Katika utafiti huu iligundulika kuwa msanii wa Tamthiliya ya *Mashetani Wamerudi* ametumia mtindo wa mbinu ya kitaswira katika kujenga dhamira kama ifuatavyo:

*(i)* *"Shina la mbuyu, ka shina la mbuyu-walilibadilisha jiti kubwa lenye virutubishi."*

*(ii)* *"Wakalifanya tanda la kulalia na kisha pahala pa kurukia katika maendeleo yao" (uk. 7).*

*(iii)* *"Wale waliocheza na kufundisha wananchi dansi ya waltz" ( uk11).*

*(iv)* *"Nyuma ya kibanda shetani alijigeuza kuku, au bata mzinga ananifukuza mimi" (uk. 29).*

*(v)* *"(Nyuma ya kibanda. Kijana anamfukuza jogoo. Jogoo anapaparika. Kokoro,*

*(vi)* *kokoro, kokoro-jogoo anakokoreka" (uk. 2).*

*(vii)* *"Labda shetani amekufunga hapo kitandani" (uk. 47).*

*(viii)* *"Kumbe unaweza kukata minyororo ya kuketi na koleo ya kinywa?" (uk. 51).*

*(ix)* *"Simba alingojea kwa hamu na alipofika huko simba na kumvamia punda kwa nguvuna kukata vipande mbali mbali na kumla" (uk 56).*

*(x)* *"Katika karne hii hatuwezi kuwa kinyesi cha mbuzi kinachotawanyika" (uk. 62).*

*(xi)* *"Tunataka tuwe sangara kwenye mlolongo wa pamoja" (uk 62)*

*(xii) "Ninasimamia mwega kwani wewe huoni?" (uk. 70).*

**Jedweli Na. 4.10: Taswira na Maana zake katika *Mashetani Wamerudi***

| Na. | Taswira | Maana |
|---|---|---|
| 1 | Shina la Mbuyu (uk.2) | Bara la Afrika |
| 2 | Dansi ya waltz (uk. 11) | Utamaduni wa Kimagharibi |
| 3 | Kibanda (uk.29) | Mandhari ya bara la Afrika |
| 4 | Shetani (uk. 47) | Ukoloni mamboleo |
| 5 | Kuku (uk. 29) | Sera kikoloni |
| 6 | Bata mzinga (uk. 29) | Sera za kikoloni |
| 7 | Jogoo (uk. 12) | Mkoloni |
| 8 | Kukata minyororo (uk. 51) | Kupambana na ukoloni |
| 9 | Koleo ya Kinywa (uk. 51) | Ukandamizaji |
| 10 | Simba (uk. 56) | Tabaka lenye nguvu |
| 11 | Kinyesi cha mbuzi (uk. 62) | Utabaka |
| 12 | Sangara kwenye mlolongo (62) | Umoja na mshikamano |
| 13 | Mwega (uk.70) | Utegemezi |
| 14 | Punda (uk.29) | Tabaka tawaliwa |

Chanzo: Data kutoka *Mashetani Wamerudi* Jualai, 2017///

### 4.5.2.4 Misemo katika *Mashetani Wamerudi*

Dhana yamisemo inarejelea kifungu kifupi cha maneno kinachofumbata maana kimafumbo ambayo imekusudiwa kutoa funzo kwa jamii. Ni maneno yanayotumika mara kwa mara kama yalivyo katika mazingira maalumu kuleta maana maalum (Wamitila, 2003). Data za utafiti huu zinaonesha kuwa Tamthiliya ya *Mashetani Wamerudi* imetumia misemo. Baadhi ya misemo iliyotumika ni kama ifuatayo:

*"Mguu na njia" (uk:31)*

Katika msemo huu msanii amekusudia kuonesha dhiki, shida wananazokumbana nazo wananchi wa tabaka la chini katika kupambana na maisha ya kila siku. Msanii analishadidia hili kwa kutueleza kwamba baadhi ya watu katika jamii wako katika hali mbaya ya kimaisha na umasikini uliokithiri. Pia, watu wa tabaka la chini

wanaonekana kuhangaika hapa na pale katika kufanya kazi ili kupata mahitaji ya lazima. Hata hivyo, wengi wanaonekana kuwa na hali ngumu ya maisha na kuendelea kuishi maisha ya kubahatisha. Mfano mwengine wa msemo ambao umetumika katika Tamthiliya ya *Mashetani Wamerudi* ni ule unaosema:

*"Si hayo hayo maji ya futi na nyayo? (uk. 12).*

Mwandishi ameitumia hali hii kuonesha kuwa bado hali haijabadilika katika nchi changa. Pamoja na nchi hizi kupata uhuru wa bendera zimekabiliwa na hali ngumu ya maisha kama ile iliyokuwapo wakati wa ukoloni mkongwe. Misemo mingine iliyotumika katika Tamthiliya ya *Mashetani Wamerudi* ni kama ifuatayo:

*(i) "Mafuriko ya maji huanza kuporomoka matone matone" (uk. 24).*
*(ii) "Ya jana si ya leo" (uk.24).*
*(iii) "Bora wachache wenye uthabiti kuliko wengi weye unafiki" ( uk24).*
*(iv) "Tutakutana mwambani" ( uk. 61).*
*(v) "Kukutishia nyamarero" (uk. 67)*

**4.5.2.5 Methali katika *Mashetani Wamerudi***

Methali ni semi fupi fupi zinazobeba uzoefu wa jamii kuhusu maisha na hivyo kuadilisha na kuhekimisha jamii. Methali huitajirisha fani na maudhui ya kazi ya fasihi na hutumika kama daraja la kupitishia maadili kwa jamii husika (Senkoro 1982 na 2011). Data za utafiti huu zinaonesha kuwa kuna matumizi ya methali katika *Mashetani Wamerudi*. Matumizi ya methali yanajidhihirisha kama ifuatavyo:

*"Mpanda ngazi hushuka"( uk. 43)*

Mtafiti amebaini mgogoro uliopo kati ya wale waliokuwa wameshikilia madaraka ya uongozi kabla ya mapinduzi ya Zanzibar. Msanii anaonesha maisha ya Mzee Jumai yalivyoporomoka baada ya kutaifishwa kwa mali zao zote ambapo yeye

mwenyewe anayathibitisha hayo kwa kusema kwamba familiya yao yote haikushuka ngazini bali imeporomoka.

Aidha, katika methali hii msanii anaonesha kwamba baada ya mapinduzi ya Zanzibar familia za wale waliokuwa wameshikilia madaraka ziliporomoka baada ya kutaifishiwa mashamba yao. Hivyo, badala ya kuwa na hali nzuri kimaisha, ikawa sasa wana hali mbaya ya maisha. Mifanomingine ya methali ni kama ifuatavyo:

> *"Mpanda ngazi na mshuka ngazi hawawezi kushikana mikono" (uk. 62)*
>
> *"Hakuna kilichokizuri kisichokuwa na doa" ( uk25)*

Nadharia ya Mwingilianomatini inaelezwa na Jilala (2016), kuwa ni dhana inayorejelea uhusiano wowote unaoweza kuonekana katika matini moja na nyengine au matini zaidi ya moja. Uhusiano huu unaweza kujitokeza katika kipengele kimoja au vipengele mbali mbali, fani, maudhui au hata vyote kwa pamoja.

#### 4.5.2.6 Nahau katika *Mashetani Wamerudi*

Nahau ni semi inayohusu kupunguza ukali wa maneno. Nahau hutumika kuipamba lugha ya fasihi. Pia hutumiwa na wasanii ili kuweza kutajirisha maelezo yao (Greyson na wenzake, 2010). Data zilizokusanywa na mtafiti zinaonesha kuwaTamthiliya ya *Mashetani Wamerudi* imetumia nahau ingawa kwa kiwango kidogo tu. Kwa mfano, kuna nahau inayosema:

*"Anamkata kauli kijana" (uk. 13)*

Katika nahau hii msanii anaonekana kumtumia mhusika Prof. ambaye alimkatisha kijana1 maneno yake na kumueleza athari za ukoloni mamboleo kwa kusababisha

matatizo kwa vijana ambao ndio tegemeo la taifa la kesho. Nahau nyengine iliyotumika katika Tamthiliya ya *Mashetani Wamerudi* ni ile inayosema:

*"Hazifui dafu" (uk. 24)*

Katika nahau ya hapo juu inaonesha kwamba mbinu wanazotumia wakoloni katika mataifa machanga kwa nia ya kunyonya nakukandamiza mataifa hayozimeanza kutambulika. Kwa hali hiyo hazina nafasi miongoni mwa kizazi ambacho kimeamka dhidi ya ukoloni mamboleo. Wafrika leo hii wako macho dhidi ya mbinu za kikoloni kwani tayari vyombo vyao vya habari tayari vimeshaelimisha jamii ya kiafrika.

#### 4.5.2.7 Uteuzi na Matumizi ya Tamathali za Semi katika *Mashetani Wamerudi*

Tamathali za semi ni usemi wa kufananisha kitu au dhana tofauti au zinazofanana. Tamathali za semi ni maneno au sentensi ambazo hutumiwa na wasanii wa fasihi ili kutia nguvu katika maana, mtindo na hata sauti katika maandihsi ama kusema (Senkoro, 2011). Katika Tamthiliya ya*Mashetani Wamerudi* tamatahli za usemi zimejitokeza kama ifuatavyo katika jadwali la hapa chini:

**Jedweli Na. 4.11: Tamathali za Semi katika *Mashetani Wamerudi***

| Na. | Tamathali ya semi |
|---|---|
| 1. | Tashibiha |
| 2. | Sitiari |
| 3. | Tashihisi |
| 4. | Takriri |
| 6. | Ishara |
| 7. | Mubalagha |
| 8. | Tanakali sauti |
| 9. | Kwelikinzani |
| 10. | Mjalizo |
| 11. | Karaha |

Chanzo: Data kutoka katika Tamthiliya ya *Mashetani Wamerudi*, 2017

Jadwali namba 10 hapo juu linaonesha tamathali za semi ambazo zimeonekana kutumika katika tamtiliya ya *Mashetani Wamerudi*.

Kama inavyoonekana katika jadwali hilo tamathali za semi ambazo zimetumika ni tashibiha, sitiari, tashihisi, takriri, ishara na mubalagha. Vipengele hivyo vimefanyiwa uchambuzi kama ifuatavyo:

#### 4.5.2.7.1 Tashibiha

Ni tamathali ya usemi inayotoa mfano wa vitu unaojengwa kwa maneno kwa kulinganisha vitu viwili au zaidi kwa kutumia vilinganishaji, kama, mithili ya na kadhalika (Jilala, 2016). Katika Tamthiliya ya *Mashetani Wamerudi* data zinaonesha kuwa Tamthiliya hiyo imetumia mtindo huu kama ifuatavyo:

*"Shetani anachipuka ghafla kama mche wa mti" (uk.47).*

Katika dondoo ya hapo juu msanii anaonesha namna mapambano dhidi ya ukoloni mambo leo yalivyo na changamoto. Msanii anaieleza jamii kwamba pamoja na harakati mbali mbali zinazofanywa mataifa machanga ili kuondokana na ukoloni mamboleo bado hatua hizo hazijazaa matunda. Hii inatokana na Wakoloni kuzaa mbinu mpya za ukoloni mamboleo kila uchao. Mifano mengine ya matumizi ya tashibiha ni kama ifuatayo:

*(i)* *"Uongo ni msimamo mwepesi kama njukuti mara moja hukatika kwa mwenye kujua" (uk. 6)*
*(ii)* *"Katika ndoto inaonekana wazi wazi kama binadamu kijana" (uk. 47).*
*(iii)* *"Huku utaona na kujitupa kama mzogaau utatiririka machozi" (uk. 2).*
*(iv)* *"Amesawijika uso kama vile kakasirika" ( uk. 8).*
*(v)* *"Anapiga kelele kama vile anafurusha ndege kwenye shamba la mpunga" (.uk 16).*
*(vi)* *"Anakwenda huku na huku kama askari wa doria" (uk .23).*

(vii) *"Kijana bado anajipiga kifua kama sokwe" (uk 53).*

(viii) *"Wananchi ananguruma kama ngurumo za radi" (uk58).*

#### 4.5.2.7.2 Tashihisi

Senkoro (1982), anafasili tashihisi kuwa ni tamathali ya usemi ambayo wakati mwingine huitwa tamathali ya binadamu. Kwa tamathali hii vitu visivyo na sifa walizonazo watu hupewa sifa hizo. Katika Tamthiliya ya *Mashetani Wamerudi* mtindo wa kitashihisi umetumika kama ifuatavyo:

*"Uongo unacharaza ovyo pamoja na udanganyifu ili kuukandamiza ukweli" (uk. 5).*

Katika dondoo hii hapo juu msanii ametumia mtindo wa kitashihisi ambapo uongo unapewa sifa ya kupambana na ukweli. Kupitia tashihisi hii msanii anaonesha nama ukweli leo hii ulivyokuwa hauna nafasi katika jamii nyingi. Badala yake nafasi ya ukweli imezibwa na uongo na kuufanya ukweli ni kama ndoto katika maisha ya kila siku. Wale wanaojikita katika ukweli mara nyengine huonekana kuwa ni maadui wa jamii. Mifano mengine ya matumizi ya tashihisi ni kama zifuatazo:

(i) *"Hatusemi wazi kwasabu ukweli siku hizi ni mwiko" ( uk 6.*

(ii) *"Mazingira yanakubali kwa siri" (uk. 2).*

(iii) *"Uongo unacharaza ovyo pamoja na udanganyifu ili kuukandamiza ukweli" (uk. 5).*

(iv) *"Njia ya uchumi iliyofumba kiza" (uk. 33).*

(v) *"Masikio yetuyanayosimama yana sikia mno" (uk 24).*

(vi) *"Kwa namna hii, sehemu kubwa ya nchi imefyatuka kwa vile magoti ya nchi wenyewe yamevunjika" (uk.35).*

#### 4.5.2.7.3 Sitiari

Ni tamathali ya semi inayotumika kuumba picha fulani inayotoa athari fulani au inayoamsha mwitikio fulani kutoka kwa hadhira (Mulokozi, 2002). Katika

Tamthiliyaya *Mashetani Wamerudi*data zinaonesha kwamba tamthili hii imetumia mtindo wa kisitiari kama ifuatavyo:

*"Wewe ni Chozi na mimi ni Tembo" (uk. 20).*

Katika dondoo hio hapo juu msanii ametumia sitiari ambapo analinganisha tembo (mataifa yenye nguvu) na chozi (mataifa ya kimaskini ya dunia ya tatu). Anaonesha kwamba nchi za dunia ya tatu haziwezi kushindana na nchi tajiri zilizoendelea katika sera za utandawazi kama vile; sera za ubinafsishaji na uekezaji. Matokeo ya sera hizi ni ukandamizaji unaoendelea dhidi ya mataifa ya dunia ya tatu. Sera ambazo hazina nia njema kwa nchi hizo zimekuwa zikididimiza uchumi wa nchi changa na kulazimisha siasa chafu. Mifano mengine ya matumizi ya sitiari katika Tamthiliya ya *Mashetani Wamerudi* ni kama ifuatavyo:

*(i) Nyinyi mnatoa lakini utoaji wenu wa sadaka ni ulimbo unaotega ndege ili wanaswe! (uk. 50)*

*(ii) Sisi wananchi tumefanywa vinyago au mabwege (uk. 55)*

*(iii) Wema wetu ndio ndoana ya kuua samaki (u. 71)*

### 4.5.2.7.4 Takriri

Ni mtindo wa usemi ambao msemaji hurudia neno au maneno yale yale kwa makusudi ya kutia mkazo au kusisitiza katika jambo. Salem (2013), anawanukuu Kahigi na Mulokozi (1979), wakiielezea takriri kuwa ni uradidi, yaani urudiaji wa sauti, neno, kirai, kishazi na hata sentensi katika kazi za kifasihi. Katika Tamthiliya ya *Mashetani Wamerudi* data zinaonesha kwamba msanii ametumia mbinu ya takriri kama ifuatayo:

> *"Amkeni watetezi wa uhuru wa haki, Amkeni Waaafrika ... Amkeni Waasia, Amkeni Karebian" (uk. 28)*

Katika dondo hiyo hapo juu msanii amerudia rudia neno *amkeni* ili kuonesha umuhimu wa kufanya harakati za ukombozi ulimwenguni ili kuondokana na ukoloni mamboleo. Ukoloni ambao umekuwa ukikandamiza nchi hizi ambazo zinanyonywa na nchi zilizoendelea. Msanii anaonesha kuwa si bara la Afrika tu ambalo linakabiliwa na tatizo la ukoloni mamboleo bali Waasia na wananchi kama vile Karebania ukoloni mamboleo bado ni tatizo. Mifano mengine ya takiriri ni kama ifuatayo:

*(i)* *"Wamesharudi…wamesharudi…wamesharudi" (uk. 7).*

*(ii)* *"Amkeni watetezi wa uhuru wa haki, Amkeni Wafrika ... Amkeni Waasia, Amkeni Karebian" (uk. 28).*

*(iii)* *"Karibu. Karibu basi. Karibu sana. Karibu msichana mwerevu ulieamka" (uk. 31).*

*(iv)* *"(Kijana mmoja anatingisha huku akijipiga kifuani) bado, bado, bado…mimi shujaa"( uk. 53).*

*(v)* *"Hatukubali…..hatukubali tena….kamwe hatukubali" (uk. 60).*

*(vi)* *"Wananchi…Wananchi…Wananchi" (uk. 76).*

*(vii)* *"Wanakuja na virungu… wanakuja na virungu" (uk.7).*

*(viii)* *"Shina la mbuyu…shina la mbuyu" (uk. 7).*

### 4.5.2.8 Majazi

Ni jina lenye kubeba maana ambayo aghalabu huakisi tabia au hali ya mhusika mwenye jina hilo. (Senkoro, 1982). Mwandishi wa Tamthiliya ya *Mashetani Wamerudi* ametumia majazi kama vile;

Jina la *Shetani*

Jina la *Prof.*

Shetani ni jina lilotumiwa kimajazi. Jina hili linaakisi hali halisi ya ukoloni mamboleo ambao umekuwa ukikandamiza na kunyonya mataifa maskini

ulimwenguni. Kama ilivyo kawaida ya shetani, mhusika huyu amekuwa akijitapa kutokana na vitimbi vyake. Kwa mfano, Sheta anasema:

> *"Hapa si petu sisi? Sipetu hapa? Kasema nani? Sisi ni wananchi wa nchi zote duniani…Hapana nguvu yoyote ya kutudhibiti maana sisi tuko nchini mwetu tunabonyeza remote control. Kwani mmesahau kwamba utandawazi ndio remote control zaidi kuliko ukoloni mamboleo" (uk. 61).*

Katika maelezo ya hapo juu msanii anaonesha namna wakoloni walivyojimilikishia ulimwengu na kuufanya chini ya mamlaka yao. Wakoloni leo hii wanatumia sera ya utandawazi kudhibiti ulimwengu na kutenda mambo kwa manufaa yao. Hivyo, lazima nchi changa zitambuwe kuwa zimekumbwa na janga kubwa zaidi la sera ya utandawazi ambayo nia yake ni kukandamiza na kunyonya nchi maskini kwa mbinu mpya.

**4.5.2.9 Mdokezo**

Mdokezo ni hali ya mtunzi kukatiza maneno au kuacha maneno bila kukitaja kitu au maneno ambayo kwa kawaida ni wazi na huweza kujazwa kwa ubunifu (Wamitila, 2008). Data zilizokusanywa na mtafiti kutoka Tamthiliya ya *Mashetani Wamerudi* zilionesha kuwa Tamthiliya hiyo imetumia mtindo wa mdokezo kama ifuatavyo:

> "*Hatukubali…Hatukubali kamwe…" (uk.60)*

Katika dondoo ya hapo juu msanii ametumia mdokezo. Ambapo anadokeza harakati za wananchi kutaka kujikomboa dhidi ya ukoloni mamboleo ambao umekuwa ni kikwazo kikubwa katika ujenzi wa jamii mpya. Hii ni kusema kuwa baadhi ya watu leo hii, kama vile mhusika Prof. katika Tamthiliya ya *Mashetani Wamerudi* wanauelewa juu ya vitimbi vinavyofanywa na wakoloni ambavyo vinalengo la

kunyonya na kukandamiza bara hili la Afrika. Hivyo, wako msitari wa mbele katika kupinga sera kandamizi za kikoloni. Mifano mengine ya mdokezo ni kama ifuatayo:

*(i) "Mpaka leo…mpaka leo" (uk.8).*
*(ii) "Mazingaombwe mapya …" (uk.11).*
*(iii) "Sijui kama…kama…kama ninafanya mchezo…Naona nime…" (uk.33)*
*(iv) "Bwanyenye, mla mla ya umma…Aaaa" (uk.41).*
*(v) "Mimi?...Mimi unanijuwa?...Unanijua mimi?..." (uk.39).*
*(vi) "Prof…. Hata nikiondoka hapa ni petu…" (uk. 53).*
*(vii) "Wananchi…wanachi….wananchi" (uk. 75).*
*(viii) "Hatutaki...Hatutaki…" (uk. 75).*
*(ix) "Tunataka amani…Tunataka amani…Tunataka amani…" (uk.75).*

#### 4.5.2.10 Nidaa

Ni msemo unaoonesha kushangaa au kushangazwa na jambo fulani (Senkoro, 2011). Data za utafiti huu zinaonesha kuwa mbinu hii pia imetumiwa na msanii wa Tamthiliya ya *Mashetani Wamerudi* katika kuisanii kazi yake. Mifano ya matumizi ya nidaa katika Tamthiliya hii ni kama ifuatavyo:

*"Nitakuwepo tena na tena!" (uk. 44)*

Katika dondoo hii msanii ametumia mtindo wa nidaa ili kuonesha ukoloni mamboleo ulivyojikita katika bara la Afrika hata baada ya nchi hizi kupata uhuru wa bendera. Maelezo haya yanayotolewa na sheta (mkoloni), ni dalili ya mipango ya muda mrefu ya kuhakikishi kuwa ukoloni utaendelea kuwepo katika bara hili pamoja na harakati nyingi zinazofanyika ili kujitoa kutoka katika makucha ya kikoloni. Mifano mengine ya matumizi ya nidaa ni kama ifuatayo:

*(i) "Prof… Mfukuze haraka! Anahaha profesa" (uk 11)*
*(ii) "(Analalamika) kichwa kinaniuma!" (k 13)*

*(iii) "Utaumwa ugonjwa wa upumbavu daima! (Anashtuka) milele! Daima?" (uk. 23)*

*(iv) "Kinachotisha ni mashuzi!" (uk 19).*

*(v) "Kinyume na walivyosema wao!" (uk.22)*

*(vi) "kuna wakubwa wako njiani wanakuja!" (uk. 23)*

*(vii) "huku wakicheza!" (uk. 24)*

*(viii) "Ha! Haaaaa!" (uk. 25)*

*(ix) "Wewe ! siku moja!" (uk. 26)*

*(x) "Lo! Looo ya nini? Tazama uone!" (uk. 27)*

*(xi) "Ninayo! Basi haya! Ikanitia kizunguzungu cha kizungu!" (uk. 29).*

*(xii) "Ewaaa!" (uk. 30).*

*(xiii) "Ahaaa, wewe kumbe!" (uk. 32)*

*(xiv) "ugonjwa wa kukwepa hapa Afrika ni ugonjwa mbaya kabisa!" ( uk. 33.)*

*(xv) "Nitakuwepo tena na tena!" (uk. 44).*

*(xvi) "bila hivyo tutakufa!" (uk. 45).*

*(xvii) "Kheri ya kuonana" (uk 45).*

#### 4.5.2.11 Mchanganyo Ndimi

Data za utafiti huu zinaonesha kuwa wahusika wa Tamthiliya ya *Mashetani Wamerudi* imetumia misamiati ya lugha za kigeni. Matumizi ya mbinu za uchanganyaji ndimi imetumiwa kama ifuatavyo:

> *sauti kubwa ya kujenga ubwana…teke la grand narratives likipigana na public narratives chini kuna grand narratives (uk. 15)*

Katika dondoo ya hapo juu msanii ametumia misamiati ya lugha ya Kiengereza kama vile grand narratives akiashiria athari za ukale katika bara la Afrka na *public narrative* akiashiria athari za ukoloni mamboleo ambao umeenea sasa katika bara hili la Afrika. Mifano mengine ya mchanganyo ndimi ni kama ifuatayo:

*(i) "Coca cola atawezaje kutia fora mbele ya togwa?" (uk 7-8)*

*(ii) “Abbrogation yaani vidonge vya dawa ndani ya sheria ya kufuta na*
*(iii) kukanusha” (uk.8*
*(iv) Sheta: Rubish..*

*Prof: Rubish au Rabishi?*
*Sheta: Rubish au labda Rubishi (uk.20)*

(i) *“Colonial discourse ipo hadi sasa sema utakalo andika utakalo, tupingeubwana wao mradi kejeli tu kilichopo kwa upande wetu na upande wao” ( uk 22)*
(ii) *“Sisi tuna counter discourse” (uk 22)*
(iii) *“Decolonization” (uk. 28)*
(iv) *“Public narratives ndio inayotaka hata kama kila mtu akisema sentensi moja tu ni sawa” (uk. 34).*
(v) *“Mna mengi ya kulalamika hasa kwenye mitandao ya kijamii kama vile facebook na WhatsApp” (uk. 34)*
(vi) *Si kwa utamaduniwa Oksidental au Occidental, bali kuna Oriental pia” (uk.17).*

Mwandishi ametumia lugha ya kingereza kwa baadhi ya wahusika wake kama vile Prof. Kijana 1, Kijana 2 na Kijana 3 ili kuonesha athari za elimu ya Kimagharibi katika bara la Afrika. Pia, imetumika ili kuonesha tabaka la wasomi waliopata Elimu ya Kimagharibi. Kwa hivyo, ni kawida kwa wasomi wanapokuwa katika mazungumu mara nyingi huwa wanachanganya lugha. Hivyo msanii amelionesha hili ili kuleta mvuto na mnaso katika mazungumzo ya wasomi kama ni kitambulisho cha athari ya kikoloni.

#### 4.5.2.12 Kweli Kinzani katika *Mashetani Wamerudi*

Data za utafiti zilizokusanywa kutoka katika Tamthiliya ya Mashetani Wamerudi zinaonesha kuwa Tamthiliya hiyo imetumia kweli kinzani. Kwa mfano, kuna kweli kinzani inayosema:

*"shetani aliepo ingawa hayupo, yaani hayupo na sasa yupo" (uk. 11).*

Katika dondoo hilo hapo juu msanii anaonesha namna hali ya ukoloni mamboleo ilivyo katika jamii. Msanii anaonesha kuwa ile dhana ya kuwa Afrika ilifanikiwa kuondoa ukoloni sivyo ilivyo. Hii ni kwa sababu wakoloni waliondoka kutokana na ukoloni mkongwe hata hivyo, leo hii ukoloni umerejea kwa mbinu mpya. Ukoloni uliondowa utawala wake wa moja kwa moja katika kuzitawala nchi za Kiafrika. Hata hivyo, wakoloni huko huko kwao wamekuwa wakitunga sera ambazo zinazisukuma nchi za dunia ya tatu kutekeleza sera hizo kandamizi. Mifano mengine ya kweli kinzani katika Tamthiliya ya Mashetani Wamerudi ni kama ifuatayo:

*(i) Sisi hatufi kifo cha kifo, tunakua kifo cha kuwepo (uk. 16)*
*(ii) Kabla hujaondoka maana wewe hufa leo…(uk. 47)*

#### 4.5.2.13 Mjalizo katika *Mashetani Wamerudi*

Data za utafiti zinaonyesha kwamba mwandishi wa Tamthiliya ya*Mashetani Wamerudi* ametumia mtindo wa mjalizo.Mifano ya mjalizo katika Tamthiliya hii imejitokeza kama ifuatavyo:

*"Ujamii, utamaduni, elimu, uchumi, teknolojia, sayansi, kilimo vyote vimebanwa" (uk.23).*

Katika dondoo hapo juu msanii anadokeza namna nchi za dunia ya tatu zilivyokwama katika kila nyanja ya maisha. Nchi hizi zimevamiwa na wakoloni katika masuala ya kijamii, utamaduni, elimu, uchumi, teknolojia, sayansi, na kilimo. Kwa mantiki hiyo, hali ya nchi za dunia ya tatu bado ni mbaya kutokana na athari za kikoloni. Mifano mengine ya mjalizo katika Tamthiliya ya Mashetani Wamerudi ni kama ifuatayo:

*"Vitu, mambo, majambo matendo, biashara" (uk. 8).*

*"Anatazama huku na huku mara nyingi, kulia na kushoto, nyuma na mbele,huku anatuta na kutoa pumzi kwa nguvu" (uk. 16).*

*"Sisi hatufi kifo cha kifo, tunakufa katika kifo cha kuwepo" (uk. 16).*

#### 4.5.2.14 Karaha katika *Mashetani Wamerudi*

Huu ni utumiaji wa maneno ambayo huleta karaha au matusi kwa watu. Maneno haya huwa hayakubaliki na wanajamii kuzungumzwa katika hadhara ya watu. Katika Tamthiliya ya *Mashetani Wamerudi* msanii ametumia mtindo huu kama ifuatavyo:

*"Alikojoa" (uk.14).*

Neno la hapo juu inaonesha matumizi ya karaha ambapo Uswahilini neno"*alikojoa"* huleta karaha kwa wasikilizaji.Neo hili huondolewa katika mazungumzo ama maandishi kwa kutumia neo *"kujisaidia"* likiwa na maana ya kwenda *"haja ndogo."* Mifano mengine ya matumizi ya karaha katika Tamthiliya ya Mashetani Wamerudi inajitokeza katika mifano ifuatayo:

(i) "*Si mizinga, si **mashuzi** Profesa" (uk.12)*

*(ii) "Jamaa zako wanaanza **kujikojolea** mikojo na kujipaka kinyesi" ( uk. 27)*

*(iii) "Kinachotisha ni **mashuzi**" (uk. 19)*

#### 4.5.2.15 Matumizi ya Lahaja katika *Mashetani Wamerudi*

Data za utafiti huu zinaonyesha kwamba msanii wa Tamthiliyaya *Mashetani Wamerudi*ametumia maneno ya lahaja ya Kipemba. Matumizi ya lahaja yamejidhihirisha kama ifuatavyo:

"*Kiduchu kiduchu" (uk. 24)*

"*Nitaselelea papa hapa petu" (uk. 78)*

Katika maelezo ya hapo juu kuna matumizi ya neno *kiduchu kiduchu* ambalo lina maana ya *kido*  na neno *papa papa* lenye maana ya *hapa hapa*. Matumizi ya lahaja ya Kipemba yanatokana na historia ya mtunzi wa Tamthiliya ya Mashetani Wamerudi kuwa ni mzaliwa wa Kisiwa cha Pemba na lahaja ya Kipemba ni lugha yake ya kwanza.

#### 4.5.2.3 Mbinu Nyengine za Kimtindo katika *Mashetani Wamerudi*

Mbali na vipengelevya kimtindo vilivyotumka pia kuna matumiziya mbinu nyengine za kimtindo kama ifuatavyo:

**Jedweli Na. 4.12: Matumizi ya Mbinu Nyingine za Kimtindo katika *Mashetani Wamerudi***

| Na. | Mbinu ya Kimtindo |
|---|---|
| 1. | Mtindo wa Nyimbo |
| 2. | Mtindo wa Ndoto |
| 3. | Mtindo wa Masimulizi |
| 4. | Mtindo wa Matumizi ya Nafsi |
| 5. | Mtindo wa Wahusika wa Fasihi Simulizi |
| 6. | Mtindo wa Mandhari ya Fasihi Simulizi |
| 7. | Mtindo wa Majigambo |

Chanzo: Data kutoka Mashetani Wamerudi. Julai, 2017

Data zilizokusanywa na mtafiti zinaonesha kuwa Tamthiliya ya *Mashetani Wamerudi* imetumia mbinu nyengine za kimtindo kama zinavyoonekana katika jadwali namba 11. Mitindo hiyo ni mtindo wa nyimbo, mtindo wa ndoto, mtindo wa masimulizi, mtindo wa matumizi ya nafsi, mtindo wa wahusika wa fasihi simulizi, mtindo wa mandhari za fasihi simulizi na mtindo wa majigambo. Vipengele hivi vimefanyiwa uchambuzi kama ifuatavyo:

#### 4.5.2.3.1 Mtindo wa Nyimbo katika *Mashetani Wamerudi*

Nyimbo ni kila kinachoimbwa (Mulokozi, 1996). Data zilizokusanywa na mtafiti kutoka Tamthiliya ya *Mashetani Wamerudi* zilionyesha kwamba Tamthiliya hii imetumia mtindo wa nyimbo kwa kiasi kikubwa. Msanii amemtumia mhusika Mwanambele ambapo kila mwanzo wa onesho mhusika huyo anaimba nyimbo. Mifano ya nyimbo hizo imejidhihirisha kama ifuatavyo:

*Jambo hilo la kihoro,*
*Lile jambo la kihoro,*
*Jambo lile la kiwewe,*
*Tena jambo la kiwewe,*
*Jambo lile la kidonda,*
*Tena homa ya kidonda,*
*Aaaa, 'ukoloni'ni kihoro,*
*Ukoloni ni kiwewe na kihoro,*
*Ukoloni homa ya kidonda!*
*Hasa hasa ukoloni mamboleo,*
*Umepewa jina jipya,*
*Linaloitwa utandawazi. (Uk10)*

Maelezo ya hapo yanaonesha kuwa bado ukoloni ni kikwazo kikubwa katika jamii. Msanii anaufananisha ukoloni na kihoro, kidonda na kiwewe. Msanii anaona kwamba ukoloni leo hii umekuja kwa mbinu mpya. Ambapo leo hii ukoloni umebeba sura ya utandawazi. Hivyo, athari za utandawazi zimekuwa mwiba kwa nchi changa. Kwa mantiki hii sera za utandawazi kama vile soko huria, ubinafsihaji, uekezaji na upokeaji na utoaji mikopo kwa nchi maskini ni mbinu tu za kikoloni katika kuendeleza unyonyaji. Mfano mwengine wa mtindo wa nyimbo unasema:

*Mwanambele: (Anaingia kwa mahaba. Mwanambele.*

*Anaimba kwa sauti wimbo wa sheria)*

*Sheria zilizotumika zamani na jinsi tulivyoachiwa sasa,*

*Sheria walizoturithisha,*

*Sheria za kuchukua mali zetu,*

*Sheria wanazotupunja katika kandarasi,*

*Kwa pesa ndogo na thamani kubwa (uk.39).*

Katika wimbo wa hapo juu msanii anajadili sheria zinazotumika katika bara la Afrika. Sheria hizo ni zile tulizozirithi kutoka kwa wakoloni. Msanii anaonesha kwamba bado sheria hizo zina myanya ya ukoloni mamboleo. Sheria hizo hutoa nafasi kwa nchi maskini kuendelea kunyonywa na kukandamizwa na wakoloni wakishirikiana na vibaraka wa wakoloni. Mfano mwengine wa mtindo wa nyimbo unasema:

*Mwanambele: (Wimbo wa umoja )*
*Kamateni mikono,*
*Shikamaneni pamaja,*
*Vishindo vitakuja ,*
*Lakini vitadunda,*
*Vitadunda vitadunda*
*Vitadunda siku ya kudunda!*
*Kwa sababu sisi tumekamatana,*
*Kama nguvu za minyororo(.uk63)*

Wimbo huu unawataka Waafrika kushikamana, kushirikiana na hatimae kuwa kitu kimoja ili kuleata umoja na mshikamano miongoni mwao katika kupambana na dhulma, uonevu, ukandamizaji na unyonyaji unaofanywa na wakoloni. Wafrika wajuwe kuwa katika kupambana na ukoloni kunachangamoto watakumbana nazo hata hivyo changamoto hizo watazishinda iwapo Afrika itakuwa kitu kimoja.

#### 4.5.2.3.2 Matumizi ya Ndoto *Mashetani Wamerudi*

Data za utafiti huu zinatuonyesha kwamba mwandishi wa Tamthiliya ya *Mashetani Wamerudi* ametumia mtindo wa ndoto kwa kututoa katika ulimwengu halisi tuliouzowea na kutupeleka katika ulimwengu wa ndoto baina ya kifo na uhai. Msanii matumizi ya mtindo huu kwa kumtumia Prof. kama ifuatavyo**:**

> *Prof: Amechoka. Anaanza kulala na kuota.Tochi kali ina mwangaza lakini haamki. Kitanda cha mayowe kinatetemeka kila akigeuka geuka. Anafurukuta na kuweweseka yumo ndotoni. Ndoto ya vijana wanaoanza kuchachamaa. Anaota kwa fikra ya nchi yake lini itakwamuka. Mara anaanza kukoroma. Chenene analia nje, bila ya kunyamaza. Katika ndoto yake, Prof. anaonana na kijana. Ndani ya ndoto Prof. na kijana wanapambana na kulumbana na shetani (uk46*

Mwandishi anaonyesha jinsi wasomi katika bara la Afrika walivyo na msimamo wa kutaka kuondokana na ukoloni mamboleo. Msanii anamtumia mhusika Prof. akiwa ni mfano wa wasomi waliomstari wa mbele katika kupambana na ukoloni. Kwa hivyo, mwandishi wa Tamthiliya hii anaona kuwa vijana ndio nyezo ya kipekee katka kuleta mabadiliko katika nchi hii na bara la afrika kwa ujumla. Jambo la kufurahisha na kutia moyo ni kwamba vijana leo hii nao wameamka na wako mstari wa mbele katika kuleta mabadiliko katka nchi yao ili kupigavita ukoloni mamboleo.

#### 4.5.2.3.3 Mtindo wa Masimulizi katika *Mashetani Wamerudi*

Msanii wa Tamthiliya ya Mashetani Wamerudi ametumia mtindo wa masimulizi katika Tamthiliya yake kama ifuatavyo:

> *Kijana 1: Tunatazamwa na mabwana zetu sawa na Punda wa dobi aliyekamatwa kwa rai ili awe mke wa simba. Hatimae simba amrukie punda na kumparura kwa kucha na kumtoa damu lakini katika kujivuta aliwahi kukimbia na kutoroka. Baadae kwa kutumia mbinu ile ile ya kutaka kuolewa, alidai kwa mara ya pili. Simba alimngojea*

> *kwa hamu na alipofika huko alimkamata na kumvamia Punda kwa nguvu na kumkata vipanda mbali mbali na kumla* (uk.56).

Katika maelezo haya msanii ametumai mtindo wa masimulizi kupitia Kijana 1 ambaye anaeleza kisa cha simba na punda na kilichotokea kwa punda baada kutokana na kitendo kibaya alichofanyiwa na simba. Kupitia simulizi hii msanii yaelekea anaimani kwamba iko siku itakuwa kweli. Siku ambapo ukoloni utashindwa na mataifa ya dunia ya tatu.

#### 4.5.2.3.4 Mtindo wa Matumizi ya Nafsi katika *Mashetani Wamerudi*

Data zilizokusanywa katika Tamthiliya ya *Mashetani Wamerudi* zinaonesha kwamba msanii ametumia nafsi zote tatu. Baadhi ya mifano ya matumizi ya nafsi hizo imefanyiwa uchambuzi kama ifuatavyo:

##### 4.5.2.3.4.1 Mtindo wa Nafsi ya Kwanza

Data zinaonesha kuwa katika Tamthiliya ya *Mashetani Wamerudi* kuna matumizi ya nafsi ya kwanza. Mathalan mhusika Shetani anatumia nafsi ya kwanza wakati wakati akieleza namna anavyoweza kujibadilisha. Kwa mfano, msanii anasema:

> *"Shetani: Nitazame mwili wangu, nitazame nafsi yangu"* (uk. 72).

Katika maelezo ya hapo juu msanii anatuonesha namna ukoloni unavyochukua sura tofauti tofauti. Leo hii wakoloni wamekuwa wakibadilika kwa kubadilisha sera za utandawazi ambazo zina nia ya kuendeleza ukoloni katika nchi changa.

##### 4.5.2.3.4.2 Mtindo wa Nafsi ya Pili

Pia, data zinaonesha kuwa Tamthiliya ya Mashetani Wamerudi imetumia nafsi ya pili. Mathalani, matumizi ya nafsi ya pili tunayaona wakati wa mazungumzo kati ya mhusika Prof. na kijana. Mazungumzo hayo yanasema:

*"Ukiwa karibu nae ushuzi wake ukikuingia bongoni basi utaumwa na* kichwa milele" (uk 13).

Msanii hapo juu anatumia taswira ya ushuzi kuingia katika bongo na matokeo yake ni kupata ugonjwa. Kupitia mazungumzo haya msanii anaonesha kuwa ushirika ambao wamekuwa wakiufanya wakoloni katika Bara la Afrika huwa hauna mwisho mwema. Hii ni kwa sababu matokeo ya ushirikiano dhidi ya wakoloni ni kuzififisha nchi changa katika kila nyanja ya maendeleo.

**4.5.2.3.4.3 Mtindo wa Nafsi ya Tatu**

Pia, data katika Tamthiliya ya Mashetani Wamerudi zinaonesha kuwa kuna matumizi ya nafsi ya tatu. Mathalani, matumizi ya nafsi ya tatu tunayaona wakati mhusika Prof. akisimulia hoja za mataifa tajiri ambayo yanaendeleza ukoloni ulimwenguni. mfano,

*"Wakakataa mashetani kuwa wanaangamiza watu" (uk 14)*

Mwandishi hapo juu ameonesha kuwa pamoja na athari mbaya ambazo wamekuwa wakisababisha wakoloni katika nchi maskini bado wanadai kuwa wao ni wahisani na wanasaidia nchi hizo. Hii ni kauli ya kinafiki ili kuwaaminisha Waafrika kuwa wahisani wao wakubwa ni mataifa yaliyowahi kuwa wakoloni wao. Hata hivyo, ukweli unabakia kuwa ukoloni mamboleo unaendelea kuwa na athari mbaya kwa nchi maskini.

**4.5.2.4 Mtindo wa Kutumia Wahusika wa Fasihi Simulizi katika *Mashetani Wamerudi***

Data za utafiti huu zinaonesha kwamba mwandishi wa Tamthiliya ya *Mashetani Wamerudi*ametumia wahusika ambao hutumika katika fasihi simulizi za kiafrika.

Mathalani, mwandishi ametumia wahusika kama vile; shetani, jogoo, simba, punda, kuku na bata mzinga. Mhusika Sheta ni mfano wa mhusika wa fasihi simulizi wanaopatikana katika hadithi simulizi za Uswahilini. Mhusika Sheta ametumika kuwakilisha ukoloni mamboleo katika bara la Afrika. Mwandishi amedhihirisha mtindo kama ifuatavyo:

> *"nyuma ya kibanda sheta alijigeuza kuku au bata mzinga akanifukuza mimi" (uk 29*)

Katika maelezo ya hapo juu msanii anamtumia mhusika sheta akiashiria ukoloni na namna anvyochukuwa mabadiliko. Kubadilika huko ni ishara ya mabadiliko yanayofanywa wakoloni kila uchao ilikuendeleza ukandamizaji na unyonyaji kwa mataifa maskini. Mifano mengine ya wahusika wa kifasihi simulizi ni kama ifuatavyo:

> *"Kijana anamfukuza jogoo. Jogoo anapaparika. Kokoro, kokoro, kokoro-jogoo anakokoreka" (uk 12).*

> *"Simba alimngojea kwa hamuna alipofika huko simba Alimkamata kwa nguvua na kumvamia punda na kumkata vipande mbali mbali na kumla" (uk. 56).*

### 4.5.2.5 Mtindo wa Mandhari za Kifasihi Simulizi katika *Mashetani Wamerudi*

Data za utafiti huu zinaonesha kwamba mwandishi wa *Mashetani Wamerudi* ameisawiri Tamthiliya yake kwa kutumia mandhari za fasihi smulizi za kiafrika. Kwa mfano, kuna mandhari ya kwenye shina la mbuyuna nyuma ya kibanda. Matumizi ya mandhari ya fasihi simulizi yanajitokeza kama ifuatavyo:

> *"kisha tazameni **kibanda** kile kidogo. Kimesimama tisti. Ndani anatoka mtetezi. Anakuja Profesa hafi leo –wala kesho. Pole pole ataingia uwanjani-uwanja wa utandawazi. Katikati ya **kibanda** karibu na kibanda lipo **shina la mbuyu**. Kinaanza kutoa chipkizi. Zinaota chipkizi. Miaka mingi imepita (uk 2)*

Katika dondoo la hapo juu msanii amechota ujumi wa Muafrika kwa kuchota mandhari za kifasihi simulizi za Kiafrika. Msanii anatumia mandhari ya shina la mbuyu ili kuonesha namna ukoloni mamboleo unavyoendelea kuliathiri eneo hili la Afrika. Mifano mingine ya mandarin za fasihi simulizi ndani ya Tamthiliya ya Mashetani Wamerudi inajidhihirisha kama ifuatavyo:

(i) *"Prof,..anasimama. anakwenda kwenye **shina la mbuyu** kijana anafuata Profesa. Analikagua shina la mbuyu kila kipembe kisha anatizama juu mbinguni" (uk 6).*

(ii) *"Prof...**Shina la mbuyu**, shina la mbuyu-walilibadilisha jiti kubwa lenye virutubisho wakalifanya **tanda la kulalia** na kisha pahala la kurukia katika maendeleo yao" (uk 7).*

#### 4.5.2.6 Mtindo wa Majigambo katika *Mashetani Wamerudi*

Data zilizokusanywa na mtafiti zinaonesha kuwa Tamthiliya ya *Mashetani Wamerudi* imetumia mtindo wa majigambo. Mhusika Sheta (mkoloni) amekuwa akijisifia kutokana na uwezo walionao. Pia, sheta naonesha kuwa wanauwezo wa kuhodhi mamlaka ya kiulimwengu. Mfano wa jigambo ni pale mhusika Sheta anaposema:

"*Sheta: Ndiye mimi.Ndiye ndiye mimi hasa! Mimi wa eropleni na maroketi na mizinga*

*Aaa, mara moja hii umenitambua mimi nani? Ewe wa zamani (uk17")*

#### 4.5.2.7 Mtindo wa Tamthiliya ya Majaribio katika *Mashetani Wamerudi*

Katika utafiti huu mtafiti alichunguza mbinu za kimtindo ambazo zimetumika kutunga Tamthiliya ya *MashetaniWamerudi.* Hivyo basi, data zilizokusanywa kutoka Tamthiliya ya *MashetaniWamerudi* zilibainisha kuwa Tamthiliya hii ni ya kimajaribio. Mathalani, tunaona kuna matumizi ya masimulizi, ambapo

tunasimuliwa hadithi ya punda na simba katika kutoa taswira ya ukoloni mamboleo ambao unafananishwa na simba ambae alikuwa akimsumbua punda (nchi za dunia ya tatu). Hali hii ni sawa na ukoloni leo hii ambapo mataifa matajiri yamekuwa yakiziendesha nchi maskini vile wanavyotaka wao kwa manufaa yao binafsi.

Pia, mwandishi wa Tamthiliya hii ametumia wahusika ambao hutumiwa na fasihi simulizi mfano mwandishi amemtumia shetani kama mhusika. Kama ilivyokwishaelezwa kabla kuwa kwa kawaida fasihi andishi hutumia wahusika watu, lakini mwandishi anapotumia viumbe wengine ambao si watu ana kuwa anatengeneza kazi yake kuwa fasihi ya majaribio.Vile vile msanii ametumia mandhari tunazokutana nazo katika fasihi Simulizi za Kiafrika. Mathalani, msanii anatumia mandhari ya kwenye mbuyu na kibanda ili kuakisia ujumi wa Kiafrika. Msanii anasema:

> *"Prof,..anasimama. anakwenda kwenye* ***shina la mbuyu*** *kijana anafua Profesa. Analikagua shina la mbuyu kila kipembe kisha anatizama juu mbinguni" (uk 6)*

## 4.6 Kulinganana Kutofautiana kwa Mitindo ya tamthiliya ya *Mashetani na Mashetani Wamerudi*

Sehemu hii inahusu ulinganishaji wa Tamthiliya ya *Mashetani* na Tamthiliya ya *Mashetani Wamerudi* ilikubaini vipengele vya kimtindo vinavyowafananisha na kuwatofautisha waandishi wa Tamthiliya teule.

Ulinganishaji na utofautishaji wa vipengele hivyo umezingatiwa kwa umakini kwa kurejelea lengo mahususi la pili la utafiti huu lisemalo: Kulinganisha na kulinganua matumizi ya mitindo katika tamthiliya teule za *Mashetani* na *Mashetani Wamerudi.*

Kwa hakika lengo hilo mahsusi la pili limekwenda sambamba na swali la pili la utafiti huu lisemalo: Ni jinsi gani mitindo inafanana na kutofautiana katika tamthiliya ya *Mashetani* na *Mashetani Wamerudi*. Hivyo basi uchambuzi unaofuata umezingatia lengo na swali hilo ipasavyo ikihusisha na nadharia ya Fasihi linganishi kama ifuatavyo:

Saleem (2013), anawanukuu Senkoro (1982), Wamitila (2003) na Chimerah (2003), wakieleza kuwa kila mwandishi ama msanii wa kazi ya sanaa hutofautiana na mwandishi mwingine katika maudhui na fani. Kila mwandishi ana upekee wake katika kuwasilisha masuala mbalimbali ya kijamii na namna anavyoyawasilisha ni tofauti na mwandishi mwengine. Utafiti huu ulichunguza sifa za kimtindo zinazotofautisha kazi za *Mashetani* na *Mashetani Wamerudi* ili kuona ni jinsi gani wasanii wa kazi hizo wanafanana ama kutofautiana katika matumizi ya mtindo na dhamira. Ili kufikia lengo hilo mtafiti alichambua data zilizokusanywa kutoka Tamthiliya ya *Mashetani* na *Mashetani Wamerudi* na kisha kubainisha vipengele vya kimtindo na dhamira vilivyotumika. Mtafiti aliviweka pamoja vipengele ambavyo vilifanana na kuhusiana na vile vilivyokuwa na sifa sawa na kisha kuviweka katika kundi moja. Hivyo basi, sehemu ifuatayo zinajadili kwa kina jinsi Tamthiliya teule zinavyofanana na kutofautiana katika matumizi ya kimtindo.

### 4.6.1 Ulinganishi na Ulinganuzi katika Sifa za Kimtindo katika Mashetani na *Mashetani na Mashetani Wamerudi*

Data za utafiti huu zilionesha kuwa Tamthiliya ya *Mashetani* na *Mashetani Wamerudi* zimetumia mitindo iliyofanana na kutofautiana. Tofauti hizo na kulingana kwa watunzi hawa katika Tamthiliya teule zimejidhihirisha kama ifuatavyo:

#### 4.6.1.1 Kufanana Mitindo ya Mashetani na *Mashetani Wamerudi*

Data za utafiti huu zinaonesha kuwa zipo sifa za kimtindo ambazo zimefanana kwa watunzi waTamthiliya za *Mashetani* na *Mashetani Wamerudi*. Hivyo basi, katika utafiti huu iligundulika kuwa Tamthiliya hizi zina sifa za kimtindo zinazofanana. Kielelezo namba 12 kifuatacho kinaonesha kufanana kwa Tamthiliya hizo teule.

**Jedweli Na. 4.13: Mitindo ya Lugha inavyofanana katika *Mashetani na Wamerudi***

| Na. | *Mashetani* | *Mashetani Wamerudi* | Kufanana |
|---|---|---|---|
| 1. | Jazanda | Jazanda | √ |
| 2. | Taswira | Taswira | √ |
| 3. | Ishara | Ishara | √ |
| 4. | Sitiari | Sitairi | √ |
| 5. | Tashibiha | Tashibiha | √ |
| 6. | Takriri | Takriri | √ |
| 7. | Tashihisi | Tashihisi | √ |
| 8. | Methali | Methali | √ |
| 9. | Misemo | Misemo | √ |
| 10. | Mchanganyo ndimi | Mchanganyo ndimi | √ |
| 11. | Kejeli | Kejeli | √ |

Chanzo: Data kutoka *Mashetani* na *Mashetani Wamerudi*, Julai 2017

Data zinazojitokeza katika Jedwali Na. 4.13 hapo juu zinaonesha kuwa Tamthiliya ya *Mashetani* na *Mashetani Wamerudi* zimefanana katika matumizi ya mitindo ya vipengele vya lugha. Tamthiliya zote zimetumia jazanda, taswira, ishara, sitiari, tashibiha, takriri, tashihisi, methali, misemo na mchanganyondimi.

Kwa mfano, Tamthiliya zote zimetumia taswira ya shetani kuwakilisha ukoloni mamboleo katika bara la Afrika. Pia, tamthiliya zote zimetumia uteuzi wa neno *waltz* ili kuonesha namna mataifa ya Afrika yanavyofuata sera zilizotungwa na wakoloni. Sera ambazo ni kandamizi katika bara hili.

Tukirejelea nadharia ya Mwingilianomatini tunaona kwamba kuna mwingiliano matini katika matumizi ya neno waltz katika Tamthiliya teule. Hii ni dhahiri kwamba mtunzi wa tamthiliya ya *Mashetani Wamerudi* ameathiriwa na matini ya Tamthiliya ya *Mashetani*.

Vile vile, Tamthiliya teule zimetumia mtindo wa uchanganyaji ndimi ambapo wahusika kama vile; Kitaru na Juma wa Tamthiliya ya *Mashetani* na mhusika Prof. wa Tamthiliya*Mashetani Wamerudi* wanatumia maneno ya lugha za kigeni kama vile Kiengereza. Mtindo huu umetumika kuonesha athari za elimu ya kikoloni katika jamii zetu. Elimu ambayo haikuwa na nia ya kumuendeleza Muafrika.

Tukirejeleanadharia ya Fasihi Linganishi ambayo inahusu ulinganishaji wa kazi za fasihi, na Nadharia ya Mwingilianomatini ambayo huonesha muathiriano baina ya kazi moja ya fasihi na kazi nyengine ambazo zinaongoza utafiti huu tumeona kuwa zinalandana na mitindo iliyotumiwa na wasanii wa Tamthiliya teule. Tamthiliya ya *Mashetani Wamerudi* imechota mitindo kutoka katika tamthiliya ya *Mashetani*.

Hivyo, mitindo hiyo imetumiwa na msanii ili kuonesha namna wakoloni walivyovamia nchi za dunia ya tatu kwa kutumia mbinu kandamizi kama vile ubinafsishaji, utoaji wa mikopo na uekezaji na hivyo kuendeleza ukoloni mamboleo.

#### 4.6.1.1.1 Kufanana kwa Mbinu Nyengine za Kimtindo katika Tamthiliya Teule

Tamthiliya teule zimefanana katika mbinu nyengine za kimtindo kama ifuatavyo:

**Jedweli Na. 4.14: Mbinu Nyengine za Kimitindo Zinazofanana**

| Na. | *Mashetani* | *Mashetani Wamerudi* | Kufanana |
|---|---|---|---|
| 1. | Mtindo wa kishairi | Mtindo wa kishairi | √ |
| 2. | Mtindo wa nyimbo | Mtindo wa Nyimbo | √ |
| 3. | Mtindo wa majigambo | Mtindo wa Majigambo | √ |
| 4. | Mtindo wa Matumizi ya nafsi | Mtindo wa matumizi ya nafsi | √ |
| 5. | Mtindo wa mandhari za Fasihi Simulizi | Mtindo wa mandhari ya fasihi Simulizi. | √ |
| 6. | Mtindo wa Matumizi ya Ndoto | Mtindo wa Matumizi ya Ndoto | √ |
| 7. | Mtindo wa Tamthiliya za Majaribio | Mtindo wa Tamthiliya za Majaribio | √ |
| 8. | Mtindo wa majigambo | Mtindo wa majigambo | √ |

Chanzo: Data za utafiti, kutoka *Mashetani* na *Mashetani Wamerudi,* Julai 2017

Jadwali namba 13 hapo juu linaonesha mbinu nyengine za kimtindo ambazo zinafanana katika Tamthiliya ya *Mashetani* na *Mashetani Wamerudi.* Utafiti huu uligundua kuwa, Tamthiliya zote zimetumia mitindo ya kishairi, nyimbo, mtindo wa masimulizi, mtindo wa matumizi ya nafsi, mtindo wa mandhari za fasihi simulizi ndani ya fasihi andishi, mtindo wa kutumia wahusika wa fasihi simulizi, mtindo wa ndoto, mtindo wa majigambo na mtindo wa tamthiliya za Kimajaribio.

Matumizi haya yameonesha uigaji wa mwandishi mmoja na mwengine hasa katika dhima za mtindo huo. Kwa mfano, Tamthiliya za *Mashetani* na *Mashetani Wamerudi* zote zimetumia mhusika Shetani ambaye ni mhusika wa fasihi simulizi zikimaanisha ukoloni mamboleo. Pia, tamthiliya hizi zimetumia mandhari ya kwenye shina la mbuyu zikionesha ujumi wa Muafrika. Vile vile, kuna majigambo ambayo

katika Tamthiliya zote teule yamekuwa yakitolewa na mhusika Shetani ili kuonesha ubabe wa Wakoloni dhidi ya nchi maskini.

Tamthiliya zote teule zimetumia mtindo wa Tamthiliya za kimajaribio ambapo watunzi wamechota tanzu na vipengele vya fasihi simulizi na kuvitumia katika kazi zao. Kwa mfano, Tamthiliya ya *Mashetani* na tamthiliya ya *Mashetani Wamerudi* zimetumia mhusika shetani, mandhari ya kwenye nbuyu, masimulizi ya hadithi simulizi na matumizi ya nyimbo.

Tukirejelea nadharia ya Mwingilianomatini na nadharia ya Fasihi linganishi zinazoongoza utafiti huu ambazo zimelenga kudhihirisha muingiliano wa kazi mbili tofauti na ulinganishaji wake, mtafiti amebaini kuwa tamthiliya ya *Mashetani Wamerudi* imekuwa kama igizo lililofumwa kutokana na kioo kinachomwirika kutoka Tamthiliya ya *Mashetani*. Tamthiliya teule zina mitindo inayofanana kifani na hata kimatumizi katika kuibua dhamira za mtunzi. Hali hii inafanana na ile waliogundua Ngesa na wenzake (2015), kuwa Tamthiliya ya *Mashetani* na Tamthiliya ya *Kijiba chaMoyo* ni kama pande mbili za shilingi moja.

#### 4.6.1.2 Kutofautiana kwa matumizi ya Mtindo katika TamthiliyaTeule

Pia, utafiti huu ulichunguza tofauti za matumizi ya kimtindo zinazotofautisha Tamthiliya ya *Mashetani* na *Mashetani Wamerudi.* Data zilizokusanywa na mtafiti zilibainisha kuwa Tamthiliya teule zinatofautiana katika viwango vya kimtindo ingawa kwa kiwango kidogo sana. Tofauti hizi zinajitokeza kwa namna msanii anavyokitumia kipengele kimoja katika ujenzi wa dhamira za kazi yake. Sifa kuu za kimtindo zinazowatofautisha ni kama zinavyojionesha katika jadwali namba 15 hapo chini.

**Jedweli Na. 4.15: Matumizi ya Kimtindo yanavyotofautisha *Mashetani* na*Mashetani Wamerudi***

| Na | ***Mbinu ya Kimtindo*** | ***Mashetani*** | ***Mashetani Wamerudi*** |
|---|---|---|---|
| 1 | Mbinu ya Taswira | Imetumika Taswira (manyoya, kisu, na binadamu) | Imetumika (jogoo, simba, punda, kuku na batamzinga) |
| 2. | Mtindo wa ngano | Imetumika | Haijatumika |
| 3. | Matumizi ya mchezo ndani ya mchezo | Imetumika | Haikutumika |
| 4. | Matumizi ya lugha ya karaha | Haikutumika | Imetumika |
| 5. | Matumizi ya lahaja | Haikutumika | Imetumika |

Chanzo: Data za utafiti kutoka *Mashetani* na *Mashetani Wamerudi* Julai, 2017

Data za hapo juu katika jadwali namba 14 zinaonesha kwamba Tamthiliya hizi pamoja na kufanana kwa ukaribu mkubwa katika kutumia mbinu za kimtindo kuna mwanya mwembamba unaoonesha tofauti ya mitindo iliyotumika katika Tamthiliya teule. Tofauti hizo zilifanyiwa uchambuzi kama ifuatavyo:

Tofauti ya kwanza ni katika baadhi ya taswira walizozitumia. Waandishi wote wamejenga Tamthiliya zao kwa kutumia taswira zinazosawiri dhamira ya ukoloni hasa katika matumizi ya taswira ya shetani. Pamoja na kwamba wasanii wote teule wametumia taswira tofauti iliopo ni kwamba mtunzi wa Tamthiliya ya *Mashetani Wamerudi* ametumia taswira kama vile; jogoo, simba, punda, batamzinga, chozi, tembo na kuku katika kusawiri unyonyaji na ukandamizaji wa kikoloni. Msanii wa *Mashetani* ametumia taswira ya binadamu, manyoya na kisu ili kuonesha mgongano uliopo kati ya Waafrika na Wakoloni.

Tofauti nyingine iliyojitokeza ni namna ambavyo watunzi walivyotumia igizo katika kujenga dhamira. Katika Tamthiliya ya *Mashetani* msanii ametumia mchezo ndani ya mchezo ili kujenga dhamira ya ukoloni. Msanii anatumia mchezo wa shetani na binadamu ambapo katika mchezo huo, Binadamu anamuua Shetani kwa kisu alichopewa na Shetani mwenyewe na baadaye Shetani anamcheka na kumwambia nimerudi tena kwa sura nyingine.

Hapa msanii anaonyesha kuwa harakati za kuondokana na ukoloni bado hazijafanikiwa. Kwa upande wa Tamthiliya ya *Mashetani Wamerudi* tunaona kuwa hakuna mchezo ndani ya mchezo, bali msanii anatumia taswira ya shetani ambaye amekuwa akijibadilisha umbile lake mbele ya mhusika Prof. Mabadiliko haya yanaakisi namna wakoloni wanavyotumia mbinu mbali mbali ili kuendelea kunyonya na kukandamiza bara la Afrika.

Kwa kurejelea nadharia ya Fasihi linganishi ambayo imetoa fursa kwa mtafiti ya kutambua tofauti zilizopo katika Tamthiliya hizo kwa kuzingatia misingi ya matumizi ya mitindo mbalimbali na jinsi ilivyojitokeza na kutofautika katika tamthiliya teule ya *Mashetani* na *Mashetani* Wamerudi.

### 4.6.2 Kufanana kwa Dhamira katika Tamthiliya Teule

Data za utafiti huu zinaonesha kuwa wasanii wa Tamthiliya ya *Mashetani* na *Mashetani Wamerudi* wamefanana katika kujadili dhamira zinazohusu jamii za Kiafrika hasa baada ya nchi hizi kupata uhuru wa bendera kutoka kwa wakoloni. Hivyo basi Tamthiliya teule zimefanana katika kujadili dhamira kama zinavyooneshwa katika Jadwali Na. 4.16.

**Jedweli Na. 4.16: Kufanana kwa Dhamira katika Mashetani na Mashetani Wamerudi**

| Na. | **Dhamira katika *Mashetani*** | **Dhamira katika *Mashetani Wamerudi*** |
|---|---|---|
| 1. | Matabaka | Matabaka |
| 2. | Ubadhirifu wa mali za uma | Ubadhirifu wa mali za uma |
| 3. | Ujenzi wa jamii mpya | Ujenzi wa jamii mpya |
| 4. | Nafasi ya mwanamke | Nafasi ya mwanamke |
| 5. | Uongozi mbaya | Uongozi mbaya |
| 6. | Ukosefu wa demokrasia | Ukosefu wa demokrasia |
| 7. | Elimu ya Kimagharibi | Elimu ya Kimagharibi |
| 8. | Ukoloni mamboleo | Ukoloni mamboleo |

Chanzo: Data kutoka katika Tamthiliya teule Julai, 2017

Data za hapo juu katika jadwali namba 16 zinaonesha kuwa Tamthiliya ya *Mashetani* na *Mashetani Wamerudi* zinalingana kidhamira. Dhamira zilizofanana katika Tamthiliya teule ni ukoloni mamboleo, harakati za ukombozi, ujenzi wa jamii mpya, matabaka, nafasi ya mwanamke, uongozi mbaya, matumizi mabaya ya madaraka. Kufanana huko kunakohusiana na dhamira kumefanyiwa uchambuzi kama ifuatavyo:

#### 4.6.2.1 Matabaka

Matabaka ni tofauti iliyopo baina ya kundi moja na kundi jingine tofauti hizi zinaweza kuwa za kisiasa, kiuchumi, kiutawala na kijamii (Wamitila, 2003). Waandishi teule wanafanana katika uibuaji wa matabaka ambapo wote wanaonesha matabaka yaliyopo katika jamii. Tabaka la wakoloni na tabaka la watawaliwa. Kwa mfano, katika *Mashetani Wamerudi* matabaka yanajitokeza baina ya wanajamii. Msanii anonesha kuwa ingawa nchi za Afrika zimepata uhuru bado zinakumbwa na tatizo la kiutabaka ambapo watu hawajawa wamoja. Kwa mfano, msanii anasema:

> *"Prof: Ubaya ni kwamba tumegawika kimakabila. Pia tumegawika mno kimatabaka, kiuchumi, kisiasa na kidini. Mpaka sasa hatujali sana nchi yetu.Tunajali nafsi zetu na familia zetu na marafiki zetu na makabila yetu" (uk. 64).*

Katika maelezo ya hapo juu msanii anaonesha namna Wafrika walivyokumbwa na tatizo la utabaka. Jambo ambalo linawapelekea kutokuwa na umoja. Matabaka ya kijamii yanaelezwa kuwa yanasababishwa na ubinafsi, maswala ya kiuchumi yaani kati ya wenye nacho na walalahoi, dini na maswala ya kikabila. Mambo yote haya ndiyo yanayowafanya Wafrika wasiwe na umoja.

Pia, katika Tamthiliya ya *Mashetani*, mwandishi ameonesha matabaka yaliyoko katika jamii. Matabaka yanayozungumziwa katika Tamthiliya hii ni ule utofauti wa kiuchumi ambao umesababisha kufarakana kwa Juma na Kitaru. Urafiki wao uligeuka kuwa ni wa chuki. Vile vile, msanii anaelezea hali ya utabaka kati ya Waafrika na Wakoloni ambapo wakoloni wananyonya na kukandamiza Wafrika. Kwa mfano, mwandishi anasema:

> *"Juma: Mpanda ngazi na mshuka ngazi hawawezi kushikana mikono*
>
> *Kitaru: Pili?*
>
> *Juma : Wewe unaishi leo mimi ninaishi jana.Tutakuwaje marafiki? Na kila leo yako ni kidato cha kesho yako" (uk.36)*

Kwa kuhusisha na nadharia ya fasihi linganishi na mwingiliano matini, mtafiti amebaini kuwa maelezo ya hapo juu yanaonesha namna jamii ilivyokumbwa na suala la kiutabaka. Wale ambao walishika hatamu ya uongozi kabla ya uhuru waligeuka kuwa mahasimu. Salem (2013), anasema kuwa Juma anawakilisha tabaka tawala lililoshika hatamu za uongozi kabla ya mapinduzi ya Zanzibar na Kitaru

anawakilisha tabaka lililoshika hatamu mara tu baada ya Mapinduzi ya Zanzibar. Matabaka haya yalianza kuwa hasimu hasa baada ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kutaifisha mali za wale ambao walikuwa katika madaraka kabla ya mapinduzi hayo ya Zanzibar.

#### 4.6.2.2 Ubadhirifu wa Mali za Umma

Mwandishi wa Tamthiliya ya *Mashetani* anaelezea jinsi jamii ilivyokosa uzalendo kwa nchi yao. Maadili ya uongozi yameporomoka. Wananchi wanajilimbikizia mali badala ya kufanya kazi kwa bidii kwa maslahi ya taifa. Kwa mfano, mwandishi anapoonesha Mtu 1 na Mtu2 walipokuwa wanazungumzia upotevu wa mali za umma. Tazama mfano ufuatao:

> *"MTU 1: Aaah, acha bwana we. Sasa unataka kuniambia nini? (Mlio wa gari inapita). Doo doo! Salale! Umeuona mdudu ule?*
>
> *MTU 2: Nini? Ile gari? Nimeiona. Aah, ataiuza kesho ile. We ngoja tu.*
>
> *MTU 1: Kwani we unamjua yule?*
>
> *MTU 2: Kwani we humjui?*
>
> *MTU 1: Hata.*
>
> *MTU 2: Jana hatukuwa wote pamoja, alipoakitusimulia Bwana Methew juu ya kufungwa kwa ile kampuni.*
>
> *MTU 1: Aah, aah! Ndiyo, ndiyo, ndiyo. Aha! Kwani huyu ndiye bwana mwenyewe?*
>
> *MTU 2: Pesa chungu nzima bwana zimepotea. Lakini ndiyo haijulikani kuwa zimeibiwa au zimepote katika mahisabu.*
>
> *MTU 1: Alaa. Kumbe ndiye huyu? Shetani kweli kweli. (uk.42-43).*

Katika maelezo hapo juu msanii anaonesha namna watumishi wengi leo hii walivyokosa uzalendo na kuweka mbele tamaa ya kujinufaisha binafsi bila ya kujali

athari zinazojitokeza kwa jami. Watu wamekuwa ni wabadhirifu na kwa hali hiyo huwa hawatosheki kwa kile wanachokipata. Watu kama hao wanawakilishwa na Bwana Methew.

Kwa upande wa Tamthiliya ya *Mashetani Wamerudi*, msanii anazungumizia suala la ubadhirifu wa mali za umma katika jamii za Kiafrika. Anapigia mfano mtu ambaye ana majumba sabini na tatu. Yote hii ni tamaa ambayo inapelekea watu kujilimbikizia mali za uma kwa manufaa yao binafi. Msanii anasema:

> *"Mnasemaje hadhira? Mnasemaje? Si mnajua majumba makubwa ya kifahari yanayojengwa na mtu mmoja? Majumba ya kiasi cha sabiini na tatu. Majumba makubwa aliyojenga mtu mmoja" (uk. 2).*

Katika maelezo ya hapo juu msanii anaakisi tabia za watumishi wengi waliokatika sehemu za mapato ya uma wanavyotumia nafasi zao kuhujumu uchumi wa nchi kwa kutumia mali za umma visivyo. Mfano wa gumzo kama hili la uhujumu uchumi kutokana na ubadhirifu wa mali za umma limebuliwa na mapambano makali yanayoendeshwa na raisi wa awamu ya tano wa Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania na hata kuwataka watumishi waliofanya ubadhirifu kurudisha mali za taifa mara moja kabla ya sheria kuchukua mkondo wake. Suala hili linaonekana kutendeka sana katika nchi nyingi katika bara la Afrika ambapo wale wanaopewa nafasi katika serikali na mashirika ya umma huitumia nafasi hii ili kudhulumu wengine. Watendaji kama hawa ni kipingamizi kikubwa cha maendeleo.

Tukirejelea nadharia ya Fasihi Linganishi na Mwingilianomatini tunaona kuwa kunauchotaji wa dhamira ya ubadhirifu wa mali za umma. Msanii wa Tamthiliya ya Mashetani na Wamerudi anaonekana akiathiriwa na msanii wa Tamthiliya ya

Mashetani Wamerudi kuhusiana na suala la ubadhirifu wa mali za umma baada ya uhuru.

#### 4.6.2.3 Ujenzi wa Jamii Mpya

Data za utafiti huu zinaonesha kuwa Tamthiliya ya *Mashetani* na *Mashetani Wamerudi* zinajadili suala la ujenzi wa jamii za Kiafrika. Nchi ambazo zinakumbwa na ukandamizaji na unyonyaji unaofanywa na wakoloni. Tamthila ya *Mashetani Wamerudi* inajadili mbinu ya ujenzi wa jamii mpya kwa watu kuungana na kuwa kitu kimoja ili kupambana na ukoloni mamboleo. Aidha, Tamthiliya hiyo inawataka watu wapewe elimu ili kujitambua na kupambana na mbinu za kikoloni. Profesa anasema:

> *"Tushikamane mtu kwa mtu. Kundi kwa kundi. Wananchi kwa wananchi. Nchi kwa nchi. Udhaifu umo katika kutawanyika. Umoja na mshikamano ni silaha zetu" (uk. 30)*

Kutokana na dondoo hiyo hapo juu msanii anaonesha kuwa ili kujenga jamii mpya na endelevu jamii hainabudi kushikamana pamoja kuanzia mtu mmoja mmoja, makundi na hata nchi na nchi. Hivyo, umoja huo ndio ambao utapelekea bara hili kuwa huru. Msanii anaitaka ile mifarakano ya kihistoria ya wanajamii watu waondokane nayo. Kutokana na hali hiyo, msanii anamtumia Mzee Kitarua akisema:

> *"Kwa sababu hiyo ndio maana mimi na Jumai tumekuja kukuhakikishia kwamba mfarakano baina yetu haupo tena. Mimi nimeshafunzwa na ulimwengu. Nimeshafahamu mfumo uliopo wa kujijazia mali, bila ya kujali wananchi wenzetu" (uk. 64)*

Kwa upande wa Tamthiliya ya *Mashetani* mwandishi anaonesha jinsi ukoloni mamboleo unavyorudisha nyuma ujenzi wa jamii mpya. Mwandishi anamtumia

Shetani kuashiria ukoloni mamboleo ambapo anaonesha umekuja kwa sura mpya tofauti na ulivyokuwa mwanzo.

Hivyo, jamii za Kiafrika hazina budi kupambana na ukoloni mamboleo ili kujenga ukombozi wa kweli. Pia, jamii hii inaonekana ikikumbwa ni tatizo la wazawa kujilimbikizia mali kwa maslahi yao binafsi. Msanii anaitumia familia ya Kitaru ambayo ilikuwa imejilimbikizia mali. Msanii anaakisi hali hiyo kwa kusema:

*MTU 1: Aaah, acha bwana we.  Sasa unataka kuniambia nini? (Mlio wa gari  inapita). Doo doo! Salale! Umeuona mdudu ule?*

*MTU 2: Nini? Ile gari? Nimeiona. Aah, ataiuza kesho ile. We ngoja tu.*

*MTU 1: Kwani we unamjua yule?*

*MTU 2: Kwani we humjui?*

*MTU 1: Hata.*

*MTU 2: Jana hatukuwa wote pamoja, alipo akitusimulia Bwana Methew juu ya kufungwa kwa ile kampuni.*

*MTU 1: Aah, aah! Ndiyo, ndiyo, ndiyo. Aha! Kwani huyu ndiye bwana mwenyewe?*

*MTU 2: Pesa chungu nzima bwana zimepotea. Lakini ndiyo  haijulikani kuwa zimeibiwa au zimepote katika mahisabu.*

*MTU 1: Alaa. Kumbe ndiye huyu? Shetani kweli kweli. (uk.42-43).*

Tukirejelea nadharia ya Fasihi Linganishi na Mwingilianomatini tunaona kuwa kunauchotaji wa dhamira ya ubadhirifu wa mali za umma. Msanii wa Tamthiliya ya Mashetani Wamerudi anaonekana akiathiriwa na msanii wa Tamthiliya ya Mashetani Wamerudi kuhusiana na suala la ujenzi wa jamii mpya baada ya uhuru.

#### 4.6.2.4 Nafasi ya Mwanamke

Katika Tamthiliya ya *Mashetani Wamerudi* mwanamke amechorwa kama kiumbe mwenye kupata elimu na kujitambua juu hali ilivyo katika jamii zetu. Mwanamke ameoneshwa kuwa msatari wa mbele katika harakati za ukombozi wa bara hili la Afrika. Katika kulijadili hili msanii anasema:

> *"Msichana:Tunapaswa tusome katika shule au chuo cha mateso yetu ya dunia…Lakini tuyaache hayo ya kwamba tumesoma shule au chuo gani. "Bora tuendelee kunyambua mbegu mbovu. Tuendelee kupambana na maana ya matatizo, ingawa matatizo ya nchi hii hayana upeo mdogo (uk.33).*

Mwandishi anadhihirisha wazi jinsi gani mwanamke alivyosimama kidete katika kufichua maovu katika nchi yake na jamii yake kwa ujumla. Hivyo anaona ndio njia ya pekee kupambana na matatizo yaliyopo na kuikumba jamii. Aidha kwa upande wake anaona matitizo ni mengi lakini ni vyema kuendelea kupambana nayo kwa nguvu zote ili kuleta mustakbali wa nchi hii.

Pia, msanii anaamuonesha mwanamke kuwa ni mwenye kutetea utamaduni wa mtu mweusi ambao leo hii utamaduni huo umekumbwa na wimbi la utandawazi ambalo linatokana na athari za kikoloni. Kupitia mhusika msichana msanii anamuonesha mhusika huyo kukubali kuwa ipo haja ya kuiga tamaduni za wengine lakini sikila utamaduni unafaa kuigwa. Msichana anasema:

> *"Msichana: Tazameni akina mama na akina baba. Tazameni vijana wenzangu wa kike kwa wakiume. Sote siku hizi tunaelekea kwenye wigo wa kupotoshwa. Kuiga si kubaya. Kusema kweli kila mtu huiga. Kila asilia hufuatiliza yafanywayo. Lakini tukubali kizuri na tukiache kibaya. Hasa utamaduni unaopeperushwa na vyombo vya mawasiliano ya tekinolojia za kisasa kwa jina la utandawazi. Tumezipoteza mila na desturi zetu nzuri. Wazazi hawawezi kuwatazama tena watoto wao na watoto hawajali mbele ya wazazi wao ishara za ngono (uk.36).*

Maelezo ya hapo juu yanadhihirisha wazi jinsi gani mwanamke anavyojali na kuwa mstari wa mbele katika kutetea mila, desturi na utamaduni wa kiafrika ili kulinda, kujali na kuendeleza maadili mema kwa lengo la kulinda na kuthamini uafrika ili kujikinga na mataizo yanayosababisha mmongonyoko wa maadili katika jamii zetu, jambo ambalo husababisha kufanya ngono zembe na hatimae kupelekea kupoteza nguvu kazi za hapo baadae. Kwa upande mwengine wazazi wanatakiwa kushiriki kikamilifu ili kuleta mustakbali nzuri wa watoto wao.

Kwa upande wa Tamthiliya ya *Mashetani*mwandishi ameonesha nafasi ya mwanamke kwa kumchora mwanamke huyo kama ni mzazi na mlezi na mwenye kuongoza familia na kutoa elimu kwa watoto. Mtu mwenye imani potofu za ushirikina na mtu mwenye kuwapenda watoto kupita kiasi ha hatimae kudhalilisha wengine. Kwa mfano, mama Kitaru anaonekana kuwa na imani za kishirikina pale mama huyu anapoamua kutumia dawa zakienyeji kwa ajili ya kumtibia mwanawe Kitaru na kuona kwamba dawa za kizungu ambazo amepewa na daktari wake haziponeshi. Mwandishi anayadhihirisha haya kwa kusema:

*Mama:Afadhali nitafute dawa za kienyeji basi.Imekuwa dawa za kizungu hazifai.. Sasa tufanyeje?*
*Baba: Aliyesema hazifai nani?*
*Mama:Sasa leo siku ya ngapi hii? Daktari anaingia akitoka wala hujambo YenyeweSiiyoni. Mtoto kakaa tu vilevile. Nimemsimulia binti Kalinge.Yeye anasema huu. Huu ni ugonjwa wa wasiwasi tu (uk 30).*

Mwandishi anaonesha jinsi gani mama Kitaru anavyoendeleza imani za ushirikina kwa kutoamini matibabu ya kisasa licha ya usimamizi wa daktari ambaye anaonekana kuwa na taaluma ya kutibu magojwa kitaalamu na ujuzi

zaidi. Mama huyu anawakilisha jamii ya wanawake wenye kuendeleza maswali ya kijadi.

Kwa upande mwengine Mama Juma anaonekana kuwa ni mzazi na mlezi ambaye anapenda mtoto wake akuwe katika maadili na malezi mazuri ya kuwasaidia wazazi wake ingawa mama huyu anapata upinzani mkubwa kwa bibi yake Juma. Msanii anayadhihirisha haya kama ifuatavyo:

*"Mama: Haya tazama kiburi hicho.Tumemsemesha kidogo, huyoo kachomoka.Maana yake sisi wapuuzi .*
*Bibi: Afadhali andoke. Ikisha kuwa hwishi kumsumbua ah, Afadhali aondoke. Mtoto asirudi nyumbani. Akirudi tu Kwe, kwe kwe, kwe, kwe, kwe. kwe. Hm pole Basitena.*
*Mama: kusema nitasema…mtoto kiburi kimempita kimo"( uk. 38).*

Kwa kupitia maelezoya hapo juu mwandishi anaonyesh jinsi mama huyu alivyokuwa mstari wa mbele ili kuleta mustakbali mwema wa malezi ya mtoto wake, Juma lakini anaonekana kukumbana na vikwazo kadhaa kutoka kwa bibi anapomkanya na kumuonya Juma dhidi ya matendo aliyokuwa akiyafanya.

Tukirejelea Nadharia ya Fasihi Linganishi na Nadharia ya Mwingilianomatini tunagundua kwamba suala la nafasi ya mwanamke linajadiliwa katika Tamthiliya teule. Hii inamaanisha kuwa kuwa msanii wa Tamthiliya ya *Mashetani Wamerudi* ameathiriwa na msanii wa Tamthiliya ya *Mashetani* katika kuzungumzia suala la mwanamke ili kuonesha umuhimu wakekatika jamii inayomzunguka.

#### 4.6.2.5 Uongozi Mbaya

Data zilizokusanywa kutoka Tamthiliya teule zinaonesha kwamba waandishi teule wanazungumzia juu ya uongozi mbaya katika jamii. Kwa Mfano katika Tamthiliya

ya *Mashetani* mwandishi anaonesha namna utawala mbaya unavyotumia nafasi waliyonayo katika kuhujumu na kufanya ubadhirifu wa mali za uma. Msanii anamtumia mhusika Baba Kitaru ambaye anatumia pesa za kampuni kwa manufaa yake binafsi. Baba Kitaru ananunua gari la kifahari kwa fedha za ubadhirifu. Msanii analieleza hili kwa kusema:

*MTU 1: Aaah, acha bwana we. Sasa unataka kuniambia nini? (Mlio*

*wa gari inapita). Doo doo! Salale! Umeuona mdudu ule?*

*MTU 2: Nini? Ile gari? Nimeiona. Aah, ataiuza kesho ile. We ngoja tu.*

*MTU 1: Kwani we unamjua yule?*

*MTU 2: Kwani we humjui?*

*MTU 1: Hata.*

*MTU 2: Jana hatukuwa wote pamoja, alipo akitusimulia Bwana*

*Methew juu ya kufungwa kwa ile kampuni.*

*MTU 1: Aah, aah! Ndiyo, ndiyo, ndiyo. Aha! Kwani huyu ndiye bwana*

*mwenyewe?*

*MTU 2: Pesa chungu nzima bwana zimepotea. Lakini ndiyo haijulikani*

*kuwa zimeibiwa au zimepote katika mahisabu.*

*MTU 1: Alaa. Kumbe ndiye huyu? Shetani kweli kweli. (uk.42-43).*

Pia, wakoloni wanaonekana ni viongozi wabaya wanaotumia mbinu mbali mbali ili kukandamiza nchi maskini. Matokeo ya uongozi mbaya wa kikoloni ni kukithiri kwa ukandamizaji na unyonyaji katika jamii. Kutokana na uongozi mbaya wa kikoloni nchi nyingi leo hii zimeingia katika machafuko na vita na hivyo kuchafuliwa kabisa. Msanii anasema:

"SHETANI: *unanijua mimi nani?*

*Mimi shetani*
*Uwezo wangu hauhifadhiki*
*Wema wangu hauhesabiki*
*Ubaya wangu hausemeki*
*Ninajenga*
*Ninabomboa*
*Nanadhalilisha nitakavyo" (uk. 1)*

Vile vile suala la uongozi mbaya limejitokeza katika Tamthiliya ya *Mashetani Wamerudi*. Mwandishi anaelezea jinsi viongozi walivyo wabinafsi. Viongozi wengi katika bara la wanaendeleza ubinafsi kwa kupenda kujinufaisha wao wenyewe kwa maslahi yao binafsi ili kujenga familia zao badala ya kushughulikia maendeleo ya taifa. Msanii ameyadhihirisha hayo kwa kumtumia mhusika Kijana 2 kwa anaposema:

Kjana2: *Na hilo ni tatizo jengine katika orodha ya matatizo – taitzo la mtu Kuipamba na kujitembeza:maprofesa, wataalamu, mabingwa,wadadisi,wawasomi na kadhalika.Tatizo si ukubwa au elimu yake mtu,bali ubinafsi ndani ya moyo wake mkakamavu na akili zetu zenye kutokota kichwani.(uk. 34).*

Hivyo mwandishi anawataka viongozi wa bara la Afrika walioshika hatamu baada ya ukoloni mkongwe kuacha kutumia nafasi uongozi na madaraka kuwanyanyasa walio chini kwa nia ya kufikia ukombozi wa kweli. Ukombozi ambao ulitarajiwa na wananchi kuzaa matunda bora.

Tukirejelea Nadharia ya Fasihi Linganishi na Nadharia ya Mwingilianomatini tunagundua kwamba suala la uongozi mbaya linajadiliwa katika Tamthiliya teule.

Hii inamaanisha kuwa kuwa msanii wa Tamthiliya ya *Mashetani Wamerudi* ameathiriwa na msanii wa Tamthiliya ya *Mahetani* katika kuzungumzia suala la uongozi mbaya na namna uongozi mbaya unavyoathiri jamii.Kwa hivyo wote wanakemea uongozi mbaya katika jamii zetu.

#### 4.6.2.7 Ukosefu wa Demokrasia

Data zilizokusanywa na mtafiti zilionesha kuwa Tamthiliya ya *Mashetani Wamerudi* inajadili juu ya suala la demokrasia katika jamii. Msanii anaonesha kuwa ili kujenga demokrasia ya kweli lazima sheria zinazotungwa bungeni ziwe ni shirikishi. Sheria hizo zishirikishe michango ya watu kutoka vyama tofauti tofauti. Kitendo cha kushirikisha chama kimoja tu katika kutunga sheria za nchi ni kasoro kubwa katika kujenga demokrasia ya kweli. Msanii anasema:

> *"Sheria hutungwa bungeni. Katika kutunga sheria bungeni kusiwe na nguvu za chama tawala tu, bali pia nguvu za upinzani. Huu ni mkusanyo wa mwanzo wa wananchi unaotakiwa kujenga maslahi ya nchi sio ya vyama vibovu" (uk. 26)*

Maelezo haya yanaonyesha kwamba katika kutunga sheria kuwe na ushirikishwaji wa vyama vyote ili viwe na maamuzi ya pamoja katika kutnga sheria za nchi na sio kuachiwa chama kimoja kupitisha sheria hizo ukitilia maanani huu ni mfumo wa vyama vingi.

Pia, katika kujadili suala la demokrasia ya kweli msanii anaitaka jamii itekeleze masuala ya kidemokrasia bila ya kujali suala la kiutabaka. Ushirikishaji wa maamuzi ya siwe katika tabaka tawala tu. Haki ya kusema kuhusu demokrasia ni haki ya kila mtu bila ya kujali hadhi wala kabila. Aidha, demokrasia haijikiti kwenye kupiga kura tu, hasa kwa tabaka la chini. Msanii anasema:

*"Taifa litajengwa kwa namna yako Prof. Kwa wakubwa na wadogo, kwa wanaojua kwa elimu zao za vitabu na pia wasiojua chochote kuhusu elimu za vitabu, lakini pia wanojua kwa utendaji wa mapambano ya maisha yao. Demokrasia si kupiga kura tu, bali ukubalifu wa ushirikiano wa ngazi za juu hadi chini. Lazima kila mtu awe na haki ya kushirikia katika midomo ya taifa…Demokrasia inakuja kutoka kwa watu wengi si wachache wanaotumia nguvu" (uk. 34-35).*

Maelezo ya hapo juu yanasisitiza kwamba demokrasia sio kupiga kura tu bali mambo mengine kama vile kushirikishwa kwa watu katika kutoa maamuzi.Vile vile, demokrasia inakuja kwa kushirikishwa kwa watu wengi sio kushiriki watu wachache wanaotumia nguvu na maslahi yao na sio maslahi ya taifa zima.

Aidha, katika Tamthiliya ya *Mashetani* msanii anaonesha ukiukwaji wa demokrasia katika jamii za Afrika baada ya kupata uhuru wa bendera. Mara tu baada ya Wafrika kushika hatamu za uongozi, tabaka lililokuwa katika hatamu za uongozi kabla yao walinyanganywa mali zao, ikiwamo mashamba ya mikarafu na nyumba. Hali hii ilisababisha mifarakano, chuki na uhasama miongoni mwa pande hizo mbili.

Msanii anatuonesha namna Kitaru na Juma walivyo na uhasama unaotokana na msingi huu wa ukiukwaji wa demokrasia. Msanii analidhihirisha kwa kumtumia baba Kitaru ambapo ana tueleza kuwa familia ya Juma inatokea Unguja na familia ya Kitaru inatokea Tanganyika. Wazazi wa Juma walikuwa na mashamba ya mikarafuu lakini baada ya mapinduzi ya Zanzibar serikali iliyachukuwa. Mwandishi anadhihirisha hili kwa kusema:

***Baba**: (Anajaribu kubadilisha mazungumzo) Rafiki yako Juma anatoka wapi?*

*Ninafahamu anatoka Unguja. Lakini wapi? sehemu gani? Wazee wake walikuwa Wanafanya nini huko?*

***Kitaru*** *:Wazee wake walikuwa na mashamba ya karafuu lakini baada ya mapinduzi serikali iliyachukuwa" (uk26).*

Mwandishi ametuonesha tukio la utaifishaji wa huko Zanzibar lilivyoingiza migogoro kati ya Juma na Kitaru. Kitendo hiki tunakiita kwamba ni ukiukwaji wa demokrasi kwani kilifanyika bila ya kuzingatia misingi ya haki na sheria. Tukio hili limeacha huzuni za kihistoria miongoni mwa wale walioathirika. Msanii anasema:

> *"…Ulikuwa na mangapi, licha ya mabenzi. Ulikuwa na mashamba madallbasari. Ulikuwa na watu chini yako. Haya yaliopita si basi tu, mwenyewe Mungu ndivyo alivyopenda-mali yetu kuchukuliwa na kugaiwa watu. Watu tu hivi hivi, watu wasiojua hata maana ya milki ni nini" (uk. 38).*

Katika maelezo ya hapo juu mwandishi anaonesha masikitiko waliyonayo wale walionyanganywa mali zao kama vile bibi yake Juma baada yamapinuzu ya Zanzibar ambapo serikali ilichukuwa mashamba yao na kupewa watu wengine. Jambo hili linaonekana kuzua chuki na mfarakano miongoni mwa marafiki hawa. Familia ya Juma ilibidi ihamie Dar es Salam na kuanza maisha upya kwa kuanzisha biashara ya kidua.

#### 4.6.2.8 Elimu ya Kimagharibi

Katika Tamthiliya ya Mashetani msanii anajadili elimu ya Kimagharibi. Msanii anaonesha kuwa elimu ya Kimagharibi imemuandaa Muafrika kutumikia Wakoloni huku akitarajia kupata mshahara mnonono. Msanii anawatumia Juma na Kitaru, vijana waliobahatika kupata elimu ya Kimagharibi katika ngazi ya Chuo Kikuu hata hivyo hawawezi kujikomboa. Msanii anasema:

> *"Juma: Sasa unaniambia nini. Hujaniambia kitu. Kweli inauma bwana. Ukweli…acha yote hayo. Ukweli bwana, digirii iankupa tonge ya wali na mchuzi, tena mchuzi wa kuku, badala ya ugali na maharage" (uk.17).*

Pia, katika Tamthiliya ya *Mashetani Wamerudi* msanii ameonesha kuwa elimu ya Kimagharibi haikuwa na nia ya kumsukuma Muafrika kujikomboa. Kijana 4 anaieleza elimu ya Kimagharibi kuwa ni elimu iliyojaa nadharia ambazo zimekuwa zikikaririwa tu. Elimu hiyo ndani ya bara la Afrika haikuwa na nia ya kujenga nchi hizi. Kwa hali hiyo hadi leo elimu hiyo haijaweza kumkomboa Muafrika kiuchumi. Vyuo vikuu vinavyofundisha uhandisi vipo Afrika lakini navyo havijawa na chachu ya ukombozi wa bara hili. Kwa mfano, msanii anasema:

> *"Kijana 4: .. Mimi ninataka kutoa dukuduku lililomoyoni. Kwanza ni elimu tuliyonayo nchini mwetu. Elimu hii tulirithi kutoka kwa Wakoloni. Bila shaka wakoloni hawakuwa na nia ya kutuelimisha sisi kwa ajili ya kupiga hatua na kwenda mbele katika nchi na maisha yetu. Elimu tuliyonayo sasa ni elimu inayotandazwa kwa wingi wa nadharia kuliko vitendo vinavyotumiwa kujenga na kutengeneza vifaa na mashine. Ingawa vyuo vikuu vyetu vinafundisha somo la uhandisi bado hatujaunganisha vitendo vinavyoweza kutupa mapato kwa kutumia mashine na vifaa mbali mbali…" (uk. 58-59).*

Katika maelezo ya hapo juu msanii anadhihirisha wazi kwamba elimu tulionayo ambayo tumeirithi kutoka kwa wakoloni ni dhahiri kwamba hawakuwa na lengo zuri kwa waafrika .Waliitoa elimu hiyo ili watu wabara hili waendelee kuwa wategemezi ili waweze kwanyonya na kuwakandamiza.

#### 4.6.2.9 Ukoloni Mamboleo

Data zilizokusanywa na mtafiti kutoka tamthili ya *Mashetani* zinaonesha kuwa Tamthiliya hiyo imejadili kwa kina juu ya tatizo la ukoloni mamboleo baada ya nchi za dunia ya tatu kupata uhuru wa bendera. Msanii anaonesha kuwa ukoloni umekuwa ukichukua sura mpya ndani ya bara hili la Afrika. Shetani ni mhusika wa kiishara anayeashiria ukoloni. Mhusika huyo anajigamba mbele ya Binadamu kuwa ana nguvu zisizo za kawaida. Pia, tunaoneshwa kuwa Shetani amekuwa

akijibadilisha mara anakuwa ndege, upepo nakadhalika. Taswira hii inaonesha mbinu za kikoloni kama vile za sera ya utandawazi na ubinafsishaji ambazo zimekuwa zikisimamiwa na wakoloni ili kundeleza unyonyaji. Shetani anasema:

*Shetani: Unanijua mimi nani?*

*Mimi Shetani.*
*Sio Jini wa Kuhani*
*Mimi Shetani*
*Uwezo wangu hauhifadhiki*
*Wema wangu hauhesabiki*
*Ubaya wangu hausemeki*
*Ninajenga*
*Ninabomoa*
*Ninatukuza*
*Ninadhalilisha nitakavyo*
*Mimi ni nguvu na nguvu ni mimi,*
*Mimi ni uwezo na uwezo ni mimi. (uk. 1-2)*

Aidha, katika Tamthiliya ya *Mashetani Wamerudi* msanii analielezea suala la ukoloni na kutuonesha kuwa wakoloni ingawa walionekana kama vile wameondoka kutokana na ukoloni mkongwe. Hata hivyo, ukweli ni kwamba wakoloni walikuwepo, na wakajifanya kama vile hawapo lakini sasa wamerudi. Wakoloni wamekuwa wakijidai kuwa hawako kama vile walivyokuwa hapo mwanzo lakini ukweli si hivyo. Kwa sasa hali ya unyonyaji unaofanywa na wakoloni katika bara hili imekuwa mbaya zaidi. Leo hii kila unapokwenda unakutana na athari za kikoloni. Kwa mfano, Prof. anasema:

> *"Msicheke ovyo ovyo, mkizani kwamba shetani amemaliza nguvu zake. Yupo hapa hapa. Yumo angani na ardhini . Yuko kule na hapa. Yuko kokote ingawa hayuko kokote. Lakini kwa macho hatumuoni mpaka sasa. Tuko dhaifu na tumeparaganyika" (uk. 29).*

Maelezo ya hapo juu inaonesha kuwa ukoloni umekita katika kila nyanja ya maisha ya Muafrika. Ingawa wakoloni hawaonekani kutawala moja kwa moja kama hapo

mwanzo hata hivyo wapo. Wakoloni wapo katika maswala ya mawasiliano, kilimo, madini utamaduni na hata katika siasa zetu. Hivyo, inatupasa tuwe makini ili kuondokana na ukoloni.

Tukirejelea nadharia ya Fasihi Linganishi na Nadharia ya Mwingilianomatini ambazo zinaongoza utafiti huu tunagundua kuwa Tamthiliya ya *Mashetani* na Tamthiliya ya *Mashetani* Wamerudi zinamuingiliano mkubwa katika kujadili suala la ukoloni mamboleo,elimu ya kimagharibi na Ukosefu wa demokrasi. Wasanii teule wanajadili ukoloni na namna ulivyojidhihirisha baada ya ukoloni mkongwe katika jamii zilizowahi kutawaliwa na wakoloni. Tamthiliya teule zinatumia ishara ya shetani kujadili ukoloni mamboleo na athari zake kwa nchi za dunia ya tatu.

Vile vile, Tamthiliya teule zinaingiliana katika dhamira za ubadhirifu wa mali za uma, uongozi mbaya, ukosefu wa demokrasia, kujadili elimu ya Kimagharibi, ujenzi wa jamii mpya na nafasi ya mwanamke. Kama anavoeleza Salem (2013), kwamba watunzi huweza kufanana kutokana na mazingira yao na sababu za kihistoria. Kwa hali hiyo ni wazi kwamba waandishi teule wamelingana kutokana na kutoka katika jamii zilizowahi kutawaliwa na wakoloni na baadae kuwa Taifa moja. Hivyo, matatizo wanayokumbana nayo yanafanana.

### 4.6.3 Kutofautiana kwa Dhamira katikaTamthiliya teule

Katika uchambuzi mtafiti alibainisha kuwa kuna dhamira ambazo zimejitokeza katika Tamthiliya ya *Mashetani Wamerudi* lakini hazikujitokeza katika Tamthiliya ya *Mashetani.* Dhamira hizo ni kama zinazojidhihirisha katika jadweli na.17.

**Jedweli Na. 4.17: Kutofautiana kwa Dhamira za *Mashetani* na *Mashetani Wamerudi***

| Na. | Dhamira | *Mashetani* | *Mashetani Wamerudi* |
|---|---|---|---|
| 1. | Kujitoa Mhanga | Haikujitokeza | Imejitokeza |
| 2. | Umoja na Mshikamano | Haikujitokeza | Imejitokeza |
| 3. | Utandawazi | Haikujitokeza | Imejitokeza |
| 4. | Ukosefu wa Ajira | Haikujitokeza | Imejitokeza |
| 5. | Rushwa ( ufisadi) | Haikujitokeza | Imejitokeza |

Chanzo: Data kutoka *Mashetani* na *Mashetani Wamerudi* Jualai, 2017

Data za utafiti zilionesha kuwa kuna tofauti ya dhamira zinazojidhihirisha katika Tamthiliya ya *Mashetani Wamerudi* na *Mashetani.* Tofauti hizo za kidhamira zinajikita kupitia dhamira za dhulma na uonevu, kujitoa mhanga, umoja na mshikamano, utandawazi, ulevi na rushwa. Data zinaonesha kuwa dhamira hizo hazikujitokeza katika Tamthiliya ya *Mashetani.* Dhamira hizo zimefanyiwa uchambuzi kama ifuatavyo:

### 4.6.3.1 Dhuluma na Uonevu

Katika Tamthiliya ya Mashetani Wamerudi msanii anajadili suala la dhulma na uonevu ambao wamekuwa wakifanyiwa watu wa tabaka la chini. Tabaka hili limekuwa likifanya kazi kwa bidii ili kujinasua na hali ngumu ya maisha. Hata hivyo juhudi zao zimekuwa zikififishwa na tabaka la wenye nacho ambalo limekuwa likiwadhulumu haki zao za msingi. Wakati dhulma na uonevu unapotendeka mara nyingi tabaka hili linajikuta likiwa njia panda kwa kukosa sehemu sahihi ya kukimbilia ili kutafuta haki yao. Msanii anaonesha kuwa hata wanapofika katika vyombo vya sheria kama vile mahakamani hakuna juhudi yoyote inayofanyika kwa nia ya kukinga haki yao. Msanii anadhihirisha hili kwa kumtumia Kijana 2 akisema:

> *"…Nikaanza kazi ya kuchimba mgodi wa almasi. Jambo nililolichukia hapo ni kupekuliwa mpaka kwenye viungo vya siri kwa kufikiriwa kwamba tunaiba almasi. Nilikuwa mgumu kukubali kupekuliwa. Siku moja walinikamata na kunipiga vibaya kwa kiasi cha kunifanya mlemavu. Sababu ikiwa nilikataa kupekuliwa. Nilienda mahakamani angalau nipewe fidia lakini wapi! Miaka mine kesi haikwisha. Hatimae niliambulia patupu" (uk. 37)*

Maelezo haya yanaonesha jinsi tabaka tawaliwa hususanan vijana wanavyojiajiri katika sekta zisizo rasmi ili kupambana na ugumu wa maisha. Hata hivyo, juhudi zao zinaonekana kupigwa vita kwa kufanyiwa vitendo visivyo vya haki.

#### 4.6.3.2 Kujitoa Mhanga

Msanii wa Tamthiliya ya *Mashetani Wamerudi* anaonesha kuwa ili tuweze kujenga jamii mpya endelevu hatuna budi ila kupambana na ukoloni mamboleo. Katika kufanikisha mapambano hayo lazima tujitoe mhanga. Msanii anamtumia mhusika Prof. akiwa msari wa mbele katika kupambana na ukoloni (shetani). Msanii anaonesha kuwa mapambano dhidi ya ukoloni ni safari ndefu ambayo inahitaji uvumilivu.

Aidha, tunapoamua kupambana kikweli na wakoloni katika bara nchi changa wengine wanaweza kupoteza maisha. Hata hivyo, ipo haja ya watu kuendelea na mapambano hayo. Prof. anasema:

> "Profesa: *miaka au karne tunanyamaza huku midomotunayo lakini si sote tunaonyamaza. Kwa vyovyote vile mimi sinyamazi nilisema zamani, ninasema sasa na kesho nitasema ndani na nje"*. (uk. 4).

Katika kuhakikisha mapambano ya ukoloni yanaendelea msanii anawataka watu waache woga na wasimame na nia ya ukombaozi wa mapambano dhidi ya ukoloni. Anasisitiza kwamba Wafrika wakati umefika wa kuondokana na woga juu ya

mapambano dhidi ya wakoloni. Popote pale walipo waendeshe mapambano dhidi ya ukoloni. Prof. anasema:

> "Profesa: *muda wote huo mimi nimesimama, siogopi kusimama kwani maisha ni matamu. Niogpe nini na Shekspia kasema: 'Ni ujinga kuogopa kifo, kwani kifo kitakuja tu, tutake tusitake" (uk. 17).*

Maelezo haya yanaonesha mhusika Prof. alivyojitolea mhanga katika kulinda na kuitetea nchi yake pamoja na vitendo na vitisho anavyofanyiwa na shetani. Anaonekana kuwa na msimamo na haogopi kufa. Kwa upande wake anaona kifo ni jambo la kawaida kwa kila mtu.

#### 4.6.3.3 Umoja na Mshikamano

Msanii katika Tamthiliya ya *Mashetani Wamerudi* anajadili suala la umoja na mshikamano katika jamii. Msanii anaona kwamba ukoloni umekuwa ukiathiri bara la Afrika kwa sababu bado hakujawa na umoja na mshikamano. Kwa hali hiyo Afrika inaendelea kunyonywa na kukandamizwa na wakoloni na vibaraka wake. Msanii anasema:

> ***"Prof:****tushikamane mtu kwa mtu. Kundi kwa kundi. Mwananchi kwa mwananhi. Nchi kwa nchi. Udhaifu umo katika kutawanyika. Umoja na mshikamano ndio silaha yetu" (uk 30).*

Aidha, msanii anaendelea kuhimiza umoja na mshikamano kwa kuwahimiza vijana kuzungumza ukweli popote watakapokuwa kama ni ndani au nje ya bara hili waweze na kushirikiana, kushikamana kwa pamoja ili kuleta uelewa miongoni mwa jamii kuhusu ukoloni mamboleo na athari zake katika nchi za dunia ya tatu. Kwani umoja na mshikamano ndio njia pekee itakayowawezesha kufikia katika ukombozi wa kweli. Kijana 1 anasema:

> *"Katika karne hii hatutaki tuendelee kuwa kinyesi cha mbuzi kinachotawanyika, tunataka tuwe sangara kwenye mlolongo wa pamoja. Kama hatutashikamana mikono na kwenda upande mmoja, basi sote tutanguka chini na kulamba mchanga" (uk. 62).*

Mwandishi anahimiza jamii kushirikana na kuwa kitu kimojail kuleta mapambambano ya kweli dhidi ya ukoloni mamboleo. Ameifananasha jamii na mlolongo wa sangara ili kujenga taswira ya kushiriana kwa pamoja katika kuleta mabadiliko katika jamii kwani umoja ni nguvu na utengano ni udhaifu. Anatumia taswira ya kinyesi cha mbuzi ambaco huwa hakiko pamoja ili kukemea suala la utabaka ambalo hupelekea kushinwa katika kupambana na ukoloni.

Msanii anawataka Wafrika waache tofauti zao za kijadi ambazo ziliwagawa. Wafrika waligawanyika na kutokana na kugawanyika huko kukatoa mwanya kwa wakoloni kuendeleza ukoloni mamboleo. Hivyo, kukakithiri unyonyaji na ukandamizaji. Msanii anamtumia Mzee Kitarua na Mzee Jumai ambao walikuwa mahasimu hapo zamani na sasa wamekubali kuondoa uhasama wao ili kujenga jamii mpya endelevu. Msanii anasema:

> *"Kwa sababu hiyo ndio maana mimi na Jumai, tumekuja kuhakikisha kwamba mfarakano baina yetu haupo tena. Mimi nimeshafunzwa na ulimwengu. Nimefahamu mfumo uliopo wa kujijazia mali bila ya kujali wananchi wenzetu"* (uk).

Katika maelezo ya hapo juu msanii anaonesha jinsi Mzee Kitarua na Mzee Jumai walivyoweza kuwa na uelewa kuhusu mambo yaliyopo katika jamii yao hivyo wameamua kuondoa tofauti zao na kuhakikishia Prof. kwamba watashirikiana kwa kila hali na tayari hali halisi ya mfumo uliopo. Hivyo wameona kwamba waachane na tabia ya kujijazia mali bila ya kujali wananchi wa tabaka la chini. Aidha,

wasahau tofauti zao walizokuwa nazo hapo awali na kushirikiana ili kuleta mabaliko.

#### 4.6.3.4 Athari za Utandawazi

Kwa mujibu wa Kamusi la Kiswahili Fasaha (BAKIZA (2010) linaeleza kwamba utandawazi niuhusianowa kimataifa wa kisiasa, kiuchumi na kiutamaduni usio na mpaka baina ya mataifa kutokana na urahisi wa mawasiliano uliosababishwa na teknolojia ya habari. Msanii katikaTamthiliya ya *Mashetani Wamerudi* anaonekana kuliogelea kwa mapana suala la utandawazi. Huu ni mfumo huria unaosukumwa na nguvu za teknolojia mpya ya mawasiliano na mfupisho wa wakati na biashara. Msanii anaona katika jamii zetu watu wengi wamesukumwa na wimbi kubwa la utandawazi hasa ikiwa ni pamoja na utamaduni. Suala la utandawazi limekumba rika mbali mbali za watu wakiwemo wazee, hirimu, vijana na watoto wa jinsia tofauti. Utandawazi umepelekea watu wetu kudharau utamaduni wao wa asili na kukumbatia utamaduni wa kigeni.

Aidha, imedhihirika kwamba sababu kubwa ya kuiga tamaduni za Kimagharibi inasukumwa na tamaa ya kupata pesa. Kwa hivyo, jamii hujiingiza katika vikundi viovu kama vile ulevi na uasharati. Pia watu wengine hujiingiza katika wizi. Kwa mfano, vijana wengi wanaonekana kutafuta pesa kwa njia ya mkato kama vile kutumia utandawazi wa mawasiliano ya simu na kuwaibia wengine. Dhulma na ufisadi pamoja na unyanganyi unaonekana kupindukia na kuvuka mipaka katika nchi zetu. Msanii ameyaeleza haya kwa kumtumia Kijana 5 akisema:

> **Kijana 5**: *Si wazee, si hirimu, si vijana, si watoto sote tumesukumwa na na wimbi la utandawazi katika eneo baya la utamaduni. Ni*

> *kweli kwamba utamaduni wetu una mabaya lakini una mazuri pia. Sisi tumeyakumbatia maovu ya utamaduni wa wenzetu. Na yote yanatokana na utandawazi ni mambo ambayo yanaharibu dunia kwa sababu za ibada pa pesa.Ulevi na uasharati umekithiri. Dhulma ndio mchezo wetu. wizi ufisadi na unyanganyi umesambaa" (uk59).*

Mwandishi anaonesha jinsi athari za utandawazi zinavyopelekeamaadili yetu kupotea. Wazee walitarajiwa wawaongoze vijana katikamaadili mema. Hata hivyo, wazee nao wametumbukia katika kungangania utamaduni wa Kimagharibi.

Kwa upande mwengine mwadishi anaitanabahisha jamii kwamba isiwe tayari kuiga kila kitu tunachokiona kutoka kwa wengine bali wachague jambo jema na waachane na lile ambalo halina faida. Utamaduni wetu unaopeperushwa na utandawazi kwani watu wengi wanaonekana kudharau zile mila nzuri za kiafrika na kuiga utamaduni kutoka nje ambao unaonekana kutokubalika katika bara la Afrika. Kwa upande wa wazee nao wanatakiwa kuwaelekeza watoto hasa wanapowaona na ishara za ngono. Msanii amemtumia msichana kuyaweka wazi hayo kama ifuatavyo:

> **"Msichana:** *Tazamani akina mama na akina baba.Tazameni vijana wenzangu wa kike na wakiume. Sote siku hizi tunaelekea kwenye wigo wa kupotoshwa. Kuiga si kubaya. Kusema kweli kila mtu huiga. Nchi huiga. Kila utamaduni huiga. Kila jamiihuiga. Kila asili hufuatiliza yafanywayo. Lakini tukubali kizuri na kukiacha kibaya. Hasa utamaduni unaopeperushwa na vyombo vya mawasiliano ya teknolojia za kisasa kwa jina la utandawazi. Tumepoteza mila na desturi zetu mzuri wazazi hawawezi kuwatazama tena watoto wao na watoto hawajali mbele ya wazazi wao ishara za ngono" (uk. 36).*

Msanii anaonesha namna msichana anavyoitaka jamii kuachana na tabia ya kuiga utamaduni kutoka nje na kudharau utamaduni wa Mwafrika. Jamii inatakiwa kuiga yale mazuri na kuachana na tamaduni mbaya. Pia, wanasisitizwa wazazi

wawaangalie sana watoto ili wasifuate tamaduniza Kimagharibi ambazo huwapoteza hambazo huwasukuma katika kufanya ngono.

#### 4.6.3.5 Ukosefu wa Ajira

Data zilizokusanywa kutoka katika Tamthiliya **ya** *Mashetani Wamerudi* zinaonesha kuwa Tamthiliya hiyo imejadili suala la ukosefu wa ajira katika jamii.Msaniii anaeleza kuwa vijana ndio wahanga wakubwa wa tatizo hili. Mhusika kijana 2 anatoa kilio kwa hadhira kutokana na tatizo la ajira nchini. Anaonesha kwamba serikali kwa sasa imekwama katika kutatua tatizo la ajira. Ajira zinazotegemewa zinatokana na serikali. Hata hivyo, kwa sasa ajira hizo zimedhibitiwa na wazee ambao wako mbioni kustaafu huku vijana wakibakia hawana ajira. Msanii analieleza hili kwa kusema:

> "***Kijana2:*** *Nasimama mbele yenu kutoa dukuduku langu kuhusu ukosefu wa ajira na Kazi kwa vijana. Kwanza nchi yetu haina mwenendo wa kuunda ajira na kazi. Na kusema kweli kazi ziliopo ni kazi za serikali ambazo zimedhibitiwa na wazee. Na watu wenye umri mkubwa" ( uk. 56).*

Kwa upande mwengine msanii anatueleza kwamba vijana vijana wanakumbwa na suala la kukatishwa masomo kwa kukoseshwa malipo ya chuo kutokana na sababu kadhaa ikiwemo za kisiasa. Kijana 1 anatueleza kwamba alikatishwa pesa ya kuendelea na masomo kwa kishingizio kisingizio cha kisiasa. Matokeo ya hali hiyo ni kukosa shahada. Halii hii ilimfanya ashindwe kupata ajira. Msanii analieleza hili kwa kusema:

> ***Kijana 1:****Karibu na kumalizia digirii yangu ya uzamili nimekoseshwa malipo ya chuo, kwa sababu eti mimi ni mchochezi, sasa nimo kutafuta kazi lakini kila pahala naambiwa sina shahada ya kutosha ( uk36-37*).

Maelezo ya hapo juu linaonesha namna masuala ya kisiasa yanavyochangia kurudisha nyuma maendeleo ya vijana. Pia, ukosefu wa ajira kimekuwa kilio kikubwa kwa vijana hata wale wale ambao wamebahatika kufika vyuo vikuu.

**4.6.3.6 Ufisadi (Rushwa)**

Suala la rushwa limekuwa likijadiliwa na limekuwa ni tatizo kubwa katika nchi za dunia ya tatu tangu tupate uhuru. Waafrika wamekabiliwa na tatizo la rushwa na hivyo ujenzi wa jamii mpya imekuwa ni ndoto. Ruswa imekuwa ikifanyika kutokana na tama ya kitu. Ubinafsi huu ndio unaopelekea kuchukua hata mali za uma kwa manufaa yao binafsi. Msanii analieleza hili kwa kusema:

> *Kijana3:Uchafu wa roho zetu zinatofautisha baina ya makundi ya wachache na wengi. Wachache wanaipakata na kufurahia nchi kwa sababu inawafaa kwa mapato na maslahi yao.Wengi wanaitemea mate na kuichukia nchi yetu kwa sababu haiwafai na kwa ukosefu wa mapato. Pande zote mbili hizi zinataja ovyo suali la "ufisadi", lakini hakuna hata mmoja anayesema wazi wazi au anayechukuwa hatua kali" (uk.35)*

Msanii anaonesha jinsi gani rushwa ilivyotawala miongoni mwa jamii zetu.Kuna wale wanaoifurahia kwa sababu wanafaidika kwa kipato wanachokipata na kuna wengi wanaoichukia kwa sababu hawafaidiki na chochote. Hata hivyo hakuna juhudi za maksudi zinazochukuliwa kwa nia ya kupambana na rushwa. Harakati zinazofanywa humalizikia katika midomo tu.

Tukirejelea Nadharia ya fasihi Linganishi ambayo ni moja kati ya nadharia inayoongoza utafiti huu mtafiti amegundua kwamba waandishi waTamthiliya hizi teule pamoja na kuingiliana kwa kiwango kikubwa hata hivyo kazi zao pia zina tofauti ndogo katika kuakisi dhamira. Sababu ya kwanza ambayo imemsukuma

mtafiti kueleza sababu ya tofauti hizi ni tofauti za wakati ambapo kazi hizo zilitungwa.

Tamthiliya ya *Mashetani* ilitungwa miaka ya 1970 wakati Tamthiliya ya *Mashetani Wamerudi* ilitungwa miaka ya 2016. Tofauti hizi zinajitokeza katika kuzungumzia maswala yaliyoikabili jamii leo hii. Mathalani, wakati Tamthiliya ya *Mashetani* inatungwa suala la utandawazi lilikuwa bado halijaukabili ulimwengu. Leo hii tatizo hili limeikumba jamii ndio maana tunakutana na mjadala wa utandawazi katika Tamthiliya ya *Mashetani Wamerudi.* Hivyo basi, utandawazi, ufisadi, muamko wa mwanamke wa Afrika, ukosefu wa ajira kwa vijana na umoja na mshikamano ni miongoni mwa upya anaoujadili Mohamed katika Tamthiliya ya *Mashetani Wamerudi.*

Sababu ya pili inayotusukuma kuona ulazima wa kuwapo tofauti kati ya Tamthiliya teule ni kwamba mtunzi yoyote kamwe hawezi kulingana na mtunzi mwengine katika kila kipengele. Dai hili limeungwa mkono na Jilala (2016), anaposema kuwa mtindo ni tabia ya mtu binafsi inayomtofautisha na mtu mwengine katika uzalishaji wa kazi za kisanaa. Sifa hii ni ya kipekee ambayo mtunzi huwa nayo na hata kama mtunzi mmoja anaiga au kuathiriwa na mtunzi asili. Hii ni kusema kwamba hata kama mtunzi mmoja aige mtunzi mwengine kamwe tofauti zitajitokeza.

## 4.7 Hitmisho

Sura hii imefanya uchambuzi, uwasilishaji na mjadala wa data zilizokusanywa na mtafiti kwa nia ya kujibu maswali ya utafiti huu. Katika sura hii kwanza mtafiti ameeleza usuli wa waandishi teule, (Ebrahim Hussein naSaid Ahmed Mohamed),

muhtasari wa Tamthiliya teule,*(Masheni* na *Mashetani Wamerudi*) kumebainishwa vipengele vya mtindo katika Tamthiliya teule na namna vipengele hivyo vinavyolingana na kutofautiana. Pia, sura hii imefanya uchambuzi juu ya dhamira zilizojitokeza katika Tamthiliya teule. Mtafiti alieleza kuwa waandishi wa Tamthiliya teule wamefanana na kutofautiana kidogo tu katika matumizi ya mtindo na dhamira.

# SURA YA TANO

# MUHTASARI, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO

## 5.1 Utangulizi

Sura hii ni sura ya mwisho ambayo inatoa muhtasari, hitimisho na mapendekezo ya utafiti huu. Sura hii imegawanyika katika sehemu kuu tatu ambazo ni; sehemu ya kwanza inahusu muhtasari, sehemu ya pili inahusu hitimisho la utafiti huu na sehemu ya tatu ni mapendekezo ya utafiti huu.

## 5.2 Muhtasari

Utafiti huu umechunguza matumizi ya mbinu za mtindo katika Tamthiliya za Kiswahili kwa kutumia mifano kutoka katika Tamthiliya ya *Mashetani* na Tamthiliya ya *Mashetani Wamerudi*. Utafiti huu ni utafiti linganishi. Tatizo lilikuwa kutathmini namna Tamthiliya teule zilivyofana na kutofautiana katika matumizi ya mitindo. Katika utafiti huu tulichunguza kazi mbili za wasanii tofauti wa kifasihi, mwandishi wa Tamthiliya ya *Mashetani* (E. Hussein)na *Mashetani Wamerudi* (S.Mohamed) ambao wanatofautiana katika mazingira ya utunzi ambapo E. Hussein anatokea Tanzania Bara na Said A. Mohamed anatokea Tanzania Visiwani.

Nia ya kufanya utafiti huu ilikuwa ni kuchunguza kama kazi hizo zina tofauti au kufanana kokote kunakotokana na tofauti za kijiografia, kitajriba, kihistoria, kimuktadha na kadhalika baina ya waandishi wake. Hivyo kutokana na maswali hayo, tatizo la utafiti huu ni kutaka kuchunguza na kulinganisha mitindo na dhamira katika Tamthiliya ya *Mashetani* na *Mashetani Wamerudi* ili kuona jinsi Tamthiliya hizo zinavyofanana na kutofautiana kimtindo na dhamira. Lengo kuu la utafiti huu

lilikuwa ni kutathmini matumizi ya mtindo na dhamira katika Tamthiliya za *Mashetani* na *MashetaniWamerudi.*Utafiti huu una malengo mahsusi matatu ambayo ni; Kubainisha matumizi ya mitindo katika Tamthiliya za *Mashetani na Mashetani Wamerudi*, Kulinganisha na kulinganua matumizi ya mitindo katika Tamthiliya ya *Mashetani* na *Mashetani Wamerudi*, Kuchambua kwa kulinganisha dhamira zinazojitokeza katika Tamthiliya za *Mashetani* na *Mashetani Wamerudi.* Malengo haya yaliongozwa na maswali ya utafiti kama ifuatavyo:

Ni mitindo gani iliyotumika katika tamthiya teule za *Mashetani* na *Mashetani Wamerudi*? Ni jinsi gani mitindo inafanana na kutofautiana katika Tamthiliya za *Mashetani* na *Mashetani Wamerudi*? na Ni dhamira zipi zinazolingana katika tamthiya teule za *Mashetani* na *Mashetani Wamerudi*?

Umuhimu wa utafiti huu umejikita katika nyanja kuu tatu; kwanza, utafiti huu utaongeza maarifa katika nadharia na mbinu za utunzi wa Tamthiliya hususani Tamthiliya za Kiswahili ili kujenga uzoefu wa kuitumia Tamthiliya kama kazi ya fasihi inayojenga dhamira mbalimbali katika jamii. Kwa kubainisha na kulinganisha matumizi ya mtindo iliyotumika katika Tamthiliya ya *Mashetani* na *Mashetani Wamerudi* tutaweza kuona ni jinsi gani wasanii hao wanahusiana na kufanana na kutofautiana katika matumizi ya mtindo na uebuaji wa dhamira.

Pili, utatumika katika taaluma ya fasihi, hususani Tamthiliya. Hivyo, utafiti huu utatumika kama marejeo na kwa maana hiyo utawasaidia wanafunzi na watafiti wengine kupata marejeo kuhusu Tamthiliya ya Kiswahili na Tamthiliya kwa ujumla wake.

Vile vile, utafiti huu utakuwa ni changamoto kwa watafiti wengine kutupia jicho katika Tamthiliya za Kiswahili. Hivyo basi, utafiti huu utawapa changamoto watafiti wengine waweze kuchunguza na kulinganisha kazi zingine za fasihi ili kuona jinsi gani zinafanana na kutofautiana.

Mipaka ya utafiti huu ilijikita katika kulinganisha matumizi ya mtindo na dhamira katika Tamthiliya teuele. Kwa kuwa si lengo letu kuchunguza Tamthiliya nyenginezo, hivyo utafiti huu ulichunguza na kulinganisha kazi moja ya Tamthiliya ya kila mwandishi yaani *Mashetani* na *Mashetani Wamerudi*. Kwa maana hiyo, kazi zingine za fasihi za waandishi teule hatukuzishughulikia. Vile vile, kazi zingine za Tamthiliya tofauti na hizi zilizotajwa hazikuhusishwa katika utafiti huu bali ziliweza kurejelewa hapa na pale kwa lengo la kiufafanuzi na kiulinganishi.

Hivyo basi, utafiti huu ni utafiti linganishi unaolinganisha kazi mbili za Tamthiliya; Tamthiliya ya *Mashetani* na Tamthiliya ya *Mashetani Wamerudi*. Katika kulinganisha Tamthiliya hizi utafiti huu uliongozwa na Nadharia ya Fasihi Linganishi na Nadharia ya Muingiliano Matini ili kuibua mitindo na dhamira ambazo zinawafananisha na kuwatofautisha wasanii wa Tamthiliya teule.

### 5.2.1 Dhumuni Mahususi la Kwanza

Dhumuni mahususi la kwanza lilikuwa ni "Kubainisha matumizi ya mbinu za kimtindo zilizotumika katika Tamthiliya ya Mashetani na Mashetani Wamerudi." Dhumuni hili liliongozwa na swali la utafiti lisemalo "Ni mitindo gani imetumika katika tamthila Mashetani na Mashetani Wamerudi? Matokeo ya utafiti yalionesha kuwa Tamthiliya teule zimetumia vipengele vya kimtindo kama ifuatavyo:

Utafiti uligundua kuwa Tamthiliya ya Mashetani imetumia vipengele vya kimtindo vinavyohusiana na matumizi ya lugha kama vile; uteuzi wa msamiati, matumizi ya jazanda, mpangilio wa maneno, tamathali za semi, misemo, nahau, methali, mdokezo, mchanganyondimi, nidaa, tashibiha, sitiari, tashihisi, takiriri, taswira, majazi, ishara, mubalagha, tanakalisauti na kejeli.

Mbinu nyenigine za kimtindo zilizotumika katika Tamthiliya ya Mashetani ni; mandhari za fasihi simulizi, mtindo wa kishairi, mtindo wa nyimbo, mtindo wa masimulizi, matumizi ya nafsi zote tatu, mtindo wa majigambo, matumizi ya dayalojia na mtindo wa Tamthiliya za majaribio.

Mathalani, Tamthiliya ya Mashetani imetumia mtindo wa mhusika shetani ambaye ni mhusika anayeashiria ukoloni mamboleo katika bara la Afrika. Mhusika huyu anaoneshwa namna anavyoathiri bara hili na kujitapa kuwa yeye hashindiki. Kutokana na uwezo alionao ndio maana amekuwa akizivuta na kuzilazimisha nchi za dunia ya tatu katika kutekeleza matakwa ya kikoloni.

Tamthiliya ya Mashetani Wamerudi imetumia mitindo inayohusiana na matumizi ya lugha kama vile; uteuzi wa msamiati, matumizi ya jazanda, ishara, tamathali za semi, misemo, nahau, methali, mdokezo, mchanganyondimi, matumiazi ya ishara, tashibiha, sitiari, tashihisi, takiriri, majazi, ishara, mubalagha, tanakali sauti, kweli kinzani, karaha na mjalizo.

Mitindo mengine iliyotumika katika Mashetani Wamerudi ni pamoja na mtindo wa nyimbo, mtindo wa ndoto, mtindo wa masimulizi, mtindo wa matumizi ya nafsi,

mtindo wa wahusika wa fasihi simuli, mtindo wa mandhari ya fasihi simulizi, mtindo wa majigambo na mtindo wa Tamthiliya za majaribio.

### 5.2.2 Dhumuni Mahususi la Pili

Dhumuni mahususi la pili la utafiti huu lilikuwa ni “Kulinganisha na kulinganua matumizi ya mbinu za kimtindo zilizotumika katika Tamthiliya ya Mashetani na Mashetani Wamerudi.” Lengo hili liliongozwa na swali la utafiti lisemalo “Ni mbinu zipi za kimtindo zilizolingana na kutoafautiana katika Tamthiliya ya Mashetani na Mashetani Wamerudi? Utafiti uligundua kuwa, Tamthiliya teule zinafanana kwa kiasi kikubwa na kutofautiana kwa kiwango kidogo tu katika matumizi ya mbinu za kimtindo. Hivyo, Tamthiliya hizi zimefanana katika vipengele vya mtindo vifuatavyo:

Kwanza, Tamthiliya zote zimetumia taswira ya mhusika shetani yaani mhusika wa fasihi simulizi katika kuakisi dhamira ya ukoloni katika bara la Afrika. Kwa mfano, katika Tamthiliya ya Mashetani msanii anatumia mhusika shetani ambaye anapambana na binadamu ili kumdhofisha na kuonesha nguvu zake alizonazo. Kitaswira mhusika huyu anawakilisha ukoloni mamboleo. Pia, katika Tamthiliya ya Mashetani Wamerudi mtunzi anatumia mhusika shetani ili kuwakilisha dhana hiyo hiyo ya ukoloni.

Vile vile, Tamthiliya zote teule zinatumia mandhari ya fasihi simulizi ya kwenye mbuyu ili kuonesha kikale cha Afrika. Mandhari haya ndiyo yanayotumika katika Tamthiliya ya Mashetani ambako mchezo kati ya shetani na binadamu unaigizwa. Aidha, mandhari ya kwenye mbuyu yanatumiwa na msanii wa Tamthiliya ya

Mashetani Wamerudi ambapo mkutano wa Prof. na vijana unafanyika. Mkutano huo ulikuwa na nia ya kufanya ukombozi dhidi ya ukoloni.

Aidha, utafiti umegundua kuwa wasanii wote wa Tamthiliya teule wametumia mbinu ya majigambo katika kujenga dhamira zao. Tamthiliya ya Mashetani inatumia majigambo ambayo yamekuwa yakitambwa na mhusika shetani mbele ya binadamu. Majigambo haya yanamaanisha uwezo walionao wakoloni. Pia, Tamthiliya ya Mashetani Wamerudi imetumia majigambo yanayotambwa na mhusika sheta akimaanisha nguvu za kikoloni.Tamthiliya zote zimetumia mtindo wa nyimbo. Mtindo huu umetumika kwa kiwango kikubwa. Mathalani, Tamthiliya ya Mashetani Wamerudi imekuwa ikitumia mtindo wa nyimbo mwanzoni mwa kila onesho. Pia, Tamthiliya ya Mashetani imetumia nyimbo katika kuwasilisha dhamira zake.Tamthiliya zote teule zimetumia mtindo wa uchaguzi wa misamiati maalumu. Kwa mfano, Tamthiliya zote zimetumia maneno kama vile shetani likiashira ukoloni, waltz likiashiria Waafrika kufuata mkumbo kutokana na sera za kikoloni, kisu likiashiria harakati za ukombozi, prof. likiashiria muamko wa Waafrika dhidi ya ukoloni.

Utafiti umegundua kuwa tamthiliz zote teule zimefuata mtindo wa tamthila za majaribio kutokana na kuwa na sifa za kuchota vipengele vya fasihi simulizi ya Afrika na kuviingiza katika fasihi andishi. Tamthiliya ya Mashetani imetumia mhusika shetani ambaye ni mhusika tunayekutana naye katika fasihi simulizi za Kiafrika. Pia, Tamthiliya hii imetumia nyimbo, majigambo na mandhari ya kwenye mbuyu pamoja na minazi. Mitindo hii pia inajitokeza katika Tamthiliya ya Mashetani Wamerudi.

KimsingiTamthiliya teule zina mwingilianomatini wa matumizi ya mitindo ya kiishara, kitaswira, kishairi, sitiari, tashibiha, takiriri, uchanganyaji wa lugha, kejeli na usimulizi. Mitindo hii imechukuliwa moja kwa moja kama mwandishi wa Tamthiliya ya Mashetanialivyoisanii katika Tamthiliya ya Mashetani na kuingizwa katika Tamthiliya ya Mashetani Wamerudi ama imepokea tofauti ndogo ndogo sana za kisani.

Kuhusu tofauti za kimtindo zinazojitokeza katika Tamthiliya teule utafiti umegundua kuwa Tamthiliya ya Mashetani inatofautiana katika matumizi ya taswira ambapo Mashetani Wamerudi imetumi taswira ya jogoo, simba, punda, shetani, kuku, chozi, tembo na batamzinga. Wakati Mashetani imetumia taswira ya manyoya, kisu na binadamu.

### 5.2.3 Dhumuni Mahususi la Tatu

Dhumuni mahsusi la tatu lilikuwa ni Kulinganisha na kulinganua dhamira zilizojitokeza katika Tamthiliya ya *Mashetani* na *Mashetani Wamerudi*. Dhumuni hili liliongozwa na swali la utafiti lisemalo *"Ni dhamira zipi zimelingana na kutofautiana katika Tamthiliya ya Mashetani na Mashetani Wamerudi?* Matokeo ya utafiti huu yalionesha kama ifuatavyo:

Tamthiliya ya *Mashetani* na *Mashetani Wamerudi* zimelingana kidhamira kwani waandishi teule wanajadili dhamira za matabaka, ubadhirifu wa mali za umma, ujenzi wa jamii mpya, nafasi ya mwanamke, uongozi mbaya, ukosefu wa demokrasia, elimu ya Kimagharibi na ukoloni mamboleo. Kimsingi, dhamira ziliomo katika Tamthiliya ya *Mashetani* zinajitokeza katika Tamthiliya ya *Mashetani*

*Wamerudi*. Hata hivyo, Tamthiliya ya *Mashetani Wamerudi* inadhamira kama vile; kujitoa mhanga, umoja na mshikamano, utandawazi, na rushwa ambazo hazikujitokeza katika Tamthiliya ya *Mashetani.* Kujitokeza kwa dhamira hizi katika Tamthiliya ya *Mashetani Wamerudi* kunatokana na usasa wa Tamthiliya hiyo ambapo imekuwa ikiakisi bara la Afrika leo hii.

### 5.2.4 Ufafafu wa Nadharia

Utafiti huu uliongozwa na Nadharia ya Fasihi Linganishi na Nadharia ya Mwingilianomatini. Nadharia hizi zimefaa sana katika uchambuzi wa kazi hii. Kwa upande wa Nadharia ya Fasihi Linganishi tunasema kuwa inafaa kwa sababu kuna vipengele vingi mno vya kimtindo na dhamira ambavyo vinalingana katika Tamthiliya hizi.Pia, Nadharia ya Mwingilianomatini ianaonekana kufaa sana kutokana na mlingano wa kimatini uliomo katika kazi teule.

## 5.3 Hitimisho

Utafiti huu ulilenga kutafiti, kukusanya na kuchambua data zinazohusiana na matumizi ya mitindo na dhamira katika Tamthiliya ya *Mashetani* na *Mashetani Wamerudi.*Tamthiliya ya *Mashetani Wamerudi* ni Tamthiliya ya kisasa iliyokuja kuipa Tamthiliya ya Mashetani usasa. Kama asemavyo mtunzi wa Tamthiliya hii katika dibaji ya Tamthiliya ya *Mashetani Wamerudi* kuwa, Tamthiliya ya *Mashetani Wamerudi* ni umbo jipya linalotokana na Tamthiliya ya *Mashetani* ya E. Hussen (Mohamed, 2016).

Matokeo ya utafiti huu yamethibitisha kuwa tamtilia ya *Mashetan*i na*WamerudiMashetani* zimetumia mitindo na dhamira zinazolingana. Vipengele vya

kimtindo kama vile matumizi ya mhusika shetani, mandhari ya kwenye mbuyu, matumizi ya nyimbo, majigambo ya shetani na matumizi ya masimulizi, ishara na taswira yanajitokeza kwa mtindo wa kimuingilianomatini katika Tamthiliya teule.Pia, dhamira kama vile; ukoloni mamboleo, elimu ya Kimagharibi, ukosefu wa demokrasia, uongozi mbaya, ujenzi wa jamii mpya, ubadhirifu wa mali za umma na nafasi ya mwanamke zinajadiliwa kwa kina katika Tamthiliya hizo.

Muachano wa muingiliano matini katika Tamthiliya ya *Mashetani* na *Mashetani Wamerudi* ni mdogo. Mathalani, Mashetani inajitofautisha kimtindo kwa kutumia mbinu ya mchezo ndani ya mchezo na taswira ya manyoya, ambapo mbinu hizi hatuzioni katika Tamthiliya ya *Mashetani Wamerudi.* Kwa upande wa Tamthiliya ya *Mashetani Wamerudi* inatumia taswira kama vile; jogoo, simba, punda, shetani, kuku, chozi, tembo na batamzinga na dhamira kama vile; kujitoa mhanga, umoja na mshikamano, utandawazi na rushwa.

## 5.4 Mapendekezo

Utafiti huu ulichunguza Matumizi ya kimtindo na dhamira katika Tamthiliya ya *Mashetan*i na *Mashetani Wamerudi*. Mtafiti anaamini kwamba ametowa msingi imara kwa wahakiki na wasomi wa fasihi. Hata hivyo anapendekeza yafuatayo:

### 5.4.1 Kwa Watafiti

Watafiti wengine wanaweza kufanya tafiti zaidi kuhusiana na Tamthiliya za *Mashetani* na *Mashetani Wamerudi.* Tafiti hizo zinaweza kuwa katika vipengele vyengine vya fani na maudhui.

### 5.4.2 Kwa Serikali

Serikali za Afrika ziwe makini juu ya mbinu chafu zinazofanywa na wakoloni wakishirikiana na vibaraka wao kwa nia ya kukandamiza nchi changa kama ambavyo mtafiti alivyobaini alivyobainisha na kuchambua katika Tamthiliya teule kupitia utafiti huu.

# MAREJELEO


Adam, J., & Kamuzora, F. (2008). *Research Methods for Business and Social Studies.* Morogoro: Mzumbe Book Project.

Babbie, E. (1999). *The Basics of Social Research*. Belmont: Wadsworth Publishing Company.

BAKIZA ,(2010). *Baraza la Kiswahili Zanzibar* Nairob: Oxford University Press.

Bassnett, S. (1993). *Comparative Literature: A Critical Introduction.* Oxford: Blackwell.

Cohen, L. (2000). *Research Methods in Education (5th ed).* London: Routledge

Cooper, R. L. (1989). *Language Planningand Social Change.* Cambridge: Cambridge: University Press.

Cresswell, J. W. (2009). *Research Design: Qualitative, Quantitative, and Mixed Methods Approaches.* Los Angeles: SAGE Publications.

Crystal, D., & Davy, D. (1967). *Investigating English Style.* Longmans: Green and Co Limited.

Enkvist, N. E. (1973). *Linguistics Stylistics.* The Hague: Mouton

Enon, J. C. (1998), *Education Research Statistics and Measurement.* Kampala: Makerere University.

Fakih, S. J. (2017). Kutathmini Mabadiliko ya Usawiri waMwanamke katika Riwaya ya Utengano na Kamwe si MbaliTena: Tasnifu ya shahada ya uzamili Chuo Kikuu Huria chaTanzania. *(*Hakijachapishwa). Dar es Salaam, Tanzania.

Flick, U. (2011). *Introducing Reseach Methods.* London: Sage Publication Ltd.

Furlong, N., & Lavelace, K. (2000). *Research Methods and Statistics: An Intergrated Approach.*New York: Hartcourt Colledge Publishers

Haji, A. A. (1982). *Misingi ya Nadharia ya Fasihi*. Sweden: Berlings, Arlov.

Hucker, H. (2011). *Reseach Methods in Health Care and Early Age.* London: Heineman Educationed Publication.

Hussein, E. (1969). *Kinjeketile.* Nairobi: Oxford University Press.

Hussein, E. (1971). *Mashetani.* Nairobi: Oxford University Press.

Jilala, H. (2016). *Misingi ya Fasihi Linganishi: Nadharia, Mbinu na Matumizi*. Dar es Salaam: Daudi Publishing Company

Jilala, H. (2003). *Giza*. Dar es Salaam: Angaza Initiative Cooparation Ltd.

Kombo, D. K. and Tromp, D. L. A. (2006). *Proposal and Thesis Writing*: Nairobi: Pauliness.

Kothari, C. K. (1990). *Research Methods: Methods and Techniques*. New Delhi: Publications.

Kothari, C. K. (2008). *Research Methodology: Methods and Techniques.* New Delhi: New Age International Publishing Ltd

Kothari, C. K. (2004). *Research Methodology: Methods and Techniques.* New Delhi: New Age International Publishing Ltd

Madumulla, J. S. (2009). *Riwaya ya Kiswahili: Nadharia Historia na Misingi ya Uchambuzi.* Nairobi: Phoenix Publishers Limited

Marrian, S.B. (1998). *Qualitative Research and Case Study Applications in Educations Reverised and Expanded from Case Study Research in Education*. San Francisco: Jossey-Bass Publishers.

Mbogo, E. (1980). *Ngoma ya Ng'wanamalundi.* Dar es Salaam: Tanzania PublishingHouse.

Mbogo, E.(2009). *Fumo Liongo*. Dar es Salaam: Dar es Salaam University Press.

Mbogo, E. (1993). *Morani*. Nairobi: Oxford University Press.

Mlama.P.O. (2003). *Utunzi wa Tamthiliya Katika Mazingira ya Tanzania*. Katika Makala za Semina ya Kimataifa ya Waandishi wa Kiswahili 111 FASIHI. TUKI: Dar es Salam.

Mohamed, S. A. (1980). *Kivuli Kinaishi*. London: Oxford University Press.

Mohamed, S. A. (2016). *Mashetani Wamerudi*. Mombasa:Ramco Printing Works Ltd

Mningo, R.A. (2015). Mwingiliano matini katika Utunzi wa Emanuel Mbogo: Utafiti Linganishi wa Tamthiliya ya Ngoma ya Ng`wanamalundi na Fumo Liongo. Tasnifu ya Shahada ya Uzamili Katika Kiswahili, Chuo Kikuu Huria cha Tanzania (Haijachapishwa). Dar es Salaam, Tanzania.

Mosoti, Z. M. (1993). Maudhui katika Tamthiliya nne za Emmanuel Mbogo: Tasnifu ya M.A. Chuo Kikuu Cha Nairobi (Haijaschapishwa). Nairobi, Kenya.

Mulokozi, M., & Kahigi, K.K. (1979). *Kunga za Ushairi na Diwani Yetu*. Dar es Salaam: Tanzania Publishing House.

Mulokozi, M. M. (1996). *Fasihi.* Dar es Salaam: Dar es Salaam University Press.

Musioka, F. M. (1996). Uhakiki wa fani katika Tamthiliya Jay Kitsao.Tasnifu ya uzamili Chuo Kikuu cha Nairobi: (haijachapishwa). Nairobi, Kenya.

Ndungo, C. W., na Wafula, R. M. (1993). *Tanzu za Fasihi Simulizi.* Nairobi: University of Nairobi.

Ngesa, A. K., na Matundura, E. (2015). Mwingilianomatini Katika Tamthiliya Za Kiswahili: Mashetani Na Kijiba Cha Moyo.*Swahili Forum, 22(4),* 42 – 71.

Njogu, K., na Chimerah, R.M. (1999). *Ufundishaji wa Fasihi.* Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation

Njogu,K., na Wafula, R. M. (2007). *Nadharia Za Uhakiki Wa Fasihi.* Nairobi. Jomo Kenyata Foundation.

Ntarangwi, M. (2004). *Uhakiki wa Kazi za Fasihi*. Rock Island: Augustana College

Onchangu, R. N. (2013). *Mtindo katika Riwaya na Hadithi Fupi za Clara Momanyi.* (Tasnifu ya M.A. Kiswahili).Chuo Kikuu cha Nairobi imepakuliwa kutoka http:// erepository.uonbi.ac.ke tarehe 1/5/2017 saa 2.20 mchana

Ponera, A. S. (2014). *Utangulizi wa Nadharia ya Fasihi Linganishi.* Dar es Salam: Karljamer Print Technology.

Sarara, M. M. (1997). Maudhui katikaTamthiliya za Said.AMohamed. Tasnifu ya M A Chuo Kikuu Nairobi. (Hakijachapishwa), Nairobi, Kenya.

Salem, S. (2013). *Maudhui na Fani katika Tamthiliya za Kiswahili: Utafiti Linganishiwa Tamthiliya ya Mashetani na Kivuli Kinaishi*. Tasnifu ya Uzamivu katikaKiswahili Chuo Kikuu Huria cha Tanzania Haijachapisha. Dares Salaam, Tanzania.

Senkoro, F. E. M. K. (1982). *Fasihi*. Dar es Salaam: Press and Publicity Centre.

Senkoro, F. E. M. K. (2011). *Fasihi*. Dar es Salaam: KAUTTU LTD.

Senkoro, F. E. M. K. (1987). *Fasihi na Jamii.* Dar es Salaam: PPC.

Senyamanza, C. A. (2012). *Misingi ya Kazi za Kubuni: Nadharia Mbinu na Mifano ya kazi Bunilizi.* Dar es Salam: Karljamer Print Technology.

Too, M. (2011). Matumizi ya Lugha Katika Tamthiliya ya Nguzo Mama.Tasnifu ya Uzamili (haijachapishwa) Chuo Kikuu Nairobi, Kenya.

TUKI, (2004). *Kamusi ya Kiswahili Sanifu*. *(Toleo la 2).* Nairobi: Oxford University Press.

Wafula, R.M. (1999). *Uhakiki wa Tamthiliya: Historian a Maendeleo yake.* Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.

Wamitila, K. W. (2002). *Uhakiki wa Fasihi: Misingi na Vipengele Vyake*. Nairobi: Phoenix Publishers.

Wamitila, K. W. (2003). *Kamusi ya Fasihi Istilahi na Nadharia*. Nairobi: Focus Publication Ltd.

Wamitila, K. W. (2003). *Kichocheo cha Fasihi: Simulizi na Andishi.* Nairobi: Focus Publisher.

Wamitila, K. W. (2008). *Misingi ya Uchambuzi wa Fasihi.* Nairobi: Vide-Muwa Publishers Ltd.

Wamitila, K. W. (2010). *Kanzi ya Fasihi: Misingi ya Uchanganuzi wa Fasihi*. Nairobi: Vide-Muwa Publishers Ltd.

Wellek, R. (1988). *The Crisis in Comparative Literature.Concepts of Criticism.* London: Yale University Press.

Young, P. V. (1984). *Scientific Social Survices and Research.* Englewood Chiffs: Prentice Hall Inc.

Zepetnek, S. (1998). Comparative Literature: Theory, Methods and Application. Rodopi: Amsterdam- Atlanta. Imepakuliwa Tarehe 11/7/2016 kutoka:www.cles.org.uk/wp-www.cles.org.uk/wp-content/uploads/2011/01.